ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
43.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
44.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
45.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
47.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
48.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
49.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake

50.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

51.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

52.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

53.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

54.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

55.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

56.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

57.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

58.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

59.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

61. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

66.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

70.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

71.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

76.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tisa – Tarehe 22 Oktoba, 2012

(*Kikao Kilianza Saa 3:00 asubuhi*)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (*Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma dua*

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati Mezani Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi iliyoundwa mnamo tarehe 9 Agosti, 2011 kwa ajili ya kuchunguza mambo mbali mbali ambayo yalijitokeza kwenye Mkutano wa Nne wa Bajeti ya Wizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Utendaji wa Baraza la Manispaa Zanzibar (Mhe. Salmin Awadh Salmin): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati Mezani, Ripoti ya Kamati Teule ya Kuchunguza Utendaji wa Baraza la Manispaa Zanzibar.

Mheshimiwa naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 68

Ujenzi wa Barabara Pemba

Mhe. Suleiman Hemed Khamis – Aliuliza:-

Mwaka 2007 Wizara yako ilijikita katika mradi wa ujenzi wa barabara tatu (3) za Kaskazini Pemba nazo ni:-

(1) Barabara ya Wete - Gando

(2) Barabara ya Wete - Konde

(3) Barabara ya Wete – Chake – (njia Kongwe)

(a) Kwa nini barabara ya Wete – Chake bado haijaanzwa.

(b) Barabara ya Wete – Gando ina mwendo wa kusuasua ni sababu ipi inayopelekea kuzorota katika utendaji wake.

(c) Barabara ya Wete- Konde mwaka uliopita ilikuwa katika hali nzuri na wakati wa kutia lami pia nao ulikuwa mzuri, lakini kuna mashimo ya hapa na pale na mvua zimeharibu uzuri wa barabara. Je, Wizara inachukua hatua gani kutokana na kuzorota kwa kazi zote (3).

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (Kny. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano) – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi Nam. 68 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Wete - Chake bado haijaanzwa, hii inatokana na uhaba wa fedha na serikali ilikubaliana na *BADEA/SAUD FUND* wameipatia serikali mkopo wa dola milioni 20 za kujenga barabara hiyo na taratibu za kuanza kazi zinaendelea vizuri.

(b) Sababu zilizopelekea ujenzi wa barabara ya Wete – Gando kwenda mwendo wa kusuasua ni pamoja na kuchelewa kulipa fidia za nyumba na huduma kama vile maji na umeme kwenye eneo lote la barabara kama mkataba unavyoelekeza, kumchelewesha malipo ya Mkandarasi. Mkandarasi kubadilisha wafanyakazi waandamizi na kuharibika kwa baadhi ya vifaa vya Mkandarasi vya kutendea kazi.

(c) Mkandarasi kwa sasa anaendelea kuzirekebisha sehemu zilizoharibika ikiwa ni matayarisho ya mwisho wa kuanza kutia lami ya maji ikifuatiwa na lami ya mwisho.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, naomba niulize swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Barabara ya Wete – Gando, barabara ya Wete – Konde na Barabara ya Wete – Chake, alikabidhiwa kampuni ya *MECO* kuzijenga barabara hizi. Lakini mara tu tukapata taarifa kwamba barabara ya Wete – Chake, amekabidhiwa kampuni nyengine baada ya miaka kadhaa kupita.

(a) Mhe. Waziri nini sababu ya kupokonywa kwa ujenzi huo.

(b) Atakubaliana nami Waziri kwamba kampuni hii haifai kuendelea kupewa tenda kutokana na uzoroteshaji wa kazi zake zinazopita muda wa makubaliano pamoja na kuhatarisha afya ya jamii kutokana na vumbi kali ambalo linaharibu afya ya jamii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (Kny. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Mwenyekiti, naomba arudie swali lake la pili sikulielewa vizuri.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Waziri nafikiri atakubaliana nami kwamba kampuni hii haifai kuendelea kupewa tenda kutokana na uzoroteshaji wa kazi zake zilizopita muda wa makubaliano, pamoja na kuhatarisha afya ya jamii ambalo ni vumbi kali la muda mrefu ambao watu wengi wamepata athari ya vumbi hilo. Ningeomba masuala hayo yajibiwe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (Kny. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Mwenyekiti, Suala la tenda linataratibu zake za kisheria. Vile vile suala la ujenzi kwa Mkandarasi na kwa yule anayejengewa kwa maana ya serikali nalo limewekewa utaratibu. Wakati mwengine ucheleweshaji wa ujenzi inawezekana kabisa ukatokana na Mkandarasi. Lakini vile vile inawezekana ukatokana kwa serikali yenyewe ama yule ambae ameahidi kuisaidia serikali kwa maana ya msaada kwa wakati huo au kwa maana ya mkopo. Hii maana yake ni kwenye masuala ya malipo.

Kutokana na vifungu vya mkataba ndivyo vile wakati mwengine vinasababisha ujenzi. Kwangu kwa wakati huu kusema Mkandarasi ndiye mwenye makosa inaniwia vigumu. Mambo haya yana utaratibu wake wa kisheria inabidi ipitie zile taratibu mlizokubaliana na kwa msingi huo kwa kuwa bado serikali inaendelea na mazungumzo na Mkandarasi huyu. Vile vile mkandarasi huyu naye hulalamika kwa upande mwengine kwa kutopata malipo kwa wakati. Ni vigumu kusema kwamba yeye moja kwa moja ndiye aliyechelewesha jambo hili.

Lakini nataka niwahakikishie Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe kwamba serikali itachukua hatua ya kuwasiliana na Mkandarasi ili kuhakikisha kwamba kazi hii inafanyika. Na pale ambapo pataonekana pamekiukwa kwa mujibu wa Mkataba basi hatua za kisheria zitafuata ili kuhakikisha maslahi na pato la nchi hii linalindwa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumuuliza swali moja la nyongeza.

Katika majibu yake Mhe. Waziri amesema barabara ile haijaanza kutokana na uhaba wa pesa. Lakini je, serikali ni lini itapata wingi wa fedha ili ianze barabara ile ili kuondoa usumbufu wa barabara hiyo kwa wananchi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (Kny. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Mwenyekiti, sikusema kama kazi ile haikuanza kwa sababu ya uhaba wa pesa. Nilichosema ni kwamba Mkandarasi analalamika na yeye kwamba hajapata pesa zake kwa wakati.

Ni kwamba kazi ile imeanza lakini kama nilivyosema awali kwamba katika masuala mazima haya ya tenda kuna mfanyaji kwa maana ya *contractor* na yule anayefanyiwa kwa maana ya serikali. Vile vile kuna *financer* kwa hivyo panapotokea kucheleweshwa kwa upande mmoja katika maeneo haya matatu ndio ucheleweshaji wa ujenzi wakati mwengine hutokea.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ile imeanza kwa sasa na inaendelea lakini si kwa kasi inayotakiwa. Jambo la msingi hapa kwa serikali kukaa pamoja na wahusika wote hawa wakiwemo Wakandarasi na wale wanaosaidia mradi huu, ili kuhakikisha fedha zinapatikana kwa wakati na ujenzi uendelee ili kuondoa usumbufu unaotokea yakiwemo ya maradhi kama Mhe. Hemed alivyoainisha.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, siku za nyuma wakati barabara ya Mkoani /Chake ilipokuwa ikitengenezwa mimi nilikuwa Waziri Kivuli wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa wakati ule, nilipiga kelele sana kuhusu kampuni hii ya Prisimo, lakini serikali ilikuwa ikiisifu tu. Lakini kampuni ile ile ilivyokuja hapa Unguja haikumaliza kazi ikafukuzwa moja kwa moja, kuthibitisha kuwa nililokuwa nikisema ni kweli, lakini walikuwa wakisaidiwa.

Si bora Mhe. Waziri kwa hili wakati tuna hii barabara ya Wete/Chake inataka kutengenezwa kuchukua maelekezo kuwa hili suala utalifatilia kwa undani ili upate jibu sahihi ili tujue hali halisi ya Mkandarasi huyu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (Kny. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na ushauri wa Mhe. Salim Abdalla Hamad wa kutaka suala hili lifatiliwe kwa undani kwa sababu ujenzi wa barabara hizi una umuhimu sana kwa wananchi wetu na kwa hiyo tutawasiliana na Waziri muhusika ili hatua zichukuliwe na ujenzi wa barabara uendelee na tatizo pale lilipo liweze kutatuliwa.

Nam. 69

Ujenzi wa Barabara Msitu wa Ngezi

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 10

Kuuzwa kwa Mafuta Machafu

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Katika kipindi cha mwezi wa Juni na Julai 2012, vituo vya kuuzia mafuta (Diesel na Petrol) katika mji wa Chake Chake vilikuwa vikiuza mafuta machafu na yenye maji pamoja na kwamba mafuta hayo yalikuwa yakichukuliwa Wesha (*Depot* ya Serikali) jambo ambalo lilisababisha hasara kubwa kwa wenye magari ikiwa ni pamoja na kuharibika kwa *Injector Pumps* za magari yao.

Je, Mhe. Waziri ni nani wa kulaumiwa katika kadhia hii.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekitia, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 kama hivi ifuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwezi wa Februari na Machi 2012 kulijitokeza matatizo ya mafuta machafu hapa Zanzíbar pamoja na Tanzania kwa ujumla. Hii ni kutokana na mafuta ambayo yaliagizwa kupitia utaratibu mpya uliowekwa na Tanzania Bara na *Bulk Procurement*. Mafuta hayo yalikuwa na kiwango kikubwa cha *Methanol* na *Echenol* ambazo hutumika katika nchi za Ulaya ili kupunguza utoaji wa gesi mkaa (*carbon*) kwenye gari zao. Tatizo hilo lilimalizika baada ya kutambulika kwamba mchanganyiko huo husababisha mafuta kuharibika pindipo yakigusana na maji.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwenyekiti swali lake kama hivi ifuatavyo:-

Mafuta yanayoingia Zanzíbar (Unguja na Pemba) kupitia *Depot* za Mtoni na Wesha kwa hivi sasa hayana matatizo hayo tena. Matatizo ya mafuta machafu katika mji wa Chake Chake Pemba huenda kuwa yamesababishwa na wauzaji wa rejareja katika vituo vyao. Kwani baadhi ya wafanyabiashara wa mafuta ya petrol huchanganyisha mafuta aina mbili tafauti (kama vile mafuta ya taa na mafuta ya diesel au petrol na mafuta ya taa) ili kujipatia faida kubwa.

Hata hivyo tunashauri kuwa, kama kutakuwa na wasiwasi wa kuharibika kwa mafuta tunaomba uchukuliwe sampuli ya mafuta hayo na kuipeleka sehemu husika (kwa Pemba, Wizarani) na kueleza kituo gani ambacho kinasababisha matatizo na Idara husika itafuatilia na kujuwa chanzo cha uchafuzi huo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa tuna ushahidi kwamba mafuta haya yalitoka katika kituo cha Wesha yakaingizwa katika *pumping stations* zilizopo Chakechake. Yaani ni mafuta yaliyotoka katika kituo cha Serikali. Na kwa kuwa katika kipindi hichi magari mengi yaliharibika *injector pumps* na kusababisha hasara kubwa kwa wenye magari haya.

Je, serikali iko tayari kufidia gharama, kushindwa kufidia gharama za magari yake na wakati serikali imesababisha gharama ile si kuwadhulumu wananchi wa nchi hii. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nilisema katika jibu langu la msingi kwamba katika kipindi hicho tatizo lililojichomoza ni kwamba mafuta hayo yalikuwa yana *echenol* na *methanol* ambazo hutumika huko Ulaya. Hapa kwetu tunaweka mafuta kwenye maji kama nyalio zake, kwa hivyo yakichanganyika haya huwa yanaharibika na yanakuwa *contamínate* na yanakuwa yanaleta matatizo. Hili tatizo nimelikubali kwamba limetokea na sasa wananchi nawajulisha kwamba hili tatizo limetokea lakini tumejaribu kuchukua *control* ya kwamba hayatatokea tena masuala haya katika kipindi hichi kama nilivyokwisha kumjibu mwanzo.
Sasa anapozungumza suala la kufidia hiyo itakuwa ni kazikubwa sana, maana hutomjua yupi mkweli na hupi si mkweli maana tutaingia kwenye gharama kubwa sana. Kwa hivyo tuwaombe radhi wananchi kwamba hili lilitokea na tunajitahidi kwamba lisitokee tena.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kuweza kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri.

Pamoja na majibu yako mazuri Mhe. Waziri hivi karibuni tulikwenda kama Kamati Pemba na tukalikuta suala hilo na tukawaita hao watu wa kituo cha Wesha na tukawaita na wawekezaji. Lakini kilichojitokeza pale Mhe. Waziri ni suala ambalo sasa hivi kuwa magendo yamekuwa mengi Pemba.

Je, suala hilo Mheshimiwa unalionaje? Huoni kama upo haja ya kuweka mikakati kama tulivyoweka mkakati wa karafuu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, sikulipata vizuri swali lake naomba alirejee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Waziri kilichojitokeza kule Pemba ni gari moja ya Polisi ndio iliyopata maharibiko kutokana na huu mchanganyiko wa mafuta. Lakini zaidi kilichojitokeza ni kuwa na magendo makubwa ambayo yanafanyika sasa hivi Pemba ya mafuta ndiyo yanayosababisha kuelekea kuchanganywa.

Je, Mhe. Waziri tuko tayari kuweka mkakati ambao kama tulivyokuwa tukiweka karafuu ili mafuta yasiletwe kimagendo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, moja katika tatizo la uagiziaji mafuta visiwani Unguja na Pemba ni magendo. Na sisi tunajitahidi sana kupita vita suala hilo la magendo ya mafuta. Kwa sababu Mheshimiwa unaweza ukashangaa sana kwamba hawa wanaochukua mafuta ya magendo sidhani hata kama wanafikiria kama haya mafuta wanakwenda kuyauza kwenye magari. Kwa sababu haiwezekani kwamba mashua inakuwa kama ndio tangi la kuchukulia mafuta yaani wanajaza mafuta ndani ya ile mashuwa yenyewe na mashuwa inapita kwenye maji na hii inasababishia matatizo kwamba yale mafuta yanachanganyika na maji wakati wa kuchukua namna kama hiyo.

Mimi nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba nitajitahidi kuona kwamba tunazidi kupambana na magendo. Naomba na Wawakilishi waliokatika sehemu hizo watusaidie. Kuyatia mafuta kwenye ngwanda yaani boti ile kwa kweli ni kuyafanya mafuta yachanganyike na maji na wenyewe ukiwauliza watu mafuta wanakwambia ni kweli. Kuna mafuta yanakuja ndani ya boti kabisa yaani hayamo ndani ya tangi wala ndani kitu chengine chochote yaani yamo ndani ya ile boti yenyewe ndimo yanamotiwa mafuta mle. Hili tatizo ndilo tulilokuwa nalo. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona na naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, naomba kujua ni nani hapa Zanzibar mwenye wajibu wa kujua na kupima kiwango na ubora wa mafuta.

(b) Wakati mafuta yanapotokezea tatizo ama uchafu au kuadimika, Wizara ya Fedha na Wizara ya Maji huwa inatupiana mpira kwamba kila mmoja anakwepa kulaumiwa. Ni nani hasa anaewajibika kulaumiwa kati ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Maji na kama hakuna anaewajibika kulaumiwa kwa nini hatuundi chombo maalum cha kudhibiti uingiaji wa bei na ubora wa mafuta hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kimuundo wa serikali wizara yenye dhamana na suala la mafuta ni Wizara ya Maji, Nishati na Ardhi ndiyo yenye dhamana. Katika Wizara hii kuna Idara ya Nishati ndiyo inayoshughulikia masuala haya na ndio waliotoa majibu haya ambayo sasa hivi nimeyajibu.

Najua kwamba kuna sheria tunaileta hapa mpya itakayohakikisha kwamba kwa mujibu wa sheria sasa Idara ya Nishati ndiyo itakayokuwa na jukumu moja kwa moja la suala la kuingiza mafuta, kusambaza mafuta na mambo mengine, ambayo Waheshimiwa ikiletwa sheria hiyo waiunge mkono ili tuweze kufanya kazi vizuri zaidi kwa mujibu wa sheria.

Nam. 31

Ufungaji wa Mita za Maji Makadara

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Shehia ya Makadara Jimbo la Rahaleo ni eneo la mwanzo kufanyiwa majaribio ya kuwekwa mita za maji, na wakati zilipowekwa mita hizo wananchi walitakiwa kulipa Shs. 2,000 kwa mwezi na mita zinapoharibika hulipishwa fedha za matengenezo ya mita hizo.

(a) Mhe. Waziri, Je, ni sababu zipi zilizofanya kulipishwa zaidi ya shs. 15,000 kwa mwezi.

(c) Ni sababu gani zinazopelekea kuwalipisha wananchi Shs. 50,000 pale mita hizo zinapoharibika ukizingatia hali ngumu za maisha ya wananchi wetu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 31 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kutoa ufafanuzi juu ya hoja ya Mhe. Mwakilishi kwamba serikali kupitia Wizara yangu kwamba inawalipisha fedha wananchi kwa ajili ya matengenezo ya mita kila zinapovunjika.

(a) Mhe. Mwenyekiti, aidha ZAWA ilianza utaratibu wa kuchangisha huduma ya maji kwa kila mwananchi anaepata maji kwa utaratibu wa *"flate rate"* wa Shs. 2000/= kwa mwezi, lakini kwa sasa ZAWA imeanza na utaratibu wa kuwafungia wananchi mita za maji kwa baadhi ya maeneo ikiwemo Shehia ya Makadara katika Jimbo la Rahaleo, hivyo malipo ya maji kwa waliofungiwa mita *(volumetric)* yanaweza kuwa Shs. 15,000/= kwa mwezi au zaidi ya shs. 15,000/= au chini ya shs. 15,000/= ambapo hutegemea matumizi ya mteja husika. Hivyo napenda kumthibitishia Mhe. Mwakilishi kwamba ZAWA haina utaratibu wa kuwalipisha wananchi zaidi ya Shs. 15,000/= kwa mwezi.

(c) Mhe. Mwenyekiti, napenda kutokubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inawalipisha wananchi Shs. 50,000/= pale mita zinapoharibika. Ukweli ni kwamba gharama za ununuzi wa mita moja ni zaidi ya Shs. 50,000/=, lakini ZAWA inafidia gharama kwa kuwatoza wananchi kiwango cha Shs. 50,000/= kama ni gharama za ununuzi wa mita hizo.

KAULI ZA SERIKALI

Taarifa ya Serikali Kuhusu Utekelezaji Ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi Iliyoundwa Mnamo Tarehe 9 Agosti, 2011 kwa Ajili ya Kuchunguza Mambo Mbali Mbali ambayo Yalijitokeza kwenye Mkutano wa Nne wa Bajeti ya Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2011/2012

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza niombe radhi kwa makosa yaliyojitokeza katika *printing* zetu ya kabrasha hili zinavyoonyesha hatua ama maamuzi ya serikali. Lakini katika kipindi kifupi litakuwa limewasili kabrasha hapa ndani ili kuwasilisha badhi ya *copy* na zitaanza kugawiwa kwa wajumbe. Kwa hivyo niombe radhi sana kutokana na hiyo hali iliyojitokeza ya bahati mbaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutuwezesha tena kukutana hapa katika kikao hichi kitukufu kuweza kuzungumza mambo muhimu yanayohusu nchi yetu na kufanya shughuli zetu za kawaida za kibaraza.

Aidha nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kutoa taarifa ya serikali kuhusu Ripoti ya Kamati Teule ya Baraza lako tukufu. Pia nilishukuru Baraza lako tukufu kwa maamuzi sahihi yaliyochukuliwa katika kuunda Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi kufuatia hoja mbali mbali zilizoibuka ndani ya Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kueleza zaidi ningependa pia niseme jambo moja ambalo linajitokeza sana, ambalo huwa halileti sura nzuri kwa mustakbali wa nchi yetu. Mara nyingi tunapowasilisha taarifa hizi za serikali huwa za maamuzi ya pamoja na serikali na si ya mtu binafsi kama ambavyo watu wengi sasa hivi huko nje au baadhi ya watu husema hii ni taarifa ya fulani. Taarifa zinazokuja hapa ni za serikali. Mimi kwa *nature* yangu ya kazi ndio ninawasilisha kwa yale ambayo yanahusu Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa niaba ya Makamo wa Pili wa Rais. Ningependa wananchi watuelewe kwamba taarifa huwa sio ya mtu binafsi, sio yangu, sio ya Muhammed Aboud ni taarifa ya Serikali ya Zanzibar na inapitishwa rasmi na Baraza la Mapinduzi na hapa kazi yangu mimi ni kusoma kama ilivyoamuliwa.

Mhe. Mwenyekiti baada ya maelezo hayo naomba pia niwapongeze sana Mwenyekiti wa Kamati Teule na Wajumbe wote wa Kamati Teule kwa kazi kubwa na nzuri waliyoiibua mambo mbali mbali ambayo yenye nia ya kujenga nidhamu, uwadilifu na utumishi wa umma. Hiyo kumedhihirisha wazi kuwa Baraza la Wawakilishi ni kiyoo cha wananchi na ni watetezi wa wananchi ni watetezi wa kufichua maovu pale yalipo.

Nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwafanya viongozi wetu sote na watendaji sote tubadilike na tuache kufanya kazi kwa mazoea na tufanye kazi kwa kufuata na kutii uwadilifu, sheria na matokeo yake yawe ni ufanisi na tija.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kutoa shukurani hizo za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, serikali imepokea ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi iliyotaka kuifanyia kazi na kuchukua hatua mbali mbali kuhusiana na masuala yaliyojitokeza katika ripoti ya Kamati hiyo. Serikali imezingatia ripoti hiyo kwa msingi wa haki, uadilifu bila ya upendeleo wowote.

Serikali inaamini kwa dhati kabisa, kwamba msingi wa *cheque and balance* ndio uliotumika kutoa ripoti ya Kamati Teule ili kuona kuwa kila upande unatekeleza wajibu wake ipasavyo na maamuzi yatakayochukuliwa yawe na manufaa kwa nchi hii na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti baada ya serikali kuipitia ripoti hii kwa undani na kuifanyia kazi kila hoja, ili yale yote yaliyoonekana na Wajumbe wa Kamati Teule yaweze kufanyiwa kazi ipasavyo. Kwa ufupi mambo yaliyojitokeza tunaweza kuyagawa katika makundi manne makubwa kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti kundi (A) kundi la kwanza ni mambo yanayohusu ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu za utendaji ingawa Kamati hawakuyatolea mapendekezo mahsusi, lakini yameyatanabahisha serikali juu ya kasoro hizo. Mambo mengi ya namna hii yamekuwa yakifanyika serikalini kutokana na kufanya kazi kwa mazoea, kulikokuwa na nia ya kuvunja sheria. Hata hivyo baadhi ya mambo hayo yanaweza kutengeneza mianya ya rushwa, kukosa uadilifu na mambo mengine yasiyofaa katika utendaji wa serikali. Hivyo serikali imeyachukulia hatua zinazofaa mambo ya aina hii pamoja na kuna mapendekezo mahsusi ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi.

(B) Kundi la pili ni mambo yanayohusu tuhuma za ukiukwaji wa sheria na taratibu, lakini Kamati Teule haikuweza kuthibitisha kwa kiwango kinachostahiki za kuchukuliwa hatua za kiutawala. Mengi ya mambo katika kundi hili yametokana na tafsiri ya sheria ambayo Kamati Teule imetoa na ambayo serikali imeona umuhimu wa chombo cha kutafsiri sheria kufanya kazi yake. Hivyo ni wazi kuwa hitimisho baina ya Kamati Teule na serikali litakuwa na mtazamo tofauti katika kundi hili.

Serikali inahisi si vyema kuchukua hatua za kiutawala moja kwa moja bali ni vyema kuchukua hatua za kisheria kwanza kupitia vyombo vya sheria kama vile Mahkama kabla serikali kuchukua hatua za kiutawala kuhusiana na mambo hayo.

(C) Kundi la tatu ni mambo ambayo tuhuma zimethibitishwa kwa kiwango kinachohitajika. Hata hivyo kutokana ama kuwepo mikataba au hatua nyengine ambazo zilichukuliwa na wahusika, serikali haiwezi kuchukua hatua za kuvunja mkataba au kufuta maamuzi yake ili kuepusha hasara na gharama kubwa ambayo serikali ni wazi itazipata ikichukua hatua hizo.

(D) Kundi la nne ni mambo ambayo Kamati Teule imeyathibitisha kwa kiwango kinachohitajika na Serikali imechukua hatua ama za kiutawala ama imeanzisha utaratibu wa kuchukua hatua za kisheria kama ilivyoelekezwa na Ripoti ya Kamati Teule. Hata hivyo katika kupitia ripoti hiyo mbali na mengi mazuri yaliyopendekezwa na Kamati Teule kwa serikali ambayo serikali imeyachukulia hatua na mengine inaendelea kuyafanyia kazi kama ilivyoelekezwa hapo juu, pia kuna kasoro zilizojitokeza ndani ya ripoti hiyo ya Kamati Teule ambazo serikali inahisi ni vyema kuzitanabaisha kwa nia ya kujenga msingi bora zaidi kwa kazi za Kamati Teule pale zinapoundwa. Miongoni mwa kasoro hizo ni kama zifuatazo:-

Baadhi ya maelezo mbali mbali ya watendaji mbali mbali wa serikali ambao walihojiwa na Kamati hiyo hayakuzingatiwa katika ripoti hiyo, hivyo Kamati iliegemea zaidi kutumia baadhi ya taarifa katika kufikia maamuzi ya hoja zake. Jambo ambalo lilipelekea baadhi ya mambo katika ripoti hiyo kuonekana kuwa ya upande mmoja na kutosikilizwa watendaji ambao wametoa taarifa zao.

Katika matumizi ya lugha katika baadhi ya vipengele hayakuzingatia kanuni za Baraza za kutunza heshima na nidhamu ya viongozi wakuu wa nchi, mfano katika ukurasa wa 17 wa ripoti naomba ninukuu. “Aidha hata kama tunaamini kwamba imeamuliwa na Rais basi ni wazi kwamba hata huyo Rais hafahamu utaratibu wa utekelezaji wa

maagizo yake". Kitu ambacho kwa upande wa mtu mwenye akili timamu hawezi kukubaliana na usahihi wa barua hiyo kutoka kwa Mhe. Rais.

Lugha iliyotumika hapa juu ya kuzungumzia Kiongozi mkuu wa nchi kuwa hafahamu utaratibu wa maelezo yake kwa kiasi kikubwa imekwenda kinyume na vifungu vya 59(6) na 59(8) (a) vya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2012 zinapunguza heshima na nidhamu kwa viongozi wakuu wa nchi yetu.

Baadhi ya tafsiri ya sheria iliyotolewa katika ripoti ni dhahiri kuwa hazikwenda na maana halisi ya sheria husika, na hilo lilipelekea kutoa uamuzi au ushauri ambao haulingani na sheria husika. Mfano mzuri ni tafsiri ya kifungu cha 49(1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambayo kama ilivyo katika ukurasa 17 ripoti ya Kamati Teule imekosewa, jambo hilo pia lilipelekea kukosea katika ushauri uliotolewa na ripoti ya kifungu hicho, kinazungumzia kazi za Katibu wa Baraza la Mapinduzi zinazotokana na maagizo na maamuzi ya Baraza la Mapinduzi na sio shughuli za kila siku za Mhe. Rais kama ilivyoelezwa na Kamati Teule, kiutaratibu shughuli za kila siku za Mhe. Rais hufanywa na Katibu wa Rais, *private secretary* wake.

Imebainika pia Kamati Teule pia ilijiongezea hadidi rejea ambazo hazikuwemo katika hadidu rejea walizopewa na Baraza la Wawakilishi. Jambo hili ni kinyume na kifungu cha 121 (4) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, jambo hili lilitokana na tafsiri isiyo sahihi ya hadidu rejea za msingi. Hivyo kiutaratibu mambo hayo waliyojiongezea hayakupaswa kujadiliwa.

Baadhi ya ushauri uliuotolewa na Kamati Teule unaweza kukiuka taratibu na jukumu la mihimili mengine kinyume na kifungu cha 5(a) kidogo cha 3 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kwa mfano katika hadidu rejea tisa inayozungumzia mikataba ya umiliki wa nyumba, pendekezo lililotolewa na Kamati Teule haliwezi kutekelezeka kwa hatua za kiutawala kwa vile inapotokea kubishana juu ya hoja ya kisheria ni vyema suala hilo kuamuliwa na mahkama kwanza kabla hatua za kiutawala kuchukuliwa. Ingawa Kamati ina mamlaka ya kutoa maoni ya uhalali wa mikataba, lakini ni dhahiri kuwa chombo chenye mamlaka ya kuamua kama mkataba ni halali au batili ni mahkama.

Hata hivyo Kamati kwa upande wake imeeleza kwamba kwa vile mikataba hiyo ni batili, basi Ndugu Juma Ali Kidawa alipwe milioni ishirini ili ziweze kumsaidia kujinasua kimaisha. Ni dhahiri kuwa kama ushauri wa Kamati utafuatwa moja kwa moja, anayetakiwa kuchukua hatua ya kulipa fidia hiyo, hawezi kutakiwa kufanya hivyo kwa uamuzi wa kiutawala, bila ya shauri hilo kuanza kuamuliwa na mahkama labda aamue kufanya hivyo kwa hisani na sio kwa amri ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa uniruhusu kutoa ufafanuzi wa serikali wa kutokana na hoja mbali mbali zilizojitokeza katika ripoti hii kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti tukianza na hoja ya kundi la kwanza, maelezo ya tuhuma yanahusu kuna ukiukwaji mkubwa wa sheria na taratibu na uuzaji wa mali za serikali. Mhe. Mwenyekiti nitasoma kwa ufupi kwenye hoja hii ya mwanzo ya tuhuma ili niisome vile vile kwa ufupi maelezo ya Kamati Teule, halafu niisome kwa ukamilifu yale maelezo ya serikali.

Kwenye hoja hii, mapendekezo ya Kamati Teule yalikuwa kama ifuatavyo:
Moja, aliyekuwa Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi mwaka 2005/2010 na watendaji wote waliohusika katika kuingia mkataba wa Kampuni ya Coastal Fast Ferry Limited wawajibishwe kwa misingi ya sheria.

Hoja ya pili Kamati inapendekeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Miunduombinu na Mawasiliano waliombe radhi Baraza la Wawakilishi kwa kutaka kulipotosha Baraza juu ya ukweli wa uuzaji wa kiwanja kilichozungumziwa katika hoja hii, aidha watendaji mbali mbali wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wachukuliwe hatua kwa misingi ya sheria namba 4 ya mwaka 2007 hatua zinazofaa kwa kosa na kuzidanganya Kamati za Baraza la Wawakilishi.

Tatu, Baraza lichukue hadhari kubwa na matumizi ya jina la Mhe. Rais na Ofisi yake.

Nne, Katibu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano achukuliwe hatua za kinidhamu kwa kutosimamia ipasavyo mali ya Serikali iliyo chini ya Wizara yake ambapo kwa mujibu wa sheria na Kanuni za Fedha ya sheria namba 12 ya mwaka 2005 ya kanuni zake yeye ndie msimamizi mkuu.

Tano, uhaulishwaji huu si halali kisheria na kiutawala, hivyo Kamati inapendekeza kiwanja hicho kirejeshwe serikalini mara moja.
Sita, kuna utumiaji mbaya wa madaraka ya Ofisi ya Rais.
Saba, kuna matumizi mabaya ya fedha.

Nane, kukiukwa ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Baraza.
Tisa, Mawaziri kuingilia majukumu ya Makatibu Wakuu wa Wizara zao, na
Kumi, ukiukwaji wa maagizo ya maelezo ya serikali.

Kuna baadhi ya vifungu Mhe. Mwenyekiti havikutolewa maelekezo na Kamati Teule lakini kwa vile ni mambo ya msingi yaliyoibuliwa na Kamati Teule Serikali ilitoa maelekezo kama ifuatavyo:

Kuhusu Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu kilichopo Mtoni umefuatwa utaratibu wa kiutawala na kisheria, kwani Wizara kabla ya kuhaulisha ilimuandikia barua Mhe. Rais yenye kumbukumbu namba MWMU/MM/J/VOL.V 027 ya tarehe 5 Oktoba, 2010 kutaka ridhaa ya Mhe. Rais na Mhe. Rais hakuwa na pingamizi juu ya suala hili.
Kwa mujibu wa sheria ya ardhi, ardhi yote ipo chini ya mamlaka ya Rais kifungu cha 3 cha sheria namba 2 ya mwaka 1992 kinaeleza.

Aidha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano iliiandikia barua Wizara inayohusika na masuala ya ardhi yenye kumbukumbu MWMU/MM/J/VOL.V 028 ya tarehe 11 Oktoba, 2010 kuhusu kukamilisha taratibu za uhaulishaji na Wizara ya Ardhi ndio inayosimamia uhaulishaji wa kiwanja hicho.

Hata hivyo suala linaloweza kuhojiwa ni kigezo gani kilitumika katika kutathmini ardhi inayohusika, hasa ikizingatiwa ukubwa wa eneo la kiwanja hicho ni mita za mraba 7900 na ikilinganishwa na thamani ya shilingi milioni 200 iliyokadiriwa. Kinachodhihirika hapa ni kuwa hakuna utaratibu wa kisheria wa kufanya tathmini uliofuatwa, kutokana na kutowepo kwa tathmini ya ardhi, serikali imeona kasoro hii na hivi sasa wizara inayohusika inaendelea na hatua ya kuandaa sheria ya tathmini ya ardhi.

Aidha ni vyema ikafahamika kwamba hakuna fedha zozote ilizolipwa wizara husika kwa kiwanja hicho, kwani makubaliano yalikuwa ni kujenga na sio kupokea fedha. Suala la kumwajibisha mtu yoyoyote kwa kosa la kudanganya linahitaji uthibitisho usio shaka kama kweli muhusika tangu awali alikuwa na dhamira ya kudanganya.

Serikali inaamini kwamba Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano hawakudhamiria tangu mwanzo kulidanganya Baraza na hata watendaji nao pia hawakudhamiria kulidanganya Baraza. Kila mmoja wao alijibu kwa kadri ya suala husika alivyolielewa. Hata hivyo kama bado kuna shaka na dhana kwa Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri na watendaji wengine walikuwa na dhamira tangu mwanzo ya kudanganya, basi ni vyema utaratibu wa kisheria ukafuatwa kwa kuwasilisha tuhuma hizo kunakohusika, ili uchunguzi ufanyike na ikithibitika sheria iweze kuchukua mkondo wake, ikiwa ni pamoja na kuwafikisha wahusika mahkamani kujibu tuhuma hizo.

Hata hivyo ni vyema ieleweke kuwa kwa kawaida shughuli za kiutendaji za kila siku ikiwemo kujibu barua mbali mbali anazopelekewa Mhe. Rais, hujibiwa na Katibu wa Rais *private secretary* kwa maelekezo anayopewa na Mhe. Rais. Kwa hivyo hakukuwa na ukiukwaji wa taratibu au matumizi mabaya ya Ofisi ya Rais, kwa kuwa Katibu wa Rais alijibu barua iliyokwenda kwa Mhe. Rais baada ya kupokea maelekezo kutoka kwa Mhe. Rais. Na kufanya hivyo ni miongoni mwa majukumu yake ya kila siku.

Aidha ikumbukwe kuwa Mhe. Rais hazuiliki kumpa maelezo mtu yoyote kutekeleza jambo liliopo ndani ya mamlaka yake.

Kuhusu suala la matumizi, ni suala lililo wazi kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilipatiwa jumla ya shilingi milioni arobaini na tisa na laki moja kati ya shilingi milioni mia moja walizoziomba kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi yake ya kudumu. Hata hivyo fedha hizo hazikutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa, na Wizara inakiri kutumia fedha hizo kwa ajili ya kukarabati majengo ya Bohari Kuu ambayo kwa sasa ndio inayotumika kama Ofisi ya Wizara hiyo.

Wizara hiyo imeeleza kwamba waliamua kufanya hivyo kwa nia njema kutokana na dharura iliyojitokeza ya kuharibikiwa na jengo lililokuwa Makao Makuu ya wizara. Hapana shaka juu ya matumizi ya fedha hizo, bali shaka iliyopo ni utaratibu uliotumika kuzitoa fedha hizo kutoka kifungu kimoja kwenda kifungu chengine. Ni dhahiri kwamba utaratibu wa uhaulishaji, *reallocation* wa vifungu vya fedha haukufuatwa kikamilifu. Serikali itachukua hatua za kinidhamu kwa Afisa Mhasibu anayehusika kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma, wakati huo huo kuwataka na kuwahimiza maofisa na wahasibu wote kufuata sheria na kanuni za fedha kikamilifu.

Uhaulishaji wa kiwanja cha Mtoni hauna shaka umefuata utaratibu wa sheria za kiutawala kama ilivyoelezwa katika kifungu cha kwanza hapo juu. Hata hivyo tunapenda kutoa taarifa kwamba baada ya kutokea malalamiko ya kiwanja hicho aliyepewa kiwanja hicho ameamua kukirejesha serikalini na sasa watapewa Baraza la Mitihani la Taifa.

Majukumu ya Mawaziri na Makatibu Wakuu yameelezwa wazi katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Toleo la 2010 ibara ya 50(1) kwamba Katibu Mkuu wa wizara ndie atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wizara, wakati huo huo Katiba imebainisha majukumu ya mawaziri. Kwa mnasaba kila mmoja katika viongozi hao ana jukumu lake. Aidha serikali ya awamu ya saba imelipa uzito unaostahiki suala hili kwani kikao cha kwanza cha Baraza la Mapinduzi kilizungumzia kuhusu majukumu ya Waheshimiwa Mawaziri, Naibu mawaziri na Makatibu Wakuu kama ilivyoainishwa katika Katiba na ikasisitizwa tena katika semina za viongozi wanasiasa na watendaji wakuu wa serikali iliyofanyika mwezi Mei, 2011.

Serikali ina imani kwamba viongozi wote sasa wanajua majukumu yao na haitarajii kutokea kwa makusudi suala la kuingiliana katika utekelezaji wa majukumu baina ya mawaziri na Makatibu Wakuu. Na itakapotokea hatua zitachukuliwa mara moja.

Kuhusu wananchi walioathirika na ujenzi wa uzio wa Uwanja wa Ndege haukufuata taratibu za kisheria. Hoja hii ilitolewa mapendekezo na Kamati Teule kama ifuatavyo:-
Hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya watendaji waliohusika na malipo ya fedha za fidia walioathirika na ujenzi wa uzio kutokana na watendaji hao kutofuata ipasavyo taratibu za malipo hayo kwa mujibu wa sheria za fedha namba 12 ya mwaka 2005 pamoja na kanuni zake.

Mwananchi ambaye bado hajalipwa fidia Ndugu Ali Mwinchande Simba alipwe fidia yake kwa mnasaba wa thamani ya mali zake wakati tulionao sio tena wakati uliopita. Kwa sababu tokea muda uliofanywa tathmini hadi leo maisha yameshabadilika na thamani halisi ya nyumba yake imebadilika.

Kwa kutumia kanuni za Baraza la Wawakilishi Kamati inapendekeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Miundombinu na mawasiliano, waliombe radhi Baraza la Wawakilishi, kutoa maelezo yasio ya kweli kuhusiana na ulipwaji wa fidia kwa wananchi walioathirika na ujenzi wa uzio uwanja wa ndege. Hatua zinazofaa kwa mujibu wa sheria namba 4 ya mwaka 2007 zichukuliwe kwa watendaji wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, waliohusika na upotoshaji wa Kamati kwa kutoa taarifa zisizo za ukweli.

Maamuzi ya Serikali. Kifungu cha 1994(1) cha Kanuni za fedha za umma, kinaelekeza kwamba anaelipa fedha za serikali analazimika kuweka alama za dole ikiwa hawezi kuandika. Hii ni kusema kwamba kifungu hiki kinamtaka anayeweza kuandika lazima a-sign kwa maandishi. Utaratibu huo umefuatwa kikamilifu na walipaji wa fidia kwa wahusika. Watu wote waliolipwa wametia *sign* katika vocha za malipo na vocha ambazo zimeonekana hazina *sign* ni zile ambazo wahusika hawakujitokeza kuchukua fedha zao, licha ya kuwa wametangaziwa mara kadhaa.

Ndugu Ali Mwinchande Simba ndiye aliyetajwa ni mwananchi aliyekuwa hakulipwa fedha zake za fidia, suala hili linafafanuliwa kuwa muhusika alikuwa na fidia za aina mbili, ile ya mazao na ya pili ya nyumba. Ndugu Mwinchande alipokea fedha zake za fidia ya mazao kama wenziwe mara tu fidia hiyo ilipolipwa ambazo ni shilingi milioni ishirini, laki tisa sitini na tano elfu na mia tatu.

Aidha fedha kwa ajili ya fidia za nyumba pia zilikuwa zipo tayari na wahusika walikwenda kuzichukua lakini Ndugu Mwinchande alikataa kuzipokea fedha hizo kwa sababu anazozijua yeye mwenyewe. Hata hivyo kabla ripoti ya Kamati Teule haijawasilishwa na Baraza la Wawakilishi, Ndugu Ali Mwinchande Simba alikwishalipwa fidia ya shilingi milioni thalathini na nne, laki saba na hamsini elfu kwa vocha namba 124 ya tarehe 25 Januari, 2012 na *cheque* No. 002416 ya tarehe 1 Februari, 2012. Hivyo suala hilo limeshamalizika na ifahamike pia Kamati Teule

yenyewe imekiri kwamba tathmini ya nyumba imefanyika vizuri, lakini inashangaza kuwa ni kwa ndugu Ali Mwinchande tu ndio haki haikutendeka.

Kama ilivyokwishaelekezwa, serikali inaamini kwamba aliyekuwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano wakati huo na Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano hawakuwa na dhamira ya kulidanganya Baraza hili, bali walijibu kwa mujibu wa taarifa walizokuwa nazo wakati huo. Hata hivyo kwa kuwa wao ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ambao wanabanwa na kanuni za Baraza ni juu yao sasa kupima na kuamua watakavyoona inafaa.

Kuhusu watendaji wanaohusika na tuhuma ya kupotosha Kamati kwa kutoa taarifa zisizo za kweli, ni vyema chombo kinachohisi kimekosewa kikawasilisha suala hilo katika Taasisi husika ili ifanyiwe uchunguzi ikithibitika wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria.

Tatu, fungu la tatu uzembe wa makusudi umejitokeza katika ununuzi wa jenereta. Maelezo ya Kamati. Hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa watendaji wote waliohusika na uzembe wa ununuzi wa jenereta hilo, huku msisitizo ukiwekwa kwa Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango na Maendeleo na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Mkurugenzi na Meneja Mamlaka ya Uwanja wa Ndege ili kuondosha matatizo kama haya, Kamati inapendekeza matumizi ya fedha kama hizi yabaki katika Wizara moja tu ambayo ndio yenye mahitaji na inayojua upatikanaji wake.

Kamati inapendekeza ndani ya mwezi mmoja tu baada ya kutoa ripoti hii jenereta hilo lifanyiwe *installation* ili liweze kujulikana uzima au ubovu wake, na kama litakuwa bovu Kamati inaendelea kusisitiza kwamba hatua za kurejeshwa kwa fedha hizo ziwe dhidi ya Makatibu Wakuu wa Wizara ya Miundombiunu na Mawasiliano pamoja na Ofisi Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Maelezo ya Serikali. Serikali imejiridhisha kwamba zilikuwepo kasoro za kutofuatwa kikamilifu kwa baadhi ya hatua zilizotakiwa kuchukuliwa katika utaratibu mzima wa kununua jenereta la akiba la uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Amaan Karume kama ilivyotakiwa na sheria husika. Kasoro hizi zimetokea zaidi katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambayo ndio iliyohusika zaidi na mchakato mzima wa kupata kampuni iliyouza jenereta hilo.

Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo ilihusika kwa ku-*sign* mkataba baada ya Wizara ya Miunduombinu na Mawasiliano kukamilisha mchakato wa Zabuni na kuwasilisha ripoti yake Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Na ililazimika kufanya hivyo kwa sababu ya malipo yalitakiwa yafanywe kwa utaratibu wa kufungua LC *Letter of Credit.* Serikali inawataka watendaji wake kuwa makini zaidi, na wahusika watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma.

Kutokana na utaratibu wa matumizi ya fedha ya NBRI hakuna taasisi inayopatiwa fedha lakini hupatiwa bidhaa au huduma zinazohitajika na malipo hufanywa moja kwa moja na IMF kupitia Benki Kuu ya Tanzania. Jenereta limejaribiwa na limeonekana kuwa ni zima, hatua zinazoendelea hivi sasa ni kulifunga ili liweze kutoa huduma iliyokusudiwa kikamilifu.

Eneo la nne, mikataba takriban yote ya ukodishwaji wa uwanja wa ndege tayari imeshapitwa na wakati na kukosa sifa za msingi za kisheria. Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe Kamati Teule ilikuwa na maoni yafuatayo:

Kwa kuwa sasa Idara ya Anga ni mamlaka kamili ya Uwanja wa Ndege, Kamati inapendekeza mikataba yote iliyohusiana na ukodishwaji wa biashara mbali mbali katika eneo la uwanja wa ndege ipitiwe upya, ili iendane na mabadiliko ya biashara na msisitizo uwekwe katika gharama za kodi husika.

Kamati inapendekeza hatua za kisheria na kinidhamu zichukuliwe kwa watendaji wakuu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na mamlaka ya Uwanja wa Ndege waliohusika na upoteshaji wa Kamati kwa kutoa taarifa zisizo za kweli. Fedha na malipo yote ambayo hayajalipwa na taasisi za kampuni zilizokodishwa lazima kabla ya Mamlaka ya Uwanja wa Ndege haijaingia tena mkataba na kampuni hizo za biashara katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar.

Watendaji wa Mamlaka wa Uwanja wa Ndege wanaohusika na usimamizi wa ukodishwaji wa maeneo ya Uwanja wa Ndege msisitizo ukiwekwa kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege Captain Said Ndombugani

wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa kushindwa kuwajibika kusimamia mikataba hiyo, huku baadhi yao wakigeuka ni wafanyabiashara katika eneo la kazi, matokeo yake kupoteza mapato ya serikali.

Maamuzi ya Serikali. Pendekezo hilo la Kamati tayari limeshafanyiwa kazi, mikataba yote imeshapitiwa upya na wahusika wameshapatiwa mikataba mipya ya ukodishwaji wa maeneo hayo kwa mujibu wa kifungu 23(5) cha sheria namba 8 ya mwaka 2011.

Kama ilivyokwishaelezwa suala la kwamba watendaji waliopotosha Kamati linahitaji uthitibitisho usio shaka kama watendaji hao walikuwa na dhamira ya makusudi ya kuidanganya Kamati. Ni vyema suala hilo likafikishwa katika taasisi inayohusika ili lifanyiwe uchunguzi na ikithibitika sheria ichukue mkondo wake.

Serikali imeufanyia kazi ushauri huu na madeni mengi yamelipwa ingawa haikuwezekana kwa kampuni zote zilizokuwa na madeni kutolipa mikataba mipya kwa vile kungesababisha huduma zetu zilizokuwa zikitoka kusita na hivyo kusababisha usumbufu.
Ni kweli kwamba ulikuwepo udhaifu katika usimamizi wa mikataba ya zamani ambayo ilisainiwa kabla ya Mkurugenzi Mkuu wa sasa kuanza kazi. Hali hiyo sasa imebadilika kwani mikataba yote ilipitiwa upya kama ilivyokwishaelezwa. Hata hivyo, serikali inakubaliana na Kamati Teule kwamba, si sahihi Kampuni ya *Acro Tech* kukodishwa sehemu na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Kampuni hiyo kukodisha sehemu hiyo kwa kampuni nyengine tena kwa bei kubwa zaidi kitendo ambacho kinaikosesha mapato Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Aidha, serikali inakubaliana na Kamati Teule kwamba, si sahihi wala si kimaadili kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka kuwa mmiliki wa kampuni ambayo imeingie mkataba na mamlaka anayoiongoza ingawa *Captain* Said Iddi Ndombugani alimiliki Kampuni ya *Acro Tech* muda mrefu kabla ya kuteuliwa kwa Mkurugenzi Mkuu alipaswa kuweka bayana suala hilo na kuacha kuwa na hisa zozote katika kampuni hiyo. Serikali inamtaka Mkurugenzi Mkuu Said Iddi Ndobugani pamoja na mwanawe kujiondoa katika kampuni hiyo na wasimiliki hisa zozote katika kampuni hiyo iwapo wanataka kuendelea kuongoza mamlaka hiyo.

Kundi la Tano. Kiuhalisia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano yaani imehusika na uajiri wa wafanyakazi wake kuliko mamlaka husika. Idara ya Utumishi Serikalini kutokana na wafanyakazi hao kuajiriwa katika nafasai zilizokuwa hazijaelekezwa na mamlaka husika na hivyo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano bila ya utaratibu wowote kwa kuona wao tu inafaa wameamua kuondosha katika nafasi zilizoelekezwa na kujaza nafasi wanazotaka wao bila ya hata kuangalia sifa na uwezo wa wafanyakazi.

Maamuzi ya Kamati Teule:

Viongozi na watendaji wakuu wa wizara zote mbili Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Ofisi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora waliohusika na kadhia hii wawajibishwe kwa mujibu wa sheria. Fedha zote alizolipwa ndugu Mwanakombo Vuai Iddi katika ngazi ya utaalam ambayo hakuifikia zirejeshwe serikalini kwa utaratibu wa kukatwa mshahara wake na hatua hizi zitumike kwa wafanyakazi wote walioajiriwa mara mbili, ingawaje kwa wafanyakazi hawa fedha hizo zirudishwe kupitia mishahara ya watendaji wakuu wa wizara hizi mbili zinazohusika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Ofisi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Uajiri wa Wafanyakazi wote ambao kamati imegundua kwamba hawana sifa za kuajiriwa kufanyike upya kwa kufuata muongozo wa sheria zilizopo sasa.

Maamuzi ya Serikali:

Serikali inakubaliana na Kamati Teule kwamba zilikuwepo kasoro za kiutendaji kwa taasisi zote mbili zilizohusika na suala zima la uajiri uliofanyika katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Ofisi ya Utawala wa Umma na Utawala Bora, na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kasoro hizo zilichangiwa sana na kutokuwepo kwa sheria rasmi iliyoongoza masuala ya utumishi. Kasoro hizo hazitarajiwi kutokea tena baada ya Sheria ya Utumishi wa Umma kuanza kazi rasmi Julai, 2011 kwa kuwa suala hili la kiutendaji zaidi ni watendaji ndio waliohusika na si viongozi Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hizo. Serikali itakuwa makini zaidi na kuhakikisha kuwa sheria ya Utumishi wa Umma inafuatwa kikamilifu na makosa kama hayo hayatatokea tena.

Kuhusu mfanyakazi aliyetuhumiwa kuajiriwa katika taasisi mbili za wizara moja imebainika kuwa ajira aliyokuwanayo katika Shirika la Bandari haikuwa ya kudumu ilikuwa ni *temporary*. Kwa hivyo, hakuwa na kosa kwake kuomba ajira ya kudumu, *permanent employment*. Hata hivyo, imebainika kwamba mhusika hakuwahi kuchukua mshahara tangu alipoajiriwa kwa utaratibu wa kudumu.

Pamoja na kasoro zilizojitokeza katika suala zima la ajira itakuwa ni kinyume na sheria kuwaachisha kazi vijana waliohusika kwa vile wao hawakuwa na makosa yoyote. Serikali itawapangia majukumu kulingana na sifa zao isipokuwa waliogundulika kughushi vyeti ambao hatua za kisheria zitachukuliwa zidi yao.

Kuhusu kusumbuliwa kwa wafanyakazi kwa madai kwamba walitoa mashirikiano kwa Kamati, serikali haiwezi kulitolea maelezo suala hili kwa sababu wahusika hawakuainishwa katika ripoti ya kamati.

Kundi la Sita. Mamlaka ya Uwanja wa Ndege wakati huo ilikuwa Idara ya Anga kwa kiasi kikubwa imehusika katika mgogoro ambao wao wenyewe wameshindwa kuutatua.

Mapendekezo ya Kamati. Pamoja na Viongozi waandamizi wa Ushirika wa *ZAP* na Ndugu Khamis Mussa Juma kushinda kununua hisa katika kampuni hiyo kutokana na umasikini wao, ingawaje ndugu Khamis amenunua asilimia 5, serikali kupitia mamlaka zinazohusika ziwasaidie kununua *share* hizo kwa asilimia 50. Mamlaka ya Uwanja wa Ndege isijiingize katika mgogoro huu na badala yake iwe muangalizi au msimamizi wa majukumu ya kampuni hii.

Majibu ya Serikali. Suala hili mgogoro binafsi hivyo si vyema serikali kujiingiza katika mgogoro huo bali ziachiwe taasisi binafsi zenyewe zilizo katika mgogoro huo kutafuta suluhu ya jambo hilo.

Kundi la Saba. Kuna uvamizi mkubwa wa maeneo ya fukwe na uharibifu wa mazingira na kamati imejiridhisha kwamba ujenzi wa miradi ya mahoteli Zanzibar hauzingatii matakwa ya sheria zinazoelekeza juu ya masuala ya ardhi na mazingira.

Maamuzi ya Kamati. Serikali ndani ya miezi mitatu kuanzia tarehe ya kuwasilishwa ripoti hii iunde kamati itakayofuatilia suala la uvamizi na uharibifu wa mazingira katika miradi yote ya mahoteli Zanzibar na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaobainika kukiuka na kadhia hiyo huku pia ikizichukulia hatua za kisheria hoteli zote zitakazobainika kukiuka taratibu za uwekezaji. Iwapo baada ya kumalizika muda huu wa miezi mitatu, serikali imeshindwa kufanya hivyo kuunda kamati hiyo ya Baraza la Wawakilishi itekeleze jukumu hilo na kuunda kamati maalum ya muda ya kufuatilia suala hili na ripoti yake iwasilishwe katika Baraza la Wawakilishi.

Aliyekuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Mhe. Machano Othman Said awajibishwe na kushiriki kwake kwa kiasi kikubwa katika uharibifu uliofanywa na ujenzi wa Mradi wa Pemba Misali *Sun Set Beach Hotel* wakati yeye ni kiongozi wa serikali. Kwa kuwa sheria Nam. 2 ya mwaka 1996 imewapa mamlaka inayofaa Idara ya Mazingira kumchukualia mtu yoyote atakaekiuka sheria hiyo hatua za kisheria jambo ambalo halikufanyika. Kamati inapendekeza watendaji Wakuu wa Idara ya Mazingira wanaohusika na kusimamia mazingira wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa kushindwa kwao kusimamia sheria. Watendaji Wakuu wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara walioshiriki katika ufukiaji wa ardhi, katika Hoteli ya *Maruhubi Beach Villa* wachukuliwe hatua za kinidhamu ili iwe ni funzo kwa watendaji wengine.

Maagizo ya Idara ya Mazingira iliyoyatoa kwa wawekezaji hao kuhusiana na uvamizi wa fukwe na uharibifu wa mazingira waliofanya kufuatia ujenzi wa miradi yao ikiwa pamoja na kuvunja majengo ya mikahawa iliyojengwa ndani ya fukwe katika hoteli ya *Zanzibar Ocean View* yasimamiwe na Serikali Kuu huku ikihakikisha inatekelezwa ndani ya miezi miwili tokea tarehe ya kuwasilishwa kwa ripoti hii na taarifa za utekelezaji wake ziwasilishwe katika Baraza la Wawakilishi.

Serikali isimamie ndani ya mwezi mmoja ihakikishe kwamba malipo yote ya leseni za biashara ya utalii ambazo hazikukatwa na wawekezaji hao tokea kuanza kwa miradi yao zilipwe mara moja kama sheria inavyoelekeza huku ikihakikisha kwamba wawekezaji hawa wanafuata ipasavyo mikataba ya sheria zinazohusika na uwekezaji kabla ya kupewa leseni na vibali vyengine vyovyote vinavyohusika na miradi yao.

Hatua za kisheria zinazohusiana na mazingira na uwekezaji wa miradi ya utalii kwa ujumla zichukuliwe mara moja zidi ya wawekezaji hawa na taarifa za hatua hizo ziwasilishwe katika Baraza la Wawakilishi katika mkutano wa Nane wa Baraza unaotarajiwa kuanza mwezi wa Septemba – Oktoba 2012.

Maamuzi ya Serikali. Serikali kimsingi inakubaliana na Kamati Teule kuhusu hoja ya kulifanyia kazi suala zima la uvamizi na uharibifu wa mazingira katika hoteli mbali mbali. Hata hivyo, utaratibu unaopendekezwa na Kamati Teule ni vigumu kuutekeleza kwa vile utakuwa ni wa gharama kubwa kwani wajumbe watakaoteuliwa katika kamati hiyo au kamati iliyoteuliwa na Baraza la Wawakilishi itabidi walipwe posho na ikitiliwa maanani idadi kubwa ya hoteli zilizopo na wingio wa Wajumbe na siku zinazohitajika kukamilisha kazi hiyo. Gharama kwa kazi hiyo itakuwa kubwa sana kwa mfano,

Iwapo kamati itakuwa na watu wasiozidi saba na posho lapo wataliwap ni wastani wa shilingi laki moja kwa siku utahitaji shilingi laki saba kwa siku. Kuna zaidi ya mahoteli ya 200 na iwapo kila hoteli itakaguliwa siku moja tu kutahitajika si chini ya shilingi 140 milioni kwa ajili ya posho, bado kuna gharama nyenginezo nyingi kama vile usafiri, vifaa vya kuandikia, sekereteriet na kadhalika. Kwa hivyo, serikali imeona ni vyema kazi hiyo ikafanywa na taasisi za serikali zinazohusika zikiwemo Idara ya Ardhi, Idara ya Mazingira, *ZIPA* na Kamisheni ya Utalii na wamiliki wa mahoteli zitakazobainika kuwa na makosa watakaotakiwa kurekebisha makosa yaliyobainika na wasipotekeleza watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Kazi hiyo itakuwa endelevu na serikali itahakikisha kwamba taasisi hizo zinasimamia ipasavyo zitekeleze wajibu wake kwa mujibu wa sheria.

Kuhusu ushauri wa Kamati Teule wa kuwaajibisha Mhe. Machano Othman Said, Kamati Teule imeshindwa kutoa ushahidi usioshaka kwa jinsi Mhe. Machano alivyoshiriki katika vitendo vya uharibifu wa mazingira katika hoteli iliyotajwa. Aidha, jukumu zima la kusimamia masuala ya mazingira lipo kwa taasizi zinazohusika na kwa hivyo serikali imeshindwa kufahamu vipi Mhe. Machano anahusishwa na uharibifu wa mazingira katika hoteli hiyo.

Suala la yeye kuwa ana hisa katika mradi huu si hoja inayotosheleza kwani hakuna sheria inayokataza mtu kuwa na hisa katika kampuni mradi tu hakuna mgongano wa kimaslahi. Kwa suala hili Mhe. Machano hakuwa msimamizi wa taasisi ambazo zinahusika na masuala ya mazingira na kwa hivyo hoja ya kumuajibisha haina msingi. Ni dhahiri kwamba Idara ya Mazingira imetafsiri vibaya sheria ya mazingira kuhusiana na uwezo wake wa kuwachukulia hatua wahusika na hata katika kutoa amri za kusitisha *stop orders,* katika kutoa *stop orders* Idara ya Mazingira mbali ya kutoa amri ya kusitisha inatakiwa iweke alama katika sehemu iliyotolewa *stop order* kuonesha kuwa sehemu hiyo husika imetolewa amri ya kuzuia. Hivyo imeelekezwa itumie kikamilifu sheria Nam. 2 ya mwaka 1996 ili kuhakikisha kuwa uharibifu wa mazingira unazuiliwa kifungu Nam. 23 na 100 vya sheria hiyo vinaipa mamlaka Idara ya Mazingira kuchukua hatua za kisheria endapo kutakuwa na uharibifu wa mazingira. Serikali itasimamia taasisi zinazohusika zinatimiza wajibu wake na kuzitumia sheria zilizopo kikamilifu.

Watendaji wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara hawakuwa na dhamira ya kupeleka kifusi kwa Ndugu Halifa kwa nia ya kumfaidisha bali ilifanya hivyo kwa utaratibu wake wa kawaida wakati wa ujenzi wa barabara wa kuondoa udongo usiofaa kutoka katika eneo la ujenzi na kutupwa sehemu nyengine. Hivyo watendaji hao wanaopata eneo la karibu la kutupwa udongo lisilohitajika huwa ni faida kwao katika usafirishaji wa eneo lao. Kwa mnasaba wa eneo la ndugu Halifa la Maruhubi lilitupwa dongo hilo kwa kurahisishia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kazi ya utupaji udongo usiohitajika ambao kinyume chake udongo huo ungelibidi utoke Mtoni na kupelekwa Shakani ama Kibele sehemu ambazo ni mbali ukilinganisha na Maruhubi, wakati huo watendani hao walikwenda kutupa dongo hilo huku wakiwa hawana taarifa kwamba mwekezaji huyo kazuiliwa kufukia eneo hilo. Hivyo basi, hakuna sababu yoyote ya msingi kwa watendaji wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara kuchukuliwa hatua kutokana na kadhia hii.

Hatua zinachukuliwa kwa kuvunja mkahawa uliokuwa ndani ya fukwe katika Hoteli ya *Zanzibar Ocean View* na makuti yaliyokuwepo katika jeti ya Pemba *Misali Sun Set Beach* yameezuliwa na kuezekwa bati. Aidha, Idara ya Mazingira inasubiri ripoti ya tathmini ya ukaguzi wa kimazingira unaoendelea kufanya katika hoteli ya *Maruhubi Beach Villa* na *Misali Sun Set Beach* hatua za kufaa zitachukuliwa kufuatia matokeo ya ripoti hizo. Baada ya kufuatilia suala hili, imebainika kuwa miradi iliyo chini ya Kamisheni ya Utalii ni kama ifuatavyo:

Hoteli na nyumba za kulaza wageni 224, Kampuni za kutembeza wageni 144, Taasisi za wazamiaji 30, Mikahawa 36. Hiyo ndio miradi yote inayofanya kazi chini ya Kamisheni ya Utalii na hakuna mradi ambao haujasajiliwa. Hata hivyo, imejitokeza tabia ya baadhi ya wananchi kulaza wageni katika nyumba za makaazi kinyume na utaratibu. Pia

zipo nyumba za makaazi ambazo zinamilikiwa na wageni ambazo pia zinakiuka taratibu kwa kulaza wageni kinyume na utaratibu. Tabia hii imejitokeza zaidi katika Mkoa wa Kusini Unguja, Kamisheni ya Utalii inaendelea kuzifuatilia nyumba hizo na kuchukua hatua za kumaliza tatizo hilo.

Serikali imepokea ushauri huo na kuufanyia kazi kama ilivyopendekezwa na kamati teule. Hata hivyo, ni vyema Idara ya Mazingira yenyewe ichukue hatua kwanza kama sheria nambari 2 ya mwaka 1996 inavyoelekeza katika kifungu 23 na 100 ya sheria hiyo. Taasisi za serikali zinazohusika zitalifanyia kazi suala hili na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria.

Kudi nambari Nane. Kamati imebaini kwamba kuhaulishwa kwa ardhi hii kumezingatiwa kibiashara zaidi na sio kwa haja halisi ya matumizi ya ardhi husika.

Mapendekezo ya kamati teule: Uhaulishaji wa kiwanja hicho haukuzingatia masharti ya utolewaji wake kama ilivyokusudiwa na sheria, hivyo kamati inapendekeza kiwanja hicho kirudi serikalini mara moja. Kuna haja ya kuifanyia marekebisho sheria ya umiliki wa ardhi Nam. 12 ya mwaka 1992 ili sitoe mamlaka yasio na mipaka ya Mhe. Waziri kuhaulisha ardhi ya serikali. Kuna haja ya kufanya marekebisho ya kanuni zinazohusiana na masuala ya ardhi ili zitoe utaratibu wa maombi ya matumizi ya ardhi kwa mtu yoyote anayehitaji na yawe kwa kupitia Katibu Mkuu Wizara inayohusika na masuala ya ardhi.

Maamuzi ya Serikali. Sheria ya ardhi iko wazi kwamba Mhe. Waziri anayehusika na ardhi anaweza kumpa mwananchi ardhi kwa utaratibu wa kutoa haki ya matumizi ya ardhi au kwa kukodisha. Hata hivyo, ardhi iliyokwishakutolewa kwa mtu mmoja haiwezi tena kutolewa kwa mtu mwengine kwa utaratibu huo wa *grant*, ikiwa ardhi hiyo haikurudishwa serikalini, au kufutwa. Kwa hivyo, mtu anayepewa anaweza kuitoa ardhi hiyo kwa mtu mwengine kwa utaratibu wa uhaulishaji kwa mujibu wa sheria ya uhaulishaji wa ardhi ya *Land Transfer Act* ya mwaka 1994. Bila shaka utaratibu ulikosewa kisheria kwa mama Fatma Karume alikwishapewa kiwanja hicho kwa njia ya grant na kama alitaka kumpa mtu mwengine alipaswa kukitoa kwa utaratibu wa sheria ya uhaulishaji *(Land Transfer Act)* na sio *grant* tena kama ulivyofanywa na wizara husika.

Hivyo kwa kuwa Mama Fatma Karume alipewa kiwanja hicho kihalali hana haki ya kukihaulisha kwa mtu mwengine kama utaratibu unavyoelekeza, ingawa kisheria kiwanja hicho bado ni cha Mama Fatma kwa kuwa hakuna hatua iliyochukuliwa na taasisi husika kufuta hati hiyo. Lakini kwa vile yeye mwenyewe alishakiuza kwa mtu wa tatu kwa kiasi cha fedha kinachooneshwa kwa mtu huyu wa tatu alikinunua kihalali. Serikali haiwezi kumnyang'anya mtu huyo aliyekinunua mpaka ithibitishe kuwa naye alihusika na udanganyuifu kama upo. Endapo serikali itachukua hatua hizo ni wazi kuwa inaweza kushtakiwa na kupata gharama kubwa zaidi, ni wajibu wa aliyekinunua kuhakikisha kuwa taratibu zote za uhaulishaji zinafuatwa kwani dhahiri kuwa hati aliyopewa ina utata wa kisheria kwa vile haijafutwa ile ya mwanzo, hivyo inaweza kuleta mzozo wa kisheria hapo baadae.

Serikali inaendelea na hatua ya kuifanyia marekebisho sheria ya ardhi na itazingatia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati Teule. Serikali itazingatia mapendekezo ya Kamati Teule na kumhusisha Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na ardhi katika mchakato mzima wa kushughulikia maombi ya hati.

Fungu la Tisa: Mikataba yote ya umiliki wa nyumba hiyo ni batili na haina nguvu za kisehria.

Mapendekezo ya Kamati Teule. Nyumba hiyo ambayo sasa imeshajengwa hoteli ya ndugu Amina Amani Karume kamati inapendekeza hati zote za umiliki wake zifutwe na apatiwe tena hati za umiliki wa ardhi husika na baadae atakiwe amsaidie Ndugu Juma Ali Kidawa kiwango cha fedha kisichopungua shilingi 20 milioni ili kumsaidia kujinasua na maisha kwa sababu kwa mujibu wa ushahidi wa kimazingira inaonesha wazi kwamba mwananchi huyo alikusudiwa kumiliki nyumba hiyo kutokana na uhusiano wake na mmiliki wa nyumba hiyo kabla ya kutaifishwa na serikali. Hatua za kisheria zichukuliwe zidi ya wananchi wote waliohusika katika udanganyifu uliojitokeza katika upatikanaji wa mikataba ya mauziano kutoka Mamlaka ya Serikali na kumuuzia Ndugu Juma Ali Kidawa na mauziano baina ya Ndugu Juma Ali Kidawa na Ndugu Amina Amani Karume.

Hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa watendaji wakuu wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati waliohusika na upatikanaji wa Mkataba wa mauziano ya nyumba nambari 755/56 kwa thamani ya shilingi milioni tano baina ya wizara hii na Ndugu Juma Ali Kidawa. Hatua za kinidhamu hizi zichukuliwe dhidi ya watendaji wa Ofisi ya Mrajis

Mkuu wa Serikali walioshiriki katika upatikanaji wa mkataba wa mauziano baina ya ndugu Juma Ali Kidawa na Ndugu Amina Amani Karume.

Maamuzi ya Serikali. Kamati Teule haikuweza kubaini kama viwanja hivyo vilikuwa viwili tofauti, yaani kiwanja nambari moja na nambari mbili chenye ukubwa wa mita za mraba 212.94 na cha pili ni kile chenye gofu la nyumba Nam. 755/56. Kwa hivyo, kiwanga nambari moja na mbili hakina matatizo kwa vile kimetolewa kihalali kwa hati ya matumizi ya ardhi ya tarehe 17/04/2007.

Kwa upande wa Gofu lenye namba 755/56 endapo ndugu Kidawa anadai kwamba saini zilizomo kwenye hati ya kupewa na serikali na hati ya kumuuzia Ndugu Amina A.A. Karume si zake kiutaratibu ana haki ya kwenda Mahkamani kupinga kutumika kwa jina lake katika hati hizo. Wakati huo huo jambo la kushangaza ni kuwa, Kamati Teule imejiridhisha kuwa saini zilizokuwemo katika nyaraka hizo sio za Juma Ali Kidawa lakini huku inaelekeza apewe shilingi 20 milioni. Sasa je, apewe za nini wakati mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 13/05.2008 na sheria hiyo imepitishwa na Baraza la Wawakilishi nakuanza kutumika tarehe 03/11/2008. Kwa taratibu zilizokuwa zikitumika wakati huo hakuna taratibu zilizovunjwa na kwa hivyo hakuna haja ya kuchukua hatua za kinidhamu kwa mtu yeyote.

Hivi sasa ujenzi wa jengo hilo tayari umeshasimamishwa. Hata hivyo, serikali haiwezi kuchukua hatua nyegine zaidi kwa sasa kwani mkataba umeelekeza kutafutwa sulhu kwanza, pale itakapotokea pande mbili zimekosana katika kutekeleza mkataba huu kwa vyovyote ni lazima serikali iheshimu mkataba na ichukue hatua kwa mujibu wa sheria ya mkataba. Hatua zinazochukuliwa na serikali kwa hivi sasa ni kama ifuatavyo:

Imesimamia kupatikana kwa msuluhishi wa mgogoro ambaye amekubaliwa kwa pande zote, hii inahusu ile nyumba ya ujenzi wa Pemba ya Wizara ya Fedha, imeshalipa shilingi milioni tano zikiwa ni gharama za usuluhisho kwa mgogo wa msuluhishi. Tumeshatengeneza mpango kazi kwa kushirikiana na pande nyengine za mgogoro ambaye ni mjenzi na mshauri mwekezi. Nimeshaandaa hoja ya serikali ya kuziwasilisha kunakohusika, hivyo kinachosubiriwa sasa ni msuluhishi kuanza kazi zake.

Fungu 11. Ukodishwaji wa majengo ya Mambo Msiige na *Starehe Club* haukufuata taratibu za uwekezaji zinazoelekezwa na sheria zinazohusiana na uwekezaji Zanzibar.

Maamuzi ya Kamati Teule. Mkataba wa kodi kwa mwekezaji huyu *ASB holdings limited* aliyekodishwa majengo hayo usitishwe mara moja, kwa serikali kurejesha fedha za kodi iliyokwishazipokea na majengo hayo yarudi serikalini, huku serikali ikiona ipo haja ya kukodisha, basi ni lazima majengo hayo yakodishwe kwa kufuata taratibu za kisheria kwa maslahi ya taifa.
Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali, itafutiwe eneo jengine kwa matumizi ya ofisi itakayokidhi haja na hifadhi bora za kumbukumbu za taifa, huku jengo hilo la *PBZ* la zamani, lifanyiwe ukarabati liwe halivuji na kuwepo mahitaji yote muhimu ya ofisi, ikiwa ni pamoja na matumizi ya maji salama na ya uhakika na zimebaki taasisi zilizomo baada ya kuondoka Ofisi ya Mrajis.

Mamlaka ya Mji Mkongwe na Idara ya Nyaraka na kumbukumbu za taifa zishirikishwe ipasavyo katika hatua zote za ushauri na maelekezo juu ya uhifadhi wa majengo hayo ili yasipoteze haiba na historia yake.

Maamuzi ya Serikali. Mkataba wa mwekezaji *ASB Holdings Limited* aliyekodishwa majengo ya Mambo Msiige na *Starehe Club*, imefuata utaratibu wa kisheria. Tofauti iliopo ni kwamba kamati teule waliingilia suala hili kwa kufuata sheria ya vitega uchumi, *Investment Act*, wakati ukodishwaji huo umefanywa kwa kufuata sheria ya ardhi nambari 2 ya mwaka 1992 (*Land Tenure Act).*

Pia sheria ya uwekezaji hailazimishi mwekezaji lazima aanze kupitia mamlaka ya vitega uchumi anapotaka kuekeza, isipokuwa kama atataka kufaidika na fursa zinazotolewa na *ZIPA*. Kwa vile mkataba wa kuuza majengo hayo na kukodisha ardhi ya sehemu hiyo ni halali kisheria, kurejesha majengo hayo serikalini kutaipelekea serikali kuvunja mkataba na hivyo uwezekano wa kupata hasara kubwa. Utaratibu uliotumika upo kisheria, utaratibu kama huo ndio pia uliotumika kwa miradi mingine iliyo ndani ya Mji Mkongwe. Kama vile *Serena Inn, Tembo Hotel, Old Dispensary* na mengine.

Serikali ililifanyia matengenezo jengo la *PBZ* kabla ya taasisi zinazohusika kuhamia huko. Aidha, serikali inaendelea na u jenzi wa jengo jipya la Wizara ya Katiba na Sheria, ambapo Idara ya Mrajis itapatiwa ofisi katika jengo hilo jipya baada ya kukamilika. Pia ni vyema kujua kwamba nyaraka hizo muhimu hivi sasa ziko pahala pazuri zaidi kuliko zilipokuwa na zitahamishiwa katika jengo jipya mara tu litakapomalizika, ambapo ujenzi wake unatarajiwa kukamilika Novemba 2013.

Ni utaratibu wa kawaida wa serikali kuzishirikisha taasisi zake kila inapohisi kuna ulazima kufanya hivyo. Mamlaka ya Mji Mkongwe na idara ya nyaraka zinashirikishwa na zitaendelea kushirikishwa kuhusu masuala yanayohusu taasisi hizo kwani ni sehemu ya majukumu yao.

Madai ya kwamba serikali ilitumia nguvu katika kuzihamisha taasisi zake, hayana msingi wowote kwani hayayumkiniki kuwa serikali itumie nguvu kwa taasisi zake wenyewe. Ukweli ni kwamba utaratibu wa kuhama uliandaliwa na kamati maalum, iliundwa kwa kusimamia zoezi hilo na ilihusisha watendaji wa taasisi zinazohusika.

Fungu 12 serikali kupitia mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar na vyombo vyengine vinavyohusika haina takwimu yoyote inayoonesha idadi ya wageni wanaoingia kwenye kisiwa cha Changuu si kwa siku, kwa mwezi na wala kwa mwaka.

Pia haieleweki ni kiasi cha mapato ambacho mwekezaji anaingiza kutokana na biashara anazofanya kwenye kisiwa hiki, lakini kibaya zaidi hakuna hatua zinazochukuliwa wala taarifa yoyote inayopatikana kiulinzi na usalama kwenye kisiwa cha Changuu.

Mapendekezo ya kamati:

Serikali kupitia ZRB ifanye ukaguzi maalum wa kupata taarifa sahihi za wageni wanaoingia kwenye kisiwa hicho na kiasi gani cha mapato huwa kinakusanywa kutokana na biashara yoyote inayofanyika bila ya kusahau mapato yanayotokana na makobe na ripoti za taarifa hizi ziwasilishwe katika Baraza la Wawakilishi si zaidi ya mwezi mitatu kuanzia tarehe ya kuwasilishwa kwa ripoti hii.

Serikali ihakikishe kuwa inafanya tathmini ya ardhi inayotaka kukodishwa kabla haijakodishwa ili iweze kupatikana tathmini halisi ya kodi inayostahiki kulipwa kwa thamani ya ardhi hiyo. Kuna haja ya kufanya marekebisho ya ongezeko la kodi kwamba lisiishie asilimie 10 ya kodi ya awali kama ilivyo kwenye mikataba yote ya ukodishwaji wa ardhi wa hivi sasa. Kwa hivyo basi kifungu 46 cha sheria ya ardhi na Nam. 12 inafaa kiangaliwe upya utoe nafasi ya ongezeko la kodi ya zaidi ya asilimia 10 ya kodi ya awali endapo kutakuwa kuna ongezeko la kufanya hivyo.

Maelezo ya Serikali:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kupitia Bodi ya Mapato ya Zanzibar imefanya ukaguzi wa miradi iliopo katika Kisiwa cha Changuu na kutoa ripoti yake juu ilianzia Januari, 2004 hadi 2012.

Ukaguzi huo umehusisha Kampuni ya Leisure Hotel, Bawe Island Zanzibar limited ambayo inamiliki hoteli mbili katika kisiwa cha Bawe na Changuu. Hoteli hizo ni Leisure Hotel na Bawe Island Zanzibar limited na Leisure Hotel Changuu Island Zanzibar Limited.

Katika ukaguzi huo mambo yafuatayo yamejitokeza.

Leisure Hoteli Bawe Island ni hoteli ya kitalii yenye jumla ya vyumba 15 na uwezo wa kubeba wageni 30 kwa mwezi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi imekodisha ardhi kwa kampuni hiyo kwa muda wa miaka 33 kwa malipo ya kodi ya Dola elfu thalathini na tano kwa mwaka kuanzia 2000. Kutoka mwaka 2000 hakuna shughuli yoyote ya kibiashara iliyofanywa katika eneo hilo.

Leisure Hoteli Changuu Island ni hoteli ya kitalii yenye nyumba 27 na uwezo wa kulaza wageni 52 kwa pamoja kama ilivyo kwa Bawe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi imekodisha eneo hilo kwa muda miaka 33 kwa malipo ya Dola elfu kumi na moja mia mbili na sabini kuanzia mwaka 2002.

Kuanzia mwaka 2006 mpaka 2009 hoteli ilikuwa ikifanya biashara ya kulaza wageni pamoja na kutoa huduma nyengine mbali mbali. Na kuanzia 2009 mpaka 2012 shughuli za kulaza wageni zilisitishwa ila kuna wageni wanaokwenda kwa matembezi ya kutwa, wageni hao hulipa Dola nne kwa asiyekuwa raia na kwa raia wa Tanzania hulipa shilingi elfu moja.

Hoteli imeajiri wafanyakazi 24. Katika mwaka 2004-2012 hoteli imefanya mauzo ya Tanzania Shilingi bilioni moja nukta tatu, tisa ziro ambapo ililipa kodi ya Tanzania Shilingi ya milioni mia mbili ishirini na tatu, laki tano ishirini mia mbili hamsini na nane na senti sitini na tisa ambazo zimewasilishwa Bodi ya Mapato.

Pia katika kipindi hicho hoteli ilipokea wageni laki mbili sitini na sita elfu, mia mbili na sitini na tano, kati ya hao mia mbili na sitini na nne mia mbili na sitini ni wageni waliokwenda na kurudi na wageni laki moja ndio waliolala.

Kumbukumbu zinaonesha kwamba fedha zilizokusanywa kutokana na ada waliyolipwa wageni hao hotelini hazikulipiwa kodi. Hii ni kusema kwamba hoteli haikuwa ikitoa taarifa za wageni inayowapokea. Hivyo Bodi ya Mapato Zanzibar haikukusanya kodi yoyote iliyotokana na ada walizolipa wageni katika hoteli hiyo kwa kipindi hicho hicho cha ukaguzi.

Jumla ya mauzo yenye thamani ya Dola laki mbili sitini na nane elfu, mia tatu sabini na tano na yenye kodi ya VAT arobaini na tisa mia saba ishirini na tisa senti moja saba hayakuripotiwa na mlipa kodi. Hivyo kutokana na kifungu cha 31 cha sheria ya usimamizi wa kodi Tax Administration and Procedure Act Nam. 7 ya 2009, hoteli hii inapasa kulipa kodi hiyo na kutozwa adhabu ya asilimia ishirini ya kodi iliyokwepa ya jumla Dola elfu tisa mia tisa na arobaini na tano na senti thamanini na tatu.

Pia atapaswa kulipa riba iliyotokana na kodi hiyo, hivyo mlipa mkodi anatakiwa kulipa Dola laki moja elfu tano na hamsini na senti thamanini na nane ikiwa ni kodi aliyokwepa na adhabu pamoja na riba. Serikali kupitia taasisi inayohusika itahakikisha inasimamia mlipa kodi huyo ili aweze kutekeleza wajibu wake.

Suala la kufanya tathmini ya ardhi iliyokodishwa na kufanya mapitio ya kodi ya ardhi iliyokodishwa ni ya msingi, hivyo serikali inakubaliana na pendekezo hilo la Kamati Teule.

Serikali imelipokea na kulifanyia kazi suala hili, hata hivyo kinachoonekana kwamba suala hili linahitaji umakini mkubwa katika kulifanyia kazi, kwani ardhi iliyokodishwa awali thamani huongezeka mara baada ya kufanya uwekezaji bila ya shaka yoyote. Mwekezaji ndiye atakayekuwa amechangia kuipandisha thamani ardhi hiyo, hivyo kumuongezea kodi kutokana na uwekezaji wake inaweza ikavunja moyo wawekezaji. Kwa msingi huo ni vyema taasisi zinazohusika na ardhi na ukodishwaji wa ardhi walifanyie kazi suala hili na waishauri serikali ipasavyo.

Suala la kuimarisha ulinzi katika maeneo yote wanayotembelea wageni ni la msingi. Hivyo Serikali itachukua hatua za makusudi kuimarisha usalama kwenye maeneo ya visiwa vya Changuu na mengineyo.

Suala la kumsimamia mwekezaji ipasavyo ili aweze kufuata sheria na taratibu zilizopangwa ni la msingi. Serikali itazihimiza taasisi zinazohusika zitekeleze wajibu wake ipasavyo ili kuona mwekezaji anatii sheria.

Serikali inakubaliana na ushauri wa kamati na itazitaka Idara za Mazingira na taasisi nyengine zinazohusika zifanye utafiti wa tathmini na uharibifu wa mazingira katika visiwa cha Changuu na maeneo mengine itakapobainika kuwa kuna ukiukwaji wa sheria hatua zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria.

Fungu la 13 na la mwisho.

Mamlaka ya Maji (ZAWA) imeshindwa kuzitambua mali zake, majenereta 12 hali inayoonesha tokea mwanzo kwamba hawakuwa na uchungu na kuharibika kwake.

Mapendekezo ya Kamati:

Mamlaka ya Maji (ZAWA) ilitafute jenereta ambalo kamati imeshindwa kulitambua ndani ya miezi mitatu tokea tarehe ya kuwasilishwa ripoti hii na ikishindwa Mkurugenzi Mkuu wa ZAWA awajibike kulilipa kupitia mshahara wake.

Majenereta yote 11 yaliyotambuliwa na kamati yafanyiwe matengenezo ya haraka ndani ya mwezi na yapatiwe mafuta ili yaweze kutumika kama ilivyokusudiwa. Watu wanaotoa huduma vituoni watafutiwe utaratibu wa kuwajibiwa na katika kipindi chote hiki cha kusubiri ajira zao, ZAWA iliwalipe posho za kufanya kazi hiyo na suala hili litekelezwe mara moja.

Maamuzi ya Serikali:

Jenereta linalodaiwa kuwa halikuonekana na Kamati Teule ni jenereta Nambari 117003837 ambalo lipo Mombasa kwa Mchina. Tatizo lililojitokeza hapa ni kwamba wakati wa kupokea majenereta hayo, hati ya kupokea develivery note iliorodhesha majenereta mawili kwa namba moja ambapo jenereta namba 7 na namba 11 yote yalisajiliwa kwa namba 11603576.

Usahihi ni kuwa ilipaswa moja kati ya jenereta hilo lisajiliwe kwa namba 117003837. Kwa ufafanuzi huu inadhiri kuwa hakuna jenereta lililopotea.

Mamlaka ya Maji imelifanyia kazi suala hili na majenereta yamefanyiwa service na yanajaribiwa kila baada ya muda, kwa ufafanuzi zaidi majenereta yote ni 12.

Suala la ulinzi wa vituo vya visima vya maji ni muhimu kiusalama na kiafya. Utaratibu unaotumika sasa ni ulinzi shirikishi na ni vizuri uendelee. Ni vizuri kwa uongozi wa ngazi zote kushiriki katika kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kulinda vianzio vya maji, kwani itakuwa ni mzigo mkubwa kwa ZAWA kuwaajiri wafanyakazi kila penye kianzio cha maji.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa kwa ruhusa yako niwasilishe rasmi taarifa hiyo katika Baraza lako tukufu na hapa ndio mwisho wa mapendekezo na maamuzi ya serikali.

Nakushukuru sana kwa kunisikiliza.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri, sasa tunamkaribisha Mhe. Mwenyekiti wa kamati inayohusika.

Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati Teule): Kamati ipi, eeh! mbona mimi sijaarifiwa chochote.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba nimekuwa *surprise* kwa sababu sikujiandaa na hili, sikupewa taarifa kabla lakini hata hivyo ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii, na nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati Teule.

Mhe. Mwenyekiti, nitaanza kwa kunukuu Katiba ya Zanzibar kifungu cha 5 (a). Kifungu cha kwanza kinasema kwamba Zanzibar itafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka ya utendaji, mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma na mamlaka ya utekelezaji utoaji wa haki.

Kifungu hicho hicho cha 5 (a) kwenye kifungu cha pili kimesema kwamba mamlaka ya utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mamlaka ya kutunga sheria ni na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma ni Baraza la Wawakilishi na mamlaka ya kutekeleza utoaji wa haki ni Mahakama.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza mamlaka yake kikatiba ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma Baraza limeunda linatakiwa liunde kamati mbali mbali za kudumu pamoja na Kamati Teule pale haja inapotokezea kufanya hivyo. Hiyo ni kwa mujibu wa kifungu cha 120 cha Kanuni yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza kupitia Mhe. Spika aliunda Kamati Teule ambayo ilipewa majukumu ya kuchunguza mambo kadhaa kama yalivyoainishwa katika ripoti ile. Kamati yetu ile ambayo mimi niliiongoza ilifanya kazi kwa umakini mkubwa sana na hatimaye kamati iliwasilisha ripoti yake katika Baraza hili na ripoti ile ilikuwa na mapendekezo.

Mhe. Mwenyekiti, ninakumbuka kwamba Baraza lilijadili ripoti na mapendekezo yake na hatimaye Baraza liliipokea ripoti pamoja na mapendekezo yake yote na kuikabidhi serikali kwa ajili ya serikali kwenda kuyatekeleza mapendekezo yaliomo kwenye ripoti ya Kamati Teule kama yalivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kilichotokea inaonekana serikali badala ya kwenda kuyatekeleza maamuzi ya Baraza, serikali ilikwenda kuyaundia tena kamati mapendekezo yale ili kwa ajili ya kuyachunguza. Kitu ambacho serikali haikupaswa kwenda kuyachunguza mapendekezo yale bali kuyatekeleza kama yalivyokubaliwa na Baraza la Wawakilishi ambapo serikali ilikuwa ni sehemu ya maamuzi yale.

Mhe. Mwenyekiti, katika ulimwengu huu wa utekelezaji wa dhana wa utawala bora na kufuata misingi ya mgawanyo wa madaraka. Kitendo hiki kilichofanywa na serikali kwa sababu hata Mhe. Waziri alipokuja hapa alisema maamuzi ya serikali. Yale maamuzi yalikuwa ni ya Baraza. Wajibu wa serikali ni kwenda kutekeleza maamuzi ya Baraza na sio ya serikali. Serikali ilikuwa haina *option* kuwa na maamuzi mengine. (*Makofi*).

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kitendo hiki kilichofanywa na serikali, kwanza ni kulidhalilisha Baraza hili la Wawakilshi. Lakini pili kitendo kilichofanywa na serikali ni kitendo cha kuinyonga dhana ya utawala bora katika nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, kitendo kilichofanywa na serikali ni kitendo cha kuzidi kuchochea rushwa katika nchi yetu. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ninarudia kwamba kilichowasilishwa hapa ni mapendekezo ya Kamati ambayo Baraza zima iliyaridhia na serikali ikiwa ni sehemu ya Baraza. Sisi kama ni Wawakilishi ambao tulipitisha maamuzi yale hatuwezi tena kuliona Baraza hili linadhalilishwa chombo cha wananchi (*Makofi*).

Mimi kama nilikuwa ni mwenyekiti wa Kamati ile ambayo hivi sasa imevunjwa lakini kwa mujibu wa kanuni nilikuwa nina nafasi hii….

KUAKHIRISHA BARAZA KWA MUDA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa vile umeme umekatika naomba kuliahirisha Baraza hili kwa muda wakati utakaporejea umeme tutaendelea na shughuli zetu. Ahsanteni.

(Baraza lilirudia baada ya umeme kurudi)

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, naona sasa tufike pahala tuelewane. Katibu hapa anazungumzia suala la Kauli ya Serikali na kwenye order paper kuna Taaarifa ya Serikali. Sasa ipi ni Kauli ya Serikali au Taarifa ya Serikali. Hiyo moja ninataka ufafanuzi.

Lakini kwa mujibu wa Kanuni 44 (2) naomba nikinukuu kinasema hivi, “Taarifa ya Serikali inaweza kuzungumzia taarifa ya jambo lolote ambalo limechungumzwa na serikali au na mtu au taasisi yoyote kwa maelekezo ya serikali au jambo lolote ambalo limejadili na kulitolea maamuzi au mapendekezo au jambo jengine lolote ambalo serikali inahisi kuwa ni muhimu kwa ajili ya Baraza kupata taarifa na kulijadili kwa niaba ya wananchi”.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ilikuwa inahitaji ijadiliwe lakini ukiangalia kifungu cha 44 (3) kinasema Mwenyekiti wa Kamati inayohusika au Mjumbe mwengine aliyeidhinishwa na kamati atapewa nafasi ya kutoa maoni kwa niaba ya kamati kuhusiana na taarifa hiyo ya serikali.

Sasa naona Mwenyekiti yeye katangulia mwanzo badala ya kuanza kujadiliwa na baadae mwenyekiti akapata nafasi sasa na yeye kutoa maelezo yake. Kwa hivyo naomba tufuate Kanuni ya 44 ili mjadala wetu wende vizuri. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa imekubalika. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa mujibu wa Kanuni zetu kuna mambo mawili. Kuna Kauli ya Serikali na Taarifa ya Serikali.

Kauli ya Serikali ambayo ndio hata kwenye order paper ipo Kauli ya Serikali ipo chini ya kifungu cha 43. Kauli ya Serikali inapotolewa inatolewa halafu Mwenyekiti anapewa ruhusa au anapata nafasi ya kuzungumza na halafu kama kuna maswali munaruhusiwa kuuliza maswali.

Hii ni Kauli ya Serikali, kwa hivyo kinachotendeka baada ya kusema Mwenyekiti akishakumaliza unatoa ruhusa kwa Mjumbe kama atauliza maswali na maswali tena aliyetoa kauli atapata nafasi ya kuyajibu. Lakini kwa mujibu wa kifungu cha 44 Taarifa ya Serikali ndio kwa mujibu wa kifungu hicho cha 44 (4) inaruhusiwa kujadiliwa.

Sasa hii ni Kauli ya Serikali na sio Taarifa ya Serikali.

Nakushukuru.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, sahihi Mhe. Waziri wa Sheria alivyozungumza Kanuni lakini kifungu cha 44 (4) kinawataka Wajumbe kujadili Taarifa ya Serikali.

Mwenyekiti, humu sisi tunakwenda kwa taratibu za *order paper* na *order paper* inatwambia Taarifa ya Serikali. Kwa hivyo ni lazima tujadili na wala sio Kauli ya Serikali.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ukitizama *order paper* nambari 3 kuna Kauli za Serikali, ile ndio *heading* Kauli za Serikali. Sasa hiyo Kauli ya Serikali ndio Waziri anatoa taarifa lakini chini ya mwamvuli wa Kauli za Serikali. Kauli ndio *heading* na kwenye *order paper* ipo hivyo hivyo.

Sasa Kauli ya Serikali ndio ikamtaka Waziri atoe ile taarifa yake hiyo ya Kauli ya Serikali.

UTARATIBU

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili linaongozwa na taratibu, Kanuni na miongozo yake. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria anaelewa kwamba shughuli zinazoendeshwa katika kikao kinachofuata huwa taarifa zake zinapelekwa kwenye kamati ya uongozi na shughuli za Baraza kuthibitishwa.

Tulipokuwa kwenye Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza kama alikuwepo tulikubaliana kwamba taarifa hii ije kama Taarifa ya Serikali na sio Kauli ya Serikali. Ninadhani na wewe Mhe. Mwenyekiti, ni mjumbe wa kamati hiyo ya uongozi na shughuli za serikali pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria ni Mjumbe.

Kwa hivyo tulikubaliana kwenye Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza kwamba taarifa hii ije kama Taarifa ya Serikali na Waheshimiwa Wajumbe wapate nafasi ya kuijadili. Kwa hivyo kama kuna koseo ni hili la Kauli ya Serikali, hii ya mwanzo Taarifa ya Serikali ndio sahihi ndivyo tulivyokubaliana kwenye Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba tufuate taratibu za Baraza kama tulivyokuwa tumekubaliana.

Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri hapa alikwisha kuwasilisha Taarifa ya Serikali kama tulivyokwisha kumsikia mwenyewe alivyokuwa ameisoma. Sasa basi katika utaratibu huo kwa mujibu wa kifungu cha 44 (1) kinasema hivi, “Waziri anaweza kuwasilisha Taarifa ya Serikali katika Baraza kuhusiana na jambo ambalo Serikali inahitaji kuliarifu Baraza husika.

Lakini vile vile kifungu cha (2) Taarifa ya Serikali inaweza kuzungumzia taarifa ya jambo lolote ambalo lilichunguzwa na serikali au mtu au taasisi yoyote kwa maelezo ya Serikali juu ya jambo lolote ambalo serikali ilijadili na kulitolea maamuzi au pendekezo au jambo jengine lolote ambalo serikali inahisi kuwa ni muhimu kwa Wajumbe wa Baraza kupata taarifa na kulijadili kwa niaba ya wananchi.

Na kifungu cha (3) kinaeleza kwamba mwenyekiti wa kamati inayohusika au mjumbe mwengine aliyeidhinishwa na kamati atapewa nafasi ya kutoa maoni kwa niaba ya kamati husika na Taarifa hiyo ya Serikali.

Sasa hapa Mhe. Waziri alikwisha kutoa maelekezo yake na Mwenyekiti wa Kamati kwa kuangalia kile kifungu cha 43 ambacho mimi mwanzo nilikitumia alikuja na Mwenyekiti naye kutoa maoni yake.

Sasa imefika wakati wa Wajumbe kuweza kutoa maoni yao na kuweza kuchangia katika hotuba hii. Naomba ndugu Wajumbe waweze kuchangia katika hili. Mwenyekiti endelea.

Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati Teule): Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kunipa nafasi hii angalau nimalizie kwa maneno machache katika maoni ya kamati yangu.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema awali kw**a**mba serikali ilipaswa kwenda kuyafanyia kazi ama kuyatekeleza mapendekezo yale ya kamati kama yalivyoamuliwa na Baraza hili la Wawakilishi, na kwa mnasaba huo ninapenda nikazie maneno yangu kwa kunukuu *hansard* ya tarehe 20 Aprili, 2012 ambapo ilisema kwamba:

> "Nilitaka niseme hilo Mhe. Spika, na hilo ni jambo muhimu sana baada ya hayo Mhe. Wajumbe niwahoji wale wanaopokea na kukubali ripoti hii pamoja na mapendekezo na maelekezo mengine yaliyotolewa wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda". Kwa hivyo maamuzi ya kikao kile waliokubali walishinda.

Mhe. Spika, ripoti inakabidhishwa kwa serikali pamoja na mapendekezo yake na maelekezo ambayo mumeyakubali pamoja na vielelezo mbali mbali vitasaidia kwa sababu katika ripoti hii kuna baadhi ya mambo yanahitaji kuchukuliwa hatua za kisheria, vile vipo vyombo ambavyo kwa kawaida vinategemewa vifanye kazi hiyo. Kwa hivyo vile vielelezo kwa ajili ya kufanya rejea mpaka kufikia kuchukua hatua hizo za kisheria inabidi wawe navyo visaidie katika kazi hiyo".

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ninakadhia tu kwamba hoja ile ilikubaliwa na Baraza na mapendekezo yake na ilikuwa ni jukumu la serikali kwenda kuyatekeleza mapendekezo kama yalivyokubaliwa na Baraza ambapo serikali ilikuwa ni sehemu ya Baraza la Wawakilishi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tukiwa kama wajumbe tunasisitiza kwamba serikali iende ikatekeleza mapendekezo yale kama yalivyokubaliwa na Baraza. Kwa hivyo tunasisitiza kwamba serikali iende kuyatekeleza mapendekezo yale yaliyokubaliwa na Baraza la Wawakilishi bila ya kupunguza wala kuchakachua kitu chengine chochote na zaidi. (*Makofi*).

Kwa mnasaba huo ninawashauri Wajumbe wenzangu kwa kweli ile ripoti ya Serikali tusiipokee, warudi wakatekeleze mapendekezo haya. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaomba tukenda kwenye *hansard* tusisome sehemu moja tu ya *hansard. Hansard* ilisema hivyo lakini ninakumbuka kwamba serikali ilinyanyuka na ikasema inayapokea inakwenda kuyafanyia kazi na itatoa maagizo yake.

Hivi ni vyombo vitatu. Kuna serikali, Baraza la Wawakilishi na Mahakama. Kila moja ina uwezo wake na nguvu zake.

Baraza la Wawakilishi haliwezi kwa sheria ziliopo kuilazimisha serikali ifanye hivi, itatoa mapendekezo na ndio maana serikali ikasema kwamba inakwenda kuifanyia kazi. Isomeni hiyo *Hansard* au isomwe hiyo *Hansard* itizamwe, serikali ilisema inakwenda kuifanyia kazi na hiyo kazi iliyofanywa ndio hii iliyotolewa ripoti na serikali.

Ninapenda ieleweke hivyo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Wale ambao wanaotaka kuchangia tuwape ruhusa na kwa sasa tunampa nafasi Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, na ndio maana ukachukua muda mwingi sana ikawa ripoti hii ina utata kwa sababu tafsiri za watu; kila mtu hapa ana tafsiri zake za lugha za kufahamu.

Mimi ingekuwa haikuja hii ripoti basi ningesema kuwa serikali imetekeleza wajibu wa Kamati Teule. Lakini imekuja ripoti inaonesha dhahiri kuwa sasa wana kitu mvutano kati ya Kamati ya Teule na Serikali ndio maana ya kuja ripoti hii, Baraza *sorry*.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeona kwa sababu kilichokera majibu hayakuwa sahihi na *points* zenyewe zilizozungumzwa. Nitatoa mfano nakwenda kwenye umaskini mimi wa huyu kidawa.

Hata mimi sikuridhika na siipokei mimi ripoti hii kwa sababu serikali na wao wamefanya uchunguzi wa kiyakinifu kabisa na naamini hivyo. Lakini bado haikumtendea haki, hii nyumba ilikuwa wameshakabidhiwa serikali, ina maana bado serikali inajikubalisha kuwa wametoa wao na imetaifishwa hii nyumba. Hapa ndio nikasema bora tungesema kuwa ripoti hii isingeletwa hapa, hayo mambo yaliyokuwa yameshapita huko nyuma tungesema ndio, serikali imefanya jambo. Lakini imeleta ripoti hii, ndio hayo aliyosema Mwenyekiti, sasa inapingana na Baraza. Hoja ya Mhe. Abubakar Khamis, hoja ya Mhe. Salmin Awadh, hoja ya Mhe. Hija Hassan Hija na hoja ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, huyu mzee amefanyiwa *forgery is too much*, na mmekiri humu na kama mule kuna watu wenye akili ma-*professor* wamefanya kazi kwa uyakinifu kabisa, hawakubahatisha wale. Leo wanaambiwa waende mahakamani, hebu niambieni jamani si vichekesho hivyo, ni sheria gani itakayompeleka mahakamani tusidanganyane. Mimi ningekubaliana na ripoti hii kama ingekuwa yule mzee, na Kamati ilisema hivi asipewe hati mpaka huyu mzee amsaidie tena kwa kuonewa huruma Kamati imeogopa kumpeleka mahakamani yule mtu, alichukua hatua ya kuwaambia kuwa asaidiwe. Lakini bado serikali hatukuona haja ya kuweza kumsaidia huyu mzee.

Mhe. Mwenyekiti, mimi siikubali hii na nimesimama sio kwa kuiunga mkono, nimesimama kwa kuwa siikubali. Huyu mzee na yeye ana haki yake kama ni Mzanzibari, kwa nini jamani tuwadhulumu hawa wanyonge. Lilikuwa suala limekwisha, Kamati inamngojea yule mzee, amekwenda na ameshapewa haki yake kwa mujibu wa taratibu. Huyu mzee ametumikia kwa wale Wahindi, lakini ilipokuja mambo ya serikali kuchukua mali za wale hakuwa na tatizo yule mzee. Tatizo lililojitokeza ni kuwa amefanyiwa *forgery* saini zake madole matatu, hili dole la tatu ndio lipi.

Mhe. Mwenyekiti, tumekiri tumeambiwa muhusika mkuu aliyekuwemo katibu aliyeondoshwa na yeye kahusika katika kufanya ubadhirifu huo, serikali imeona hiyo, mbona haki yake jamani hapewi. Mhe. Mwenyekiti, tunasema Mhe. Waziri usitoe hati kabisa, japo una mamlaka kama tulivyoeleza. Waziri ana mamlaka ya kutoa hati na ndio mwenyewe hakuna mtu yeyote au kuhaulisha, lakini hiki kitu Mhe. Waziri unamuua mnyonge usitoe hati na wewe mzee wangu ni Al Hajj usitoe hati mpaka huyu mzee alipwe shilingi milioni 20,000,000. Kuna tatizo gani, shilingi milioni 20,000,000 kwa sasa hivi ni sawa sawa na shilingi 20,000 tu, maskini ya Mungu yule mzee.

Mhe. Mwanasheria yupo, hayupo hapa Barazani sasa hivi, kama angekuwepo mimi ningemuuliza hebu tutafutie sheria ambayo itakayomuwezesha yule mzee apande nao wale mahakamani. Jamani tusiganganyane bwana, siku zote jiwe dogo bwana halipigi jabali kubwa hata siku moja.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa kumtetea haki yake yule mzee wetu, dhambi jamani zisiwe nyingi. Mhe. Spika, juzi nakariri alisema kwamba ‘sisi ndio tutakaowajibika kwa Mwenyezi Mungu tutakwenda kusema nini’. Ninakariri tena alisema juzi hapa baada ya ile hoja yetu haikupita, basi alisema maneno mazito sana kwamba ‘sisi ndio tutakaowajibika kwa Mwenyezi Mungu tutakwenda kusema nini’. Maskini ya Mungu yule ametumika na amezeeka, leo tunakwenda kumnyang’anya. Mhe. Mwenyekiti, mimi naona nitalia machozi kwa kunyimwa. Mimi najivua, mwenzenu jamani nakwenda akhera safi kwa kumtetea haki yake yule mzee. Jukumu lenu nyinyi wazee na ni viongozi wangu wakuu, sikatai mimi kupewa lakini wale mliowataka kuwapa wapeni, lakini na yule naye lazima apewe haki kwa mujibu wa utaratibu wa Kamati Teule ikisimamiwa na Mwenyekiti wake pamoja na wahusika zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa hili siungi mkono na siipokei.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nikushukuru, lakini nataka niseme maneno matatu mafupi. Mimi niwaombe Wawakilishi wangu kwamba wakumbuke kuwa hili ni Baraza la Wawakilishi. Kwa mujibu wa kifungu cha 5A cha Katiba hii huu ni muhimili wa dola ambao kazi kazi yake kubwa ni kusimamia utekelezaji wa

serikali. Kwa hivyo, tusikubali hata siku moja kuchezewa na yeyote atakayekubali kuchezewa ni msaliti na haitendei haki nchi hii na Katiba hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilidhani kwamba serikali ingetuambia kwamba ripoti hii imewagusa wakubwa na haitekelezeki, iko wazi. Lakini hii tabia ya kutuambia kwamba tujadili wakati Katiba haisemi hivyo kwa kweli ni unyonge.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa ni Mjumbe wa Kamati lakini tulisema hapa kwamba kuna ushahidi wa karatasi mpaka Hansard. Tunapoambiwa kwamba kuna watu tumeongezea wakati Hansard ipo haisikilizwi, kwa kweli ni unyonge mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano kwenye kumiliki asilimia 10 ya Hoteli ya *Misali Sun Set Beach* ni Mhe. Machano, tuliambiwa wazi wazi na Hansard ipo kwamba aliwaomba asilimia 10 ili awalinde. Leo Kamati inaambiwa kwamba ilifanya sivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba ripoti hii isipokelewe, isijadiliwe na bora wakae nao ili wananchi wa Zanzibar waone kwamba *GNU* kazi yake ni kulinda waovu. Mhe. Mwenyekiti, *Hansard* zipo, wote tuliowahiji walikiri kwa mdomo wao, kwamba sisi tunayafanya haya kwa nguvu ya huyu. Leo serikali haikuchukua Hansard, inakusudia kupotosha kama kwamba Baraza hili lilisema uongo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba katika Wajumbe wale wa Kamati na Baraza zima hakuna Mjumbe mwenye chuki na mtu, kila mtu alihojiwa huru na alitoa maneno yake mdomoni mwake. Sasa kama kuna mtu alitoa maneno mdomoni mwake akasema tukarikodi, halafu leo tunaambiwa ni uongo.

Mhe. Mwenyekiti nawashauri sana Wawakilishi wenzangu waliochaguliwa na wananchi wanyonge kwamba ripoti hii tusiipokee, tuwarejeshee serikali ili Wazanzibari waone kwamba GNU kazi yake ni kulinda waovu. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kusema kwamba tumemsikia Mhe. Mohammed Aboud juu ya taarifa kuhusu utekelezaji wa ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi, juu ya maamuzi ya serikali juu ya ripoti ile.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, sitozungumzia juu ya taarifa ile ya serikali ambayo imewasilishwa, lakini ninachotaka kusema ni kwamba chombo hiki ni kikubwa, pamoja na kwamba Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984 ibara ya 5 imezungumzia mgawanyo wa madaraka, ama imetoa ufafanuzi juu ya mamlaka ya utendaji kwamba ni serikali, lakini mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma ni Baraza la Wawakilishi. Shughuli za umma maana yake ni shughuli zinazosimamiwa na serikali.

Kwa hivyo, chombo hiki kwa mujibu wa Katiba ndicho chombo pekee kinachoweza kuisimamia serikali na kutoa maamuzi juu ya serikali yenyewe. Kusimamia sio kuangalia tu, lakini na kutoa maamuzi. Nakumbuka Kamati Teule baada ya kutoa ripoti yake Baraza hili lilikubaliana na maamuzi ya Baraza lile kwa serikali.

Nguvu za kuendesha nchi zitatokana na wananchi wenyewe. Hapa ndipo kwenye Wawakilishi wa wanachi ambapo nguvu za wananchi zipo katika chombo hiki. Sasa kama kuna azimio ambalo limetolewa na chombo hiki cha kuitaka serikali ikatekeleze, halafu leo Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria anatuambia chombo hiki hakina mamlaka sio sahihi. Ni lazima tufahamu kwamba chombo hiki ndicho chenye mamlaka kwa serikali, kwa mujibu wa Katiba hii ya Zanzibar kifungu cha 9 na cha 2. Lakini pia kwa mujibu wa Katiba ibara ya 5 ambavyo vimeipa mamlaka chombo hiki ya kuzisimamia shughuli za utekelezaji wa shughuli za umma.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama Waziri wa Katiba na Sheria yeye ambaye ndiye anayetakiwa asimamie Katiba hii na utekelezaji wake na kuona kwamba chombo hiki hakina mamlaka yoyote ya kuiambia serikali juu ya maamuzi ya wananchi, nadhani hatutendewi haki. Mara zote Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein husema kwamba huu sio wakati wa kuwababaisha watu, wakati wa kubabaisha watu umepitwa na wakati, kwa sababu wananchi sasa hivi wanaelewa kila kitu na kila mtu anaelewa. Kwa hivyo, suala la kubabaisha sasa hivi halina nafasi katika serikali hii. Kwa hivyo, ni lazima tuwe wakweli, tusimamie vizuri ili kusiwe na masuala ya ubabaishaji katika masuala ya kusimamia maslahi ya umma.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kujenga hoja yangu hiyo kwamba sote tuelekee katika kutenda haki kila mmoja kwa nafasi yake. Lengo na madhumuni ya chombo hiki ni kusimamia serikali katika utekelezaji wake wa shughuli za wananchi. Suala la kubabaisha sasa hivi lisipewe nafasi katika masuala haya. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi kusema mambo mawili. Mimi nadhani tujadili zaidi utaratibu, kwa sababu kama utakumbuka Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi Wajumbe wako walikuwa wakidai kuundwa kwa Kamati Teule, na mara nyingi serikali huko tunakotoka walikuwa wakikinga kifua sana kwamba Kamati Teule isiundwe na kwamba serikali ingeunda kamati ya kuchunguza lile lililotokea. Wajumbe wakawa hawakubaliani nayo kwa sababu haiwezekani serikali ikafanya mambo halafu ikarudi ikajichunguza yenyewe ikawa adilifu, hilo lisingewezekana.

Ahsante Mwenyezi Mungu kwamba katika zama tulizonazo, Mhe. Spika, sasa anaridhia kuundwa kwa Kamati Teule. Kwa hivyo, kilichotokea ni nini, Kamati Teule imeundwa, imekwenda kuchunguza mambo na imeona, kwa mujibu wa majukumu yake ndio ina- *over site* serikali, kwa hivyo yale yaliyopendekezwa na Kamati Teule, Kamati Teule ni ya Baraza, maana yake ni Baraza lililopendekeza, Baraza limeagiza. Mimi nilikuwa nadhani serikali iondoe muhali, maana inachokihangaisha serikali ni kwamba serikali inaona muhali kuwajibika. Waliotenda kosa wapo kwa mujibu wa ripoti ya Kamati Teule, ushahidi umo na vielelezo vimo. Mimi nashangaa sana serikali kusema hakuna ushahidi.

Sasa mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, serikali ijifundishe na ijizoweshe kuwajibika. Mimi nahisi hapa pana mgogoro, kuna vyombo viwili vinavutana. Baraza linasema ndio majukumu yake kuiambia serikali kufanya hivi, na serikali inapaswa kufanya hivyo. Lakini kwa upande mwengine serikali inasema hapana ni lazima tuchakachue, hili tutafanya na hili hatufanyi. Mimi nadhani tuiangalie zaidi sheria inaelekeza vipi. Maana ilifika pahala mimi nikasema ikiwa mvutano utakwenda hivi, mazingira haya yanaonesha sasa ripoti ya Kamati Teule sasa tuipeleke kwenye muhimili wa tatu mahakama ikatuambie ni nani yuko sahihi. Sasa huko ni mbali sana, nilikuwa naomba tukubaliane kuwa ile ripoti ya Kamati ifanyiwe kazi na huu mgogoro umalizike.

Kwa mantiki hiyo Mhe. Mwenyekiti, haya yaliyosomwa hapa kama taarifa ya serikali ambayo ndani yake muna uchakachuaji wa yale maagizo ya Kamati Teule na mimi binafsi siipokei kabisa, kwa sababu sio utaratibu mzuri. Serikali irudi ikaifanyie kazi ripoti ya Kamati Teule iliyoundwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tuendelee na utaratibu wa kuleta vi-*note* vyenu mbele ili tuweze kwenda katika utaratibu wetu wa kawaida. Mhe. Subeit Khamis endelea.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu. Kwanza nashangaa sana kwa sababu ripoti ililetwa baada ya kuundwa Kamati Teule na kwenda kuchunguza, na ripoti ililetwa kwenye Baraza letu ikasomwa, tukaipokea na kuishangiria na serikali ikapewa jukumu la kwenda kuifanyia kazi kwa utekelezaji. Mimi nashangaa sana kuona kwamba serikali imekuja tena na yale mapendekezo ambayo iliyakubali badala ya kwenda kuyafanyia kazi imekwenda kuyachakachua na kuyagawa. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba bado serikali yetu haijawa tayari, tunaunda Kamati Teule, tukishaunda na Kamati Teule na ikishaleta ripoti, sasa serikali haijawa tayari kuyafanyia kazi, bado kuna nafasi ya kuwa inawalinda watu. Mimi najua huu ni woga wa serikali ambapo bado inawalinda watu kwa yale maovu.

Kwa hivyo, serikali isiwe na muhali kutekeleza yale ambayo yameonekana kwamba ni mabaya. Kwa maana hiyo mimi nasema kwamba hapa hakuna mjadala tena mkubwa, isipokuwa nasema kuwa na mimi naungana na wenzangu kwamba ripoti hii siikubali na siipokei, kwa sababu ripoti ya Kamati Teule ilimaliza kazi na ilitekeleza yale majukumu yake kwa ushahidi kamili na kila kitu kiko bayana. Sasa hapa utata ni nini na uzito ni nini ni utekelezaji. Bado serikali ikae kitako ione kama ina wajibu na kuleta tena hii ni kulidhalilisha Baraza lako, kwa sababu Baraza limefanyakazi limekubali. Leo tena kurudishwa ripoti hii tena kikali na kuna uchakachuaji haya tunayakubali na haya hatuyakubali, hii ni kulidhalilisha Baraza. Sasa sisi hizi Kamati Teule tunaziunda za nini, lakini bado serikali haijawa tayari kuzikubali hizo Kamati Teule, ikiwa iko tayari serikali kuzikubali Kamati Teule, basi ripoti zinapoletwa ingekuwa sasa serikali wajibu wake ni utekelezaji tu.

Kwa hivyo, na mimi siikubali ripoti hii, siipokei na siikubali. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii. Mimi sitokwenda katika mambo ya kujadili. Nadhani Mhe. Mwenyekiti, kwanza niungane na wenzangu kwa kutoipokea hii taarifa, siipokei taarifa. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kinachohitajika sasa hivi, baada ya ufafanuzi alioutoa Mhe. Salmin Awadh Salmin, baada ya *quotation* ya Katiba na kanuni, na baada ya maelezo ya Waheshimiwa Wajumbe, kinachohitajika ni mambo mawili tu na sio kujadili. Yanayohitajika ni mambo mawili tu yaani ni maamuzi ya Baraza ni mambo mawili tu. Utoe amri Mwenyekiti ya kuirudisha serikalini au Baraza tuamue kwamba tunaikataa moja kwa moja na serikali irudi ni mambo mawili tu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ikiwa Wajumbe waendelee kujadili hii hoja ambayo Baraza halitaki kuipokea, basi naona itakuwa ni kupoteza muda. Baraza haliwezi kuwa nokoa wa serikali siku zote, serikali inatakiwa itekeleze maamuzi yetu Baraza, ahsate. Siungi mkono na wala siipokei taarifa hii.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, lakini ningependa hayo yawe ni maamuzi yako, wengine waache waendelee kwa taratibu zao. Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kupata fursa hii adhimu katika suala zima ambalo linajadiliwa sasa hivi, suala zito ambalo sisi Wajumbe wako linatuumiza vichwa sana. Mimi niungane na wenzangu Mhe. Mwenyekiti, wale ambao kwa namna moja ama nyengine tumefikia pahala tunaona kwamba haki haikutendeka katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, sababu ya kusema hivyo, nilijenga dhamira, nilijenga hisia. Pale karibuni tu baada ya kufikia ule uteuzi wa Manaibu Mawaziri pamoja na watendaji wakuu wa serikali, nikasema kwamba lile ambalo Baraza walilitaka, sasa Rais wetu kwa hekima na busara zake, ameanza kulifanyia kazi. Kwa sababu wale watendaji walioondoka ndio wale watendaji ambao kwa namna moja ama nyengine ripoti ile ya Kamati Teule ilikuwa inawagusa. Hayo ndio yalikuwa matarajio yetu kwa siku hii ya leo, tulihisi kwamba taarifa hii ingekuja kutuelekeza au kutueleza yale maamuzi ambayo tayari yameshafanyiwa kazi na yale ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi.

Lakini ukisoma kwa haraka humu Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya maeneo tayari yameshafanyiwa kazi, lakini kuna baadhi ya maeneo ndio yale ambayo mimi na wenzangu tunahisi kuwa yamekuwa na ubabaishaji, hayakuwa na maamuzi. Imekuwa leo tunafikia pahala tuko katika hali ya kuchunguzana tu, mtu anamchunguza mwenzake na anayechunguzwa na yeye anasema hukunichunguza vizuri, ngoja na mimi nijichunguze. Ndio hali halisi inayoonekana katika ripoti hii na ambayo inatupa kigugumizi kikubwa sana, hata baadhi ya taarifa zake ukiangalia katika suala zima lile la kifusi, kwa kweli huoni kama kuna uzito wa serikali ambao umeleta na kutufanya sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuikubali hii ripoti.

Mhe. Mwenyekiti, mtu anakuambia kwamba wamelichukua dongo wameona Shakani mbali ndio wameona bora waende wakalitupe baharini karibu na eneo. Lakini ukiangalia kwa mantiki Mhe. Mwenyekiti, kuna vitu viwili. Kuna hasara ya kifedha, lakini kuna hasara ya maisha ya binadamu, kwa sababu kuifukia bahari pasipo na kufuata utaratibu, inaweza bahari ile ikaja kuwaangamiza watu tukaua watu wengi. Kwa hivyo, ukiangalia Mhe. Mwenyekiti, bado hii ripoti ina mapungufu makubwa, na mimi niseme kwamba kuna haja na nimshauri Mhe. Waziri, hii ripoti arudi na aende akaifanyie kazi tena ili atuletee na kuweza kuichangia kwa manufaa na maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, naomba kukaa. Ahsante.

Mhe Rufai Said Rufai: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kupata hii nafasi ili nitoe maelezo yangu kwa ufupi kabisa. Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi siungani na hoja hii iliyoletwa na serikali, kwa sababu ukiangalia katika hoja hii maeneo yote ambayo wahusika ni miongoni mwa watu wa serikali, basi kumetafutwa sababu na hoja za kuwatoa katika malalamiko yale. Lakini maeneo yote yanayowahusu wananchi wetu, basi hayo serikali ndio waliyoyakubali katika hoja hii. Kwa hivyo, inaonesha wazi kabisa kwamba serikali yetu bado haijawa tayari kutekeleza wajibu wake.
Kwa hivyo, mimi nitawaheshimu sana Waheshimiwa Wajumbe. Leo tuna hoja hii iliyofikishwa hapa na baadae tutazungumza hoja ya Baraza la Manispaa, tukitoa mwanya basi hakuna hoja yoyote itakayokuwa halali hapa Barazani. Kwa hivyo, ni vyema tujali nguvu tulizozipoteza za wananchi, jasho lao kuhusu pesa zao za kodi na tujali

Tume tunazoziunda na kazi yao kubwa waliyoifanya. Kuna wenzetu wengine hivi sasa wako majeruhi hapa, wako taabani. Leo tukifikia tuone hili ni jambo la kawaida, basi hatima yake nchi hii itakwenda na maji. Kwa hivyo, niwashauri sana kabisa kuwa hoja hii irudi ili serikali ikafanye wajibu wake. Aliyefanya makosa awajibike kisheria kama maelezo yalivyo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza na mimi napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, lakini kwa kupata hivi vioja vya leo tunavyoviona.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niungane na wenzangu kutoikubali hii ripoti. Mhe. Mwenyekiti, kinachoshangaza katika uamuzi wa kuikubali ripoti hii huko nyuma Mhe. Waziri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais alikuwa ni mtu wa kwanza katika Mawaziri ambao wameunga mkono kwamba ripoti hii haina matatizo na inapokelewa. Lakini cha kushangaza leo hii kuna mambo humu haya tuliyoelezwa humu naona hayana maana hata pesa mbili, yaani hata mtoto mdogo ukimleta hapa basi ataikataa hii.

Jengine yeye ni sehemu ya Baraza hili, kwa hivyo ina maana yale maamuzi yake ya kuikubali hii anayapotosha au anayakanusha yeye mwenyewe. Mhe. Mwenyekiti, watu walihojiwa wao wenyewe kwa mujibu wa ripoti ile tuliyoisoma walikubali wenyewe, kwa hivyo, walikuwa na makosa. Sasa mtu mwenyewe akubali kuwa kafanya kosa halafu huku watu wengine waseme kuwa hajafanya kosa. Hapa mimi nakuomba Mhe. Mwenyekiti kwa hili kama upo uwezekano basi wakatafutwe watu hao, Waziri awepo na Kamati iwepo mahojiano yafanyike na *record* zote zioneshwe kama zilikuwa ni za TV au redio ili tuone ukweli wa hili, lakini kwa hili hatuko pamoja na wao ni lazima lifanyiwe kazi na tuone ukweli wake.

Mhe. Mwenyekiti, hatutaki tena kusikia maji yakishamwagika hayazoleki, kwa sasa lazima aliyemwaga maji katika ndoo akamatwe aadhibiwe kwa mujibu wa sheria hatuwezi kupoteza pesa kila siku kwa kuunda Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, kama unakumbuka tulipokuwa tunaunda Kamati hizi nilisema mimi serikali kila siku itakuwa inaunda Kamati na kupoteza pesa za wananchi, na hili ndilo limetokezea. Mapesa mengi yameharibiwa hakuna lolote lililofanyika mpaka hivi sasa. Suala hili siungi mkono na hatukubaliani nalo hili, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chaani hili hatulikubali. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nataka nikushukuru sana kunipa nafasi hii na mimi nikazungumza machache, aidha iwe kauli au ripoti ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, tayari tumesharekebisha na Mhe. Waziri alipokuja hapa aliwasilisha taarifa ya serikali. Tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuchangia taarifa ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, taarifa hii sijaipokea na wala sitaipokea. Kwa kweli bado hatujabadilika na sijui kama tutabadilika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi naiomba sana serikali hebu tuwape matumaini wananchi wetu tunaowaongoza, waamini kwamba wameiweka serikali yao makini, ambayo itaweza kuwatendea haki wanyonge na kila mmoja aweze kupata haki yake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati *Wallahi Laadhim* ninaapa kwa mara nyengine tena leo ingawa sina Msahafu, katika ripoti ile hatukumlenga mtu wala kumdhamiria mtu vibaya, isipokuwa tulijitahidi kutenda haki na tukaleta ripoti, ili serikali ijijue ni udhaifu maeneo gani na iweze kujirekebisha maeneo gani, ili tuende vizuri. *(Makofi)*

Baada ya ripoti yetu naamini hata utendaji ndani ya serikali ulibadilika, yaani watendaji walianza kubadilika kwa kuona kwamba hivi sasa hakuna nafasi tena ya kufanya kazi kwa kutegemea mgongo wa mtu au kutegemea kuwa kuna mtu hata nikifanya kosa basi atanibeba. *(Makofi)*

Kwa kweli wengi walikuwa wanategemea taarifa hii serikali ingelisema tumechukua hatua moja, mbili, tatu, nne katika angalau kuwawajibisha baadhi ya watendaji, yaani iwe katika ripoti yote hii hakuna mtu aliyefanya kosa aa! Mimi nadhani hatuitendei haki nchi yetu na wala watu wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Waziri pale kwamba sisi Kamati yetu tulitumia fedha kwa ajili ya kuifanya hii kazi. Sasa kwa bahati kuna Kamati Teule nyengine tumeziunda kwa matumaini kwamba kwa kuwa kuna ripoti ya Kamati Teule serikali imeahidi kuwa itakwenda kuitekeleza. Kutokana na hali hii, basi sitegemei kama na hizi ripoti nyengine zitakazokuja kama zitakuwa na maana yoyote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni *watchdog*, maana yake ni walinzi wa mali za umma. Sasa leo sisi walinzi wa mali za umma tumeshasema kwamba mali hii imepokonywa irudi serikali tena kwa ushahidi na wala sisi hatukuja na ushahidi wa maandishi tu mpaka *hansard* za maneno. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kila ninavyotaka kusema naona nitaharibu. Sasa mimi nataka nitoe tahadhari tu, kwamba hata hizi Kamati zetu tunapokwenda kwenye mawizara hivi sasa Mhe. Mwenyekiti Wajumbe wako watadharauliwa sana, kwa sababu wataonekana si chochote wala si lolote, kwani hawa waliotenda makosa wanajijua kama wametenda makosa na serikali inakiri kwamba hawakutenda makosa. Kwa hiyo, tutegemee mtu ataweza kujirekebisha kweli. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunatembea tumekwenda China na katika nchi ambayo tunaisifu kwamba ina maendeleo makubwa ni China, Mhe. Mwenyekiti bado hatujajifunza chochote mpaka hivi sasa. Kwa mfano, wenzetu China wameendelea kutokana na uwajibikaji, Zanzibar bado hatujakubali uwajibikaji *business as usual*. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nadhani jambo lililobakia ni kwamba serikali ilete ripoti zake tuwapongeze, tuwasifu tuendelee. Vile vile na wale ambao wanaoendelea kutafuna mali za umma, wache waendelee kutafuna, kwa sababu hatuoni kama kuna nia ya serikali kweli kuweza kuwasimamia watendaji wake na kuchunga nidhamu katika utendaji wa serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuzungumza eneo moja tu, sisi hatukusema kwamba hoteli ya Wesha ikaezekwe mabati, leo ripoti inasema makuti au mabati. Kwa kweli tumesema eneo lile halikupaswa kuwekwa mradi wowote, na hiyo ilikuwa ni kauli ya serikali, kwamba eneo lile lipo katika *reserve* ya utafiti na uchimbaji wa mafuta, *other wise* watendaji wenu wa serikali wametudanganya. *(Makofi)*

Pia jana nilimsikia Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati akizungumza hapa kwamba katika maeneo yote ambayo yamewekwa *reserve* kwa ajili ya *research* ya uchimbaji wa mafuta yatafutwa, na leo tunakuja kuambiwa hoteli ile imeezekwa makuti, sisi tulisema kwamba imeezekwa makuti pale. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nadhani tutendeane haki, sisi hii kazi na haya mambo mengine tumeyapata kutokana na malalamiko ya watendaji wenu wenyewe wanavyoona mambo hayaendi vizuri. Kwa mfano, leo hata kukifanyika ubadhirifu unafikiri watatwambia, hawawezi kutwambia, nchi itatafunwa na kila siku *Program* ya Kuondoa Umasikini (MKUZA), *Vision* 2020 hatuendi popote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba tuwaonee huruma wananchi wetu, kwa sababu wananchi wetu wanyonge kula ya asubuhi inawashinda. Sasa leo tunapokuja sisi Wawakilishi wao kuja kuzungumzia ni namna gani serikali iweze kuwajibika, ili hiyo nusu shilingi inayopatikana iweze kuwafika na wao, leo serikali inatuletea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nafikiri serikali haikututendea haki na mimi ripoti hii namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais aichukue na wala wasijewakatujibu, basi tunaomba angalau wakaifanyie kazi kimya kimya, hatuna haja tena kujibiwa isipokuwa tunataka ikafanyiwe kazi kimya kimya. Ninaamini hata katika hayo mabadiliko yaliyofanywa ripoti yetu ingawa haikutajwa lakini imezingatiwa na sisi ni watu wazima tuna akili zetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nataka nikushukuru angalau na mimi kutoa maoni yangu. Kwa kweli sitegemei ripoti ya Shirika la Umeme na ile ya Baraza la Manispaa, nafikiri *business as usual*. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti na ripoti naikataa. *(Makofi)*

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu *Subhanahu Wataala* aliyetujaalia uhai na uzima tukawepo hapa, kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa hili.

Vile vile nikushukuru na wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika mada iliopo mezani wakati huu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na utangulizi wangu kwa kusema yafuatayo. Muhali ni mtoto aliyezaliwa Zanzibar na baada ya kuzaliwa kwake mtoto huyu amepoteza uwajibikaji, uadilifu, nidhamu na uwazi katika utendaji wa kazi. Kwa kweli jambo hili la mtoto huyu muhali ndilo ambalo limetufikisha hapa tulipo.

Kwa hivyo, nadhani Baraza hili liliamua na hichi ni chombo ambacho wanakitegemea sana wananchi, tukaunda Kamati Teule na ikakamilisha hilo na ripoti wakaifikisha huko. Lakini matokeo yake tulidhani kwamba serikali itachukua nafasi yake ya kuifanyia kazi ripoti ya Kamati hii Teule. Jambo la kustaajabisha ni kuona kwamba serikali nayo imekwenda kukaa na kupanga tena mapendekezo mengine badala ya yale ya Kamati Teule kuyafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba serikali haijawatendea haki wananchi, kwani kuna wengi ambao wamo katika sekta tofauti wenye kupoteza mali za umma. Kutokana na hali ya ripoti hii ambayo imeelezwa wazi wazi ukiukwaji wa utaratibu, kanuni, Katiba na sheria tofauti, na watu walijieleza wenyewe kutokana na usaili wa Kamati hii siwezi kuunga mkono kabisa.

Kwa hiyo, siungi mkono na wala sitaunga mkono na kufanya hivyo ni makosa, kwa sababu sisi tunatumia nguvu za wavuja jasho, ambao ni wanyonge kodi zao na tunakuja hapa kwa ajili ya kutetea maslahi yao. Kwa kweli naamini fedha hizo ambazo zinapotea zinafanyiwa upotevu wa makusudi au kwa kutumia mtoto huyu muhali wa kuoneana haya sidhani kama tutafikia malengo.

Mhe. Mwenyekiti, sikuwa na mengi ya kuyaeleza, lakini na mimi niliona nisimame hapa kuikataa ripoti hii, nasema serikali ichukue nafasi ya kwenda kuitumia hii na haya mapendekezo iyafanyie kazi Kamati baada ya kuleta mapendekezo yake haya.

Kwa hivyo, ni vyema serikali kukaa na kuona kwamba ipo haja ya kuwawajibisha wale ambao wote wamehusika na kadhia hii. Lakini sikuja kusema haikumhusu au haikumgusa wakati huku wahusika wote wamehusika kwa asilimia mia moja wamejieleza wenyewe, na wengine ni watendaji wa shughuli za serikali wanahusika hao, kwa sababu wamesema ndio watendaji katika hizo sekta zilizoguswa na wanasema liko hili na lile, lakini serikali inakataa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme hili kwamba mtoto huyu muhali aliyezaliwa Zanzibar kwa kuoneana haya baina ya mjomba na shangazi hatutafika tunakokusudia, Wazanzibari ni ndugu sote wa kifamilia, lakini maendeleo ni jambo ambalo tunalihitaji. Sasa kama tunakaa na mtoto muhali, basi tuelewe kwamba hawa waliotuchagua ambao wanaojenga matumaini kwa serikali yao huku ni kuwavunja moyo.

Kutokana na hali hiyo, niiombe serikali inapotumia nguvu za walipa kodi kwa ajili ya kufanya jambo maalum la uchunguzi, basi ni muhimu sana kurudia kwenye ripoti hizo na kuzifanyia kazi. Kwa kweli ni imani yangu kwamba serikali kwa kauli hizi za Wajumbe wa Baraza hili tukufu, ambalo ni muhimili mwengine basi itaifanyia kazi angalau wananchi wajenge imani juu ya hili.

Baada ya kuyasema hayo narudia tena mimi siipokei ripoti hii. Mhe. Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi kutoa maoni yangu kuhusu taarifa hii ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mtu mzima akilia huwa kuna jambo, nasema hivyo kwa sababu ya msingi mpaka Wajumbe wa Baraza lako tukufu hili kufikia kuundwa kwa Kamati Teule kulikuwa kuna jambo. Kwa kweli Mhe. Spika kukubali kuundwa kwa Kamati Teule hiyo na kuteua Wajumbe wa Kamati hiyo pamoja na kuwapa uwezo wa kwenda kuchunguza, hili ni jambo zuri sana.

Kwa hivyo, walikwenda kuchunguza na ripoti tukaletewa hapa na baada yake kuipokea na kuiunga mkono, baadaye ikarudi serikalini kwa ajili ya kwenda kufanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba ‘ukichelea mwana kulia hatimaye utalia wewe’. Maana yake ni kusema kama utaogopa kuwawajibisha watu waliotenda ubadhirifu ndani ya nchi hii, basi siku zote itakuwa hatufiki

shughuli tuliyokusudia. Kwa hiyo, maisha yetu tutasema kwamba serikali yetu ni changa na wala hatutapevuka hata siku moja. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, nasema ripoti hii ya serikali siiungi mkono na wala sitounga mkono, kwa sababu kama nitaunga mkono sitawatendea haki wananchi wangu na Zanzibar kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, imefika wakati na Mhe. Rais anasema kwamba tusifanye kazi kwa mazoea na kama tusifanye kazi kwa mazoea, basi haya leo ndio mazoea ikiwa hatutachukua hatua ya kuwawajibisha wote waliotenda maovu, kwa sababu Kamati imefanya kazi zake vizuri tena kwa ushahidi kamili, na mpaka leo wana msimamo kwamba ushahidi upo. Kwa hiyo, ni wajibu wetu kuirudisha ripoti hiyo ya serikali kwa ajili ya kufanyiwa kazi na wala isimuonee mtu aibu.

Kwa hayo machache nasema ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi hii kwa kupata nafasi angalau ya kuchangia machache katika taarifa hii ya serikali ambayo tunaijadili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli neno muhali kama alivyosema Mhe. Ashura Sharif Ali kwamba tumezaa mtoto muhali kama hatukumpiga mateke huyu, basi atatupiga mateke yeye.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama tunavyoisifu hapa kwamba serikali yetu ni sikivu basi isiwe kinyume chake na iwe ni sikivu kweli. Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti, tunapokwenda kwenye mawizara tukaangalia katika ufuatiliaji wetu wa shughuli zetu mbali mbali za Kamati tunakutia maovu mengi na tunayafumbia macho kiasi fulani na mengine tunayafumbulia macho kiasi fulani.

Sasa Baraza la Wawakilishi lilipodai kuundwa kwa Kamati Teule ni kwa sababu ya kuona kadhia mbali mbali zilizomo kwenye watendaji wa serikali wa sehemu tofauti.
Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwamba hakuna njia yoyote itakayotupa ukombozi hapa Zanzibar isipokuwa uaminifu, uadilifu na ukweli, basi tuwe wakweli. Kamati Teule bila ya shaka ilipoleta taarifa yake ilisema kwamba yale yote waliyoyaeleza wana ushahidi na *hansard* wanayo mkononi, hivi leo tuna kigugumizi gani cha kutekeleza yale ambayo yameonekana na *hansard* yake ipo.

Kwa hivyo, katika kutoa hoja au maelezo ya kuichangia Kamati Teule ripoti yake kipindi kile nataka nirejee maneno ya Mhe. Subeit Khamis Faki, alisema haya yaliyotajwa kwenye Kamati hii kuna maburungutu mengi kwa watendaji wa serikali kwenye wizara nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, tutakapokwenda kombo katika utekelezaji wa kuichukulia hatua hotuba hii basi tunawapa mwanya watendaji mbali mbali wa serikali kuhujumu mali na uchumi wa nchi yetu ya Zanzibar.

Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chambani siipokei taarifa hii, na nasema kwamba serikali iichukue na ikaifanyie kazi na yeyote anayestahiki kuwajibika, basi asionewe haya awajibike, kwa sababu unapomuonea haya mtoto wa shangazi basi shangazi yako haitwi bibi. *(Makofi)*

Kwa haya machache nasema kwamba siipokei ripoti hii na ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kusema maneno mawili, matatu kuhusiana na taarifa hii ya serikali.

Pili namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama katika chombo hichi kuweza kuyasema hayo mawili matatu.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, nimeshtushwa tena inanitisha taarifa hii ya serikali, kwa sababu kesho kutwa kuna Kamati nyengine Teule itakayochunguza mambo magumu zaidi ya haya, ambayo pia taarifa yake itakujaifanya kama ilivyoifanya hii. Sasa itakuwa sisi kazi yetu ni kuzitumia fedha za serikali kwa ajili ya kuunda Kamati Teule na hatimaye serikali ikafanya vile ambavyo inahisi kwa upande wao ndio sahihi.

Kwa hivyo, kazi yetu, wajibu wetu wa kuisimamia, kuishauri na kuikosoa serikali itakuwa hakuna haja yoyote, lakini sisi tunao wajibu wa kufanya hayo yote.

Mhe. Mwenyekiti, nimetizama namba 5(3) kuna kasoro zilizotokea kwenye suala fulani na serikali imekubali kuwa kasoro ipo, lakini bado kuchukua hatua inaonekana ni kwenda kinyume na hilo suala lenyewe, kasoro serikali inaikubali na kuchukua hatua ikawa ni kinyume na sheria, *I don't understand*, kwamba ni kasoro lakini kuchukua hatua ni kwenda kinyume na sheria. Sasa hapa mimi binafsi sijui na serikali sijui itatueleza nini.

Kutokana na hali hiyo, mimi na wala sio kwa kuwaiga wenzangu siipokei taarifa hii ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Mwenyekiti, kama si kanuni zako zinazotuelekeza ilikuwa mwanzo wa taarifa hii utuulize hii taarifa tunaipokea au hatuipokei. Kwa hivyo, nafikiri baada ya kusikia michango ya wengi hapa ingelikuwa ni jawabu hatuipokei, lakini kwa vile kanuni haikuruhusu basi umetupa fursa ya kusema mawili matatu.

Kwa kweli mimi nasema hichi ni kitendo cha aibu tena ni aibu kubwa sana, kwamba leo Wawakilishi wa wananchi waliotutuma kuja hapa tukaona kuwa kuna tatizo fulani kwenye serikali inayowatawala, labda niseme hivyo na nisiseme inayowaongoza hawakusikia yale ambayo wananchi wametutuma tuyaseme. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sijui kwa nini tunaunda mechi hapa, kwa sababu kila nikitizama naona kuna mechi leo tunayoitengeneza kati ya *executive* na *legislature*, kwa nini yafike haya. Sisi kila mmoja ni muhimili na Katiba imesema nchi yetu itakuwa na mihimili mitatu na ipo na muhimili huu umekamilika.

Sasa kinachonishangaza kwamba sisi kama ni muhimili uliokamilika ina maana leo inafika wakati tunapeleka taarifa kuiambia serikali hatuaminiki kiasi kwamba atokee mwengine na yeye akasahihishe ile ripoti tuliyoileta leo, itakuwa tumeaminika vipi. Kwa hivyo, nafikiri ni vyema serikali ikae na tuheshimiane mihimili yote mitatu, kwamba muhimili huu umeshasema kwamba kuna hili, basi iheshimike kauli yake kwa nini iwe leo tena sisi tuonekane hatuna faida yoyote. Mimi naona kama nimedhalilishwa kwamba chombo changu kama hichi kilichoaminiwa na wananchi kije hapa leo kiseme kuna moja, mbili, tatu atokee mwengine aseme hivyo sivyo ni moja, mbili, tatu vipi itakuwa na thamani gani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hili lisiendelee tunachokisema ni kwamba sisi ni Wawakilishi wa wananchi, ambao wametutuma na tumekuja hapa kwa ajili ya kuwatumikia wao na sheria zinasema kwamba walio na mamlaka ni wananchi, kwa hiyo tusichezeane na hii haina maana. *(Makofi)*
Kwa kweli nasema hayo na wananchi wanatusikia, itakuwa leo huko tukipita mitaani mlifanya nini na serikali ndio inafanya nini na haitaki kutusikia na wala tusifike huko na mechi imalizike hapa. Kwa hiyo, tunasema hii ripoti haitufai na mimi sitaki isije. *(Makofi)*

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kidogo ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri umeshafika wakati Kamati za Baraza la Wawakilishi kwenda kuzomewa katika taasisi inazokwenda kuchunguza, kwa sababu kikao kilichopita tulikuja hapa kwa ajili ya kujadili hii ripoti ya Manispaa na tuliambiwa kwamba hivi sasa umefika wakati kuchagua Kamati Teule kwenda kuchukua uhakika wa vitendo ambavyo vinavyofanyika na vitendo vimekwenda kuchukuliwa na kuonekana, sasa baadae serikali inakuja kutuambia tujadili tena.

Kwa hivyo, hii kazi inakuwa kama labda hizi Kamati zinapokwenda kuchunguza zinakuja kusema uongo, sasa zinaposema uongo na serikali inakubali kwamba sisi tunasema uongo. Sasa kama tunasema uongo tukienda tena kule kwa ajili ya kuchunguza hayo mambo yanayofanyika hivyo kweli sisi tutathaminika au tutazomewa. Mhe. Mwenyekiti, tutazomewa na tutaonekana kwamba sisi tunasaliti wafanyakazi, ambao kweli wanafanya ubadhirifu ndani ya taifa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali kuhusiana na ripoti hii ichukue hatua kwa sababu tayari imeshakamilika na Kamati Teule imeshakwenda kuchunguza na kuhakikisha. Kwa hivyo, naiomba serikali iamue kwamba ripoti ya Kamati Teule ifanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimesimama hapa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Matemwe walionichagua kwa ajili ya kuja kuwafanyia kazi kwa yale mabaya yote ambayo tunayaona tuyaseme na mimi naunga mkono kwamba sitaikubali ripoti hii mpaka pale serikali itakapoamua. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwanza kabisa na mimi niseme kwamba siungi mkono ripoti hii hata kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii ni aibu, tena ni aibu kubwa sana, ni dhahiri kwamba serikali haijiamini. Pili niseme nini maana ya kuundwa Kamati Teule katika Baraza la Wawakilishi. Maana ya kuundwa Kamati Teule katika Baraza la Wawakilishi ni kufichua maovu ambayo yanatendeka katika nchi. Lakini leo serikali inaona bora ifiche maovu yanayotendeka katika nchi hii. Je, Mhe. Mwenyekiti, tujiulize hao wananchi waliotuleta hapa ili kuwatendea haki wao watatuona vipi sisi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba hii ni serikali au hii ni siri kali. Naomba nifikie hapo na miye nasema kwamba hoja hii siiungi mkono, siiungi mkono, siiungi mkono. Ahsante.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipa nafasi hii kuichangia ripoti hii ambayo imefikishwa mbele yetu ili tuijadili na tuitolee maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Kamati Teule napenda kujuilisha na ihakikishe kwamba inathaminika na inatekelezwa maagizo yake yote ambayo yamefikishwa mbele ya kutoa maamuzi. Wizara zote ambazo zimefanyiwa marekebisho ambazo zimekwenda Kamati Teule kuhakikisha na kujua ukweli wa shughuli zilizofanyika ambazo zina ubaya wake na kasoro zake. Mimi napenda kujuulisha kwanza Kamati Teule iheshimike maamuzi yake.

Kamati Teule inapokwenda huwa inatumia fedha nyingi za serikali na uwezo mwingi kwa kutumia mawazo na akili na busara huwa zinafanyika katika Kamati Teule. Hivyo Kamati Teule inapomaliza maamuzi serikali ni lazima ijue kwamba imepewa kitu chenye usahihi na ukweli ndani yake.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inapopewa maagizo na Kamati Teule na serikali inapotoa maamuzi yake ni lazima itoe maamuzi mazuri kwa kuchukua hatua yoyote inayostahiki ili Kamati Teule iridhike kwamba serikali imepokea taarifa hizo na zimeheshimika. Hasa kwa vile masuala yenyewe ni nyeti sana na ya upotevu wa fedha nyingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, basi serikali ingeliweza kuamua hata kwa kutoa shukurani kwamba Kamati Teule imefanya kazi au basi serikali ingetoa angalau onyo kwa wahusika. Kwani adhabu ni adhabu tu sio lazima kuhakikisha kwamba umemtesa mtu au umemuua mtu au angalau lingetolewa onyo la maandishi kwa wahusika iwapo kama watarudia tena. Ili Kamati Teule ione kwamba imetoa neno na serikali imelipokea lakini kwa mara ya kwanza imeweza kulipokea na kuweza kutoa onyo. Basi tungeliweza kusema kwamba serikali imethamini amri ile. Lakini suala la kwamba serikali haikupokea suala hilo na imesema kwamba hakuna kosa. Hilo halikubaliki.

Mimi ushauri wangu ni kwamba ripoti hii irudi tena serikalini na ipokelewe kwamba inakwenda kufanyiwa kazi serikalini na inaporudi ije na angalau neno onyo au imelithibitisha kwamba hili suala limepokewa na serikali kwamba linafanyiwa kazi kama linavyotakiwa na Kamati. Mimi sina pingamizi na suala hili, ila naomba lirudi tena na mimi sikulipokea angalau lirudi na onyo. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi angalau ya kuweza kutoa maoni yangu katika ufafanuzi wa serikali wa hoja mbali mbali zilizojitokeza katika ripoti ya Kamati Teule.

Mhe. Mwenyekiti, tunakumbuka mara nyingi baada ya Kamati zote hizi tulizonazo ambazo ni Kamati za Baraza zinapokwenda kufanya shughuli zake katika mawizara au sekta mbali mbali mara nyingi huwa zinatoa ripoti zake. Lakini Kamati ya *PAC* mara nyingi inakuwa ni moja kati ya Kamati ambazo ziko mbele katika kutoa mambo kadha wa kadhaa ambayo yanakuwa ni maovu makubwa ya utendaji wa kazi za serikali yanayotendeka.

Nakumbuka mara moja baada ya kuonekana maovu ambayo yanatendeka baadhi ya wizara na sekta mbali mbali tulitaka kuunda Kamati Teule hapa, lakini serikali ikaweka mkono haitaki kufanya kitu kile. Kwa mujibu wa Kanuni

tuna haki sisi ya kuteuwa Kamati Teule. Baraza lina wajibu wakati maovu yanatendeka katika Mawizara yetu basi Kamati Teule zinakuwa ni muhimu katika kufatilia majukumu yale.

Leo Mhe. Mwenyekiti, mbele yetu huu ni ufafanuzi wa serikali wa hoja mbali mbali ambazo zimetolewa na Kamati Teule, hazijatupa nguvu bado wala muelekeo kuona kwamba kweli serikali ina msimamo na kuona kwamba Kamati Teule zilizochaguliwa na Baraza zinapewa nguvu. Hapa mimi nafikiri kuna mambo mengi ambayo yanatendeka katika mawizara yetu. Kuna mambo ya ubadhirifu wa fedha, kuna harufu ya rushwa inatokezea, kuna mambo ya udanganyifu ya watendaji wetu.

Kwa nini serikali haikubali kuamini ripoti ya Kamati Teule. Ripoti ya Kamati Teule ni ripoti muhimu sana na ni wajibu wake serikali kuipokea hii ripoti na kuifanyia kazi. Tatizo hapa ni kuifanyia kazi kwa sababu tayari ripoti imeshatoka na ukweli. Kwa sababu katika ripoti ya Kamati Teule ni mambo ambayo yanazungumzwa bayana baina ya Kamati na wale ambao yametokezea matatizo katika sekta zao. Kwa hivyo ni mahojiyano na ushahidi ambao unaotolewa na wakakubali kwamba sisi hili tumefanya kosa. Sasa wakati Kamati teule inatoa ripoti basi serikali iamini ile ripoti ya Kamati Teule na iende ikatekeleze. Tatizo hapa ni kutekeleza. Serikali haitaki kutekeleza ripoti ya Kamati Teule. Hivyo hatutoweza kwenda.

Mimi nafikiri kama serikali itafanya hivi itakuwa sasa tunaivunja nguvu hii Kamati Teule tunayoichagua na tumeichagua kwa pamoja katika Baraza kwamba iende ikachunguze na ilete taarifa katika Baraza na halafu tuikabidhi ripoti ile serikali na serikali iichukulie hatua. Lakini serikali inaonekana hapa labda itakuwa ni mambo ya muhali. Kwamba inaona serikali ikichukua hatua labda wao watalaumiwa. Lakini sasa tutafanya vipi na hii ni hali halisi ambayo Kamati Teule imeona.

Yale ambayo Kamati Teule imeona ndio pale serikali ichukue hatua ili kukomesha maovu yale yanayotendeka. Lakini serikali inaogopa sasa hivi kuwachukulia hatua za kinidhamu wale wote waliofanya mambo mabaya, kama ni wizi wa fedha au uharibifu wa fedha au kuna jambo fulani katika mradi fulani, fedha zimeliwa mradi haukuonekana. Kwa nini serikali iwe na kigugumizi katika kuchukua hatua.

Mimi nafikiri ili kuipa nguvu Kamati Teule ni wajibu wa serikali kuipongeza kwanza Kamati Teule kwa kazi waliyoifanya. Pamoja na kuona kwamba gharama kubwa ya fedha imetumika katika kuendesha suala lile, ni fedha nyingi tu na muda ambao uliopotea. Badala ya kuwa Kamati kwenda kufanya kazi nyengine imebidi wakaishughulikie kazi ile mara mbili tena. Mara ya kwanza ilifanywa na mara ya pili imefanywa na serikali imekwenda kulifanya lile lile ambalo serikali imepita kwa njia nyengine ili kama kuwanusuru na wasionekane kwamba watu wale hawana hatia.

Mimi nafikiri ni juu ya serikali kuipa nguvu hii Kamati Teule kwa yote ambayo Kamati Teule waliyaona na serikali ichukue hatua. Kama hatukufanya hivi Mhe. Mwenyekiti, tukachukua hatua kwa yale ambayo yaliyoonekana na tukaachilia basi, naamini yale ambayo yalikuwa yakifanywa yataongezeka kiasi mara mbili au mara tatu zaidi. Watu wataona kumbe hata Kamati Teule ikija hapa hata hatua watakazochukua lakini halafu serikali inawafunika funika watu wanaendelea na shughuli zao.

Mimi nafikiri ili kuondosha hapa tumeweka Mswada wa Rushwa tayari umeshakwenda serikalini na unataka kufanyiwa kazi, utafanyiwa kazi vipi na tunaoneana muhali, basi rushwa itaendelea. Mimi nafikiri Mheshimiwa huu ufafanuzi wa kiserikali ambao tulionao mbele yetu, namuomba Mhe. Waziri hili suala akalifanyie kazi tena ili angalau sisi Baraza turidhike. Ikiwa serikali haikuweza kuchukua hatua juu ya haya, tayari sisi tunaanza kuvunjika moyo. Ina maana sisi Kamati Teule au Baraza zima linakwenda kinyumenyume na serikali, serikali inasema hivi Baraza linasema hivi. Amri ya Baraza ni kubwa vilevile inataka lile linaloamuliwa ndani ya Baraza basi ni wajibu wa serikali kwenda kulitekeleza. Mimi naomba na nasema kwamba hii ripoti hatuwezi tukaipokea, tunairudisha kule kule ikafanyiwe kazi tena na tuone hatua gani serikali imechukua.

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Farida Amour Moh'd: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumza machache katika suala liliopo juu ya meza. Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti hii tuliyoletewa hapa ina mambo matatu muhimu, kuna maelezo ya tuhuma, kuna mapendekezo ya Kamati Teule na kuna maelezo ya serikali. Miongoni mwa

mapendekezo ya Kamati Teule na maelezo ya serikali hakuna hata moja angalau lililofanana katika utekelezaji wake.

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti hili ni jambo la kusikitisha mno. Nakumbuka hapa Kamati Teule hii ni ya mwanzo kwa kuikumbuka miye hapa iliyochukua miezi mitatu. Pesa nyingi za serikali za wavuja jasho zimetumika katika kufanya kazi katika Kamati Teule, muda mwingi ulipotea katika kutumia Kamati Teule ile kwa kufuatilia sekta hadi sekta, mtu hadi mtu kwa ushahidi uliokamilika na ikaletwa hapa. Leo majibu yake yali vyokuja Mhe. Mwenyekiti, hayajaturidhisha na inakuwa hatujawatendea haki wananchi wetu katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, wewe mwenyewe utakumbuka kuna Kamati Teule nyingi ziko juu ya meza yako, kuna Kamati Teule ya Manispaa, kuna Kamati Teule ya Shirika la Umeme ambayo tumeifanyia kazi zaidi ya miezi mitatu, kuna Kamati Teule nyengine ya Ardhi, kamati ambazo zote hizo kuna mambo, kuna madudu, kuna balaa za kila aina ndani ya Kamati hizo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kitu kimoja kama mfumo wa utekelezaji wa Kamati Teule za Baraza la Wawakilishi majibu yake ni haya basi naomba leo hii hapa, Kamati Teule zote zilizoundwa tutafute sekta moja muhimu ikiwa ni afya ikiwa ni ya kilimo wajumbe wale wa Kamati Teule tushirikiane tukafanye kazi kama ni ya kulima, kama ni ya kusafisha hospitali, lakini tusipoteze pesa za umma katika hali kama hii.

Kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, nasema miye ripoti hii siipokei na sitoipokea. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kunipa fursa hii kuchangia kwa mchango mdogo. Ningeiomba serikali kwa vile kosa limeonekana basi serikali ichukue hatua ambayo wananchi wote wako pamoja nayo na kwa vile mapungufu yameonekana basi isione muhali kwa watu wale kwa kuweza kuwajibika. Hapa yupo kiongozi wetu ambae alijiona kwamba kafanya makosa na aliwajibika. Sasa na hawa wakati tumeshawaona wana makosa basi tuwawajibishe ili wananchi wetu watuone kwamba tunawafanyia haki.

Kwa hilo mimi siungi mkono.

Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira): Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuchangia kidogo kuhusu Kamati hii Teule juu ya ufafanuzi wa serikali kuhusu hoja mbali mbali ambazo zimejitokeza katika ripoti hii ya Kamati teule.

Mhe. Mwenyekiti, Waswahili wanasema adui usimuangalie usoni na mimi nasema serikali isiwaangalie usoni wale wabadhirifu wa mali za serikali au mali za wananchi. Nadhani hakuna mjadala mkubwa ni kwamba ripoti hii haikubaliki na mimi nasema kwamba ripoti hii irudi tena ili serikali itupe maelezo zaidi. Hapa katika ripoti yake kuna kipengele kimeeleza maelezo ya ziada, nadhani watuletee maelezo ya ziada kuhusu ripoti hii ya Kamati hii. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia kidogo. Mimi Mhe. Mwenyekiti, ninavyosema kwamba tuna serikali na serikali hasa inavyotakiwa na ndio ilivyo kwamba ni kufanya uadilifu katika shughuli zake. Lakini kwa bahati mbaya au kwa bahati nzuri kiutaratibu huwa wanachaguliwa watu katika taasisi mbali mbali za serikali na kufanya kazi.

Wakati mwengine hutokea matatizo kiasi ambacho ikabidi kufanywe uchunguzi ndio hizi Kamati zetu Teule tunazozifanya. Sasa tujue kwamba Kamati Teule haitokei tu kimazingira lakini hata Mhe. Spika, hutumia umakini wake wa hali ya juu kabisa kuona kuwa chombo hiki kinatoa watu watakaoifanya kazi ambayo ripoti yake itakuwa ni yenye maslahi kwa serikali ina maana ni yenye maslahi kwa wananchi wote.

Mhe. Mwenyekiti, ndio ukaona kuna wengine walikuja hapa tokea 1995 mpaka leo hawajateuliwa kuingia katika Kamati yoyote teule kwa sababu wanaonekana pamoja na uwezo wao lakini kwa mahitaji yalivyo hutafutwa wale waliokuwa wanawashinda wenyewe katika vigezo ili ipatikane ripoti iliyokuwa ni muhimu sana.
Ripoti hii maana yake si kuchunguliwa na kuchakachuliwa tena halafu na kuletwa taarifa katika hali hii ilivyo. Maana huku kuna maelezo, kuna mapendekezo na kuna maelezo ya serikali. Mpango huu ni kama labda serikali ilikaa ikaichunguza ile ripoti halafu ikaona ifanye vyake kama kulingana nguvu. Kwa vile hizi ni taasisi mbili

tofauti, kuna serikali na kuna Baraza la Wawakilishi iliyotoa Tume. Naamini kwamba Baraza litatoa Tume ambayo itaridhika kutokana na ile adhma ya kuleta maendeleo katika nchi hii.

Kwa hivyo ili ipatikane *transparency* katika utekelezaji wa shughuli zetu ni kuona kuwa hii Kamati Teule ripoti yake imepewa uzito unaostahiki kwa mule ambamo kuna matatizo kunataka marekebisho serikali iridhie kufanya marekebisho na kwa maana hiyo ndiyo malengo hasa yaliyokusudiwa ya utendaji mzuri wa serikali unapatikana, vyenginevyo kama tume itateuliwa kama hii nzito halafu tena kukawa na kutolewa malezo mengine kama kuwa haikufanya kazi kwa uangalifu, itakuwa lego halipatikani.

Ushauri wangu tuamini kuwa Tume ilifanya kazi nzuri sana na tuamini kuwa ilifanya kazi kwa kukusudia kuona kuwa inaleta mafanikio katika shughuli zake na kuona kuwa serikali inawajibika ipasavyo. Tusingelikwenda katika mtindo huu kwa kupimana na kuwekeana maelekezo mengine, tungelifuata ushauri wa Tume ulivyo na baada ya kuridhika kuchukua hatua ili ufanisi upatikane. Kwa maana hiyo basi ningeliomba hii ripoti pamoja na uzuri wake ulivyo serikali kuchua hatua ya kutoa maelekezo lakini serikali haikufanyiwa Tume ili itolewa maelezo ni kutekeleza hayo yanayoonekana yana kasoro katika hizo sehemu zilizokusudiwa. Kwa hivyo ni vyema tena kwa roho radhi na kwa nia safi ya kuijenga serikali yetu hii ripoti irudi tusiipokee hivi sasa ikafanyiwe kazi upya kwa utekelezaji mwa mle ambamo tume imeona kunahitaji utekelezaji. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia machache katika ufafanuzi huu wa serikali kwa hoja mbali mbali zilizojitokeza katika ripoti ya kamati teule.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi niseme hii ripoti siipokei na siipokei kwa sababu imetusikitisha sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna fanya kazi zetu kwa mujibu wa kuisimamia serikali lakini pia kuisaidia serikali katika mambo yake na taasisi zao ambazo wanaziongoza.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kutokana na ripoti hii inavyoletwa tunaonekana sasa hivi Wawakilishi hatuaminiki na kazi yetu ni kuja hapa na kusema uwongo. Hilo ndilo tunaloonekana tunakuja kulifanyia kazi hapa. Kumbe ni kinyume sisi tunavyofanya kazi zetu, kuwasaidia mawaziri wetu kwa shughuli mbali mbali zilizopo kwenye taasisi zao. Siku zote hapa wanakaa wakipiga kelele kuwa tusaidieni mapato ya serikali yanavuja, tuelekezeni, lakini kumbe ni kinyume, hata lile suala linapokuja kukaribia huwa wanao wanatufanya sie kuwa ni waongo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo la kusikitisha sana leo na huko mitaani itakuwa ni aibu. Watu wanavyoisikia ripoti hii inavyosomwa ya kuwa serikali inapingana na wajumbe wake ambao kuwa wanaongozwa na katiba ya nchi hii wanaonekana kuwa ni wanafiki kuanzia leo katika Baraza hili, basi ni kitu cha kutuogopesha sana ten asana.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na ripoti hii wachilia mbali hizo Kamati Teule, hata hizo Kamati za Baraza tunazokwenda kwenye mawizara tutaogopa kutoa maelekezo na ufafanuzi kwa ajili ya utendaji wa serikali hii. Tutakunja kucha zetu kama matatizo ni haya. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, siungi mkono ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wajumbe kwa kuwa ripoti hii imechangiwa na watu wengi sana, wachangiaji karibu 24 na muda uliobakia ni mdogo sana kwa Mhe. Waziri kuweza kufanya majumuisho. Naomba kuchukua fursa hii kukuombeni Waheshimiwa Wajumbe tumpe nafasi Mhe. Waziri aende akajitayarishe kwa sababu ya majibu sahihi ili jioni atakapofika hapa aje atusaidie kutujibia baadhi ya hoja ambazo wajumbe walikuwa wametoa katika michango yao mbali mbali.

Kwa msingi huo basi naomba kuchukua fursa hii kuliakhirisha Barara hili kwa muda huu hadi jioni saa 11:00 wakati ambapo Mhe. Waziri atakuja kufanya majumuisho kwa ripoti hii ambayo leo tumeisoma hapa. Asanteni sana.

(Saa 6:22 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa jioni hii kunipatia nafasi, Mhe. Mwenyekiti nami nimesema nichangie kidogo kuhusu masuala ambayo yameletwa mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sipingi hoja za Wajumbe ambazo zile kwa kweli ni mtu mwenyewe binafsi anavyohisi kama utekelezaji umefanyika au haukufanyika. Lakini ninachopenda kusema Mhe. Mwenyekiti ni kwamba ni vyema tukaelewa utaratibu na maudhui ya hoja ile ambayo ililetwa. Hoja ile ililetwa na baadae ikateuliwa Kamati Teule, na Kamati Teule ile ikaleta mapendekezo yake kwa Baraza.

Mhe. Mwenyekiti Baraza baada ya kujadili ndio likatoa…..

UTARATIBU

Mhe. Nassor Ali Salim: Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri azungumze sote tumsikie kwa sababu anazungumza sauti ya chini kabisa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema mwanzo ni kwamba baada ya Kamati Teule kuleta mapendekezo yake Barazani, Baraza likajadili na baadae mwisho Mhe. Waziri wa Nchi alisema kwamba na naomba ninukuu moja katika maelezo yake. "Mhe. Spika, baada ya kusema maelezo hayo naomba niseme kwamba serikali imepokea ripoti hii, nataka kuhakikishia kwamba kipengele baada ya kipengele kitafanyiwa kazi na baadae tutaliarifu Baraza la Wawakilishi.

Sasa utekelezaji wa serikali Mhe. Mwenyekiti uko katika kifungu cha tano cha Katiba kama alivyosema Mhe. Salmin, lakini Mhe. Salmin ninafikiri hakwenda mbele zaidi. Kifungu cha tano kina mambo matatu kwamba mamlaka ya nchi yanafanywa katika sehemu tatu. Kwanza utendaji, ambao ni *executive*, pili ni usimamizi wa sheria na tatu ni utekelezaji wa haki. Sasa usimamizi na utungaji wa sheria uko katika Baraza la Wawakilishi, na utendaji uko katika *executive* ambao ni Rais pamoja na serikali kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti ni vyema tukajua kwamba serikali yetu na Serikali nyingi za hapa Afrika wanaita ni *executive presidential government*. Hii ina maana kwamba Rais ndio mtendaji mkuu ni tofauti kidogo na *parliamentary government* ambayo Waziri Mkuu ambaye yumo katika Baraza ndie mwenye maamuzi ya mwisho katika utendaji wa serikali. Kwa hivyo hapo Baraza kwa sababu ya utaratibu huo, Baraza linapeleka maoni ambayo yametolewa mapendekezo kwa serikali na serikali inayatekeleza. Na katika kutekeleza lazima tujue Mhe. Mwenyekiti kwamba utaratibu wa utekelezaji wa suala lolote unakwenda kwa mujibu wa sheria zetu.

Na unapounda Tume hapa na ikafanya kazi tume ile inatoa mapendekezo mengi, na mapendekezo hayo yanaweza kwa mfano yakasema kwamba fulani tunahisi kwamba amefanya kosa na afukuzwe kazi. Lakini hapo si mwisho, hilo ni pendekezo na ujue kwamba sisi tumetawaliwa na sheria. Tuna sheria Mhe. Mwenyekiti sheria ya utumishi ambayo tulipitisha hivi karibuni, nambari 2 ya 2011. Kifungu cha pili Mhe. Mwenyekiti na kifungu cha tano cha sheria hizi zinathibitisha zaidi kwamba utumishi wote mtu yoyote ambaye yupo katika utumishi wa Zanzibar, basi lazima sheria hii imuandame yaani lazima shughuli zake zote ziende kwa mujibu wa sheria ya Utumishi namba 2 ya mwaka 2011.

Kwa hivyo unapofanya uamuzi lazima uzingatie, mambo yale huwezi tu kusema hapa kwamba fulani achukuliwe hatua halafu ukachukua hatua bila ya kuzingatia sheria ile. Na sheria ile wanasema wenyewe ina-*bind* ile *government* yaani serikali ina wajibu wa kutekeleza shughuli zake kwa mujibu wa sheria ile. Kwa hivyo mapendekezo yanayotoka hapa lazima yafanyiwe kazi kwa mujibu wa utaratibu, vyenginevyo yule mtumishi anayehusika anaweza akachukua hatua nyengine za kwenda mahkamani, kwa sababu ndivyo tulivyokubaliana na ndio sheria ilivyo. Kwa hivyo hilo Mhe. Mwenyekiti napenda sana Waheshimiwa Wajumbe walijue na ndio maana serikali baadhi ya mambo ikapendekeza kwamba haya yapelekwe mahkamani, au haya yafuate utaratibu ambao upo kisheria. Tungelifanya vyenginevyo vyovyote ina maana ni kwenda kinyume na sheria zetu ambazo Baraza la Wawakilishi imezitunga. Hiyo ni moja.

Lakini la pili kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mshimba alizungumzia habari ya mzee aliyenyang'anywa nyumba na nini utaratibu wote ule, Mhe. Mshimba hakutaka kuwa mkweli, na mimi nasikitika sana kusema hivyo. Kwa sababu suala lile mtakumbuka Mhe. Mwenyekiti lilikuja wakati wa bajeti likazungumzwa, mimi binafsi nikasema nitalichukua suala hilo Mhe. Mshimba akaja ofisini kwangu, alipokuja ofisini kwangu watu hao tukawaita wanaohusika wote, tulipowaita wakakaa huko, mwisho wakakubaliana na huyo mzee anayesema alipwe milioni ishirini walikuja ofisini kwamba akasema wameshasuluhishana hakuna tatizo tena. Na mimi nilimripotia Mhe. Mshimba.

Sasa mimi ninasikitika kwamba leo anabadilika kabisa kutokana na suala hili, kwa sababu watu wenyewe wameshakubaliana, wameshayatatua matatizo yao, sasa utachukua hatua gani? Ikiwa kuna hatua nyengine ambazo anahisi ameonewa, tumesema kwamba aende mahkamani lakini sisi tunahisi hakuonewa, kwa sababu wameshakubaliana wao wenyewe na kuja ofisini kwangu wakaniambia. Na Mhe. Mshimba nikamwambia sasa sioni sababu kwa nini anasema hakubaliani na suala hili ambalo yeye mwenyewe anajua. Mimi nilimwambia.

Mhe. Mwenyekiti zaidi ni kusema kuwa tunapoendesha shughuli hizi lazima pia tujue kwamba kwa utaratibu wetu Rais ambaye na yeye kachaguliwa na watu zaidi kuliko Mwakilishi, kwa sababu Rais jimbo lake ni nchi nzima, na kwa mujibu wa Katiba ndie mwenye uwezo wa mwisho. Sasa hapa tunachofanya ni kwamba suala hili linazungumzwa hapa na linapendekezwa na serikali inachukua hatua. Kuna mambo naamini kwamba yamechukuliwa hatua, lakini pengine Wawakilishi watakuwa pengine hawakuridhika na hatua zilizochukuliwa na huo ni ubinaadamu huo hakuna matatizo wala mimi sipingi kwamba mtu hakuridhika na hatua iliyochukuliwa, lakini ni vyema tukajua kwamba utaratibu wa uendeshaji wa nchi ni hivyo.

Baraza la Wawakilishi linapokuwa na Kamati na linapotoa maelekezo yake linapeleka mapendekezo yale kwa Serikali ili yafanyiwe kazi. Sasa ufanyaji kazi huo unategemea huwezi tu kwa mfano kuna suala la jenereta. Jenereta kwa mujibu wa ripoti linasema kwamba jenereta zile moja haikuonekana, moja ika-*suspect* ile ripoti kwamba imeibiwa. Lakini serikali baada ya kufanyia kazi ikasema si kweli, jenereta hilo lipo ni namba zilibadilishwa mpaka hivi sasa ipo pahala ipo. Kwa hivyo suala la kuibiwa jenerata halipo. Kwa hivyo tungeliichukua ile ripoti tu bila ya kuifanyia kazi tukasema yule aliyehusika na jenereta afukuzwe tungelimdhulumu bure. Kwa hivyo utaratibu ni huo wa kufanya kazi, na hivyo ndivyo serikali ilivyofanya kazi.

Sasa kama kuna mambo ambayo pengine Wawakilishi hawakuridhika kidogo na hiyo ni ubinaadam ni sawasawa. Lakini utaratibu wa kufanya kazi na utaratibu wa ripoti katika Baraza la Wawakilishi hivyo ndivyo ulivyo, kwamba ripoti inajadiliwa, inakubaliwa Baraza linapendekeza kwa serikali kwamba sisi tunahisi kuna haya na haya na haya serikali inachunguza. Kuna mambo mengine ambayo huwezi kuyaamua bila ya kwenda mahkamani. Kuna mambo mengine huwezi kuyaamua bila ya kufanya uchunguzi mwengine. Kuna mambo mengine huwezi kuamua bila ya kupitia katika sheria ya utumishi. Sasa lazima serikali kwa sababu wao ndio watendaji wa shughuli hizo kwa mujibu wa sheria zetu lazima ichukue taratibu zote hizo ili utekelezaji wenyewe uwe ni wa haki na wa sheria, na hiyo ndiyo ilivyofanywa.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusema hayo, mimi nasema utaratibu ni kwamba huo ndivyo ulivyofanywa, Mwakilishi binafsi anaweze akawa hakuridhika na maamuzi ni ubinaadamu huo na ni haki yake, lakini kwa kweli serikali imetekeleza wajibu wake kwa kupitia utaratibu kama huo na kuhakikisha kwamba yale mambo ambayo yanatakiwa yapelekwe mahkamani au yale mambo ambayo yanatakiwa yafanyiwe kazi kwa mujibu wa sheria yetu ya utumishi ambayo tumeipitisha sisi wenyewe yamezingatia utaratibu huo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitangulie kukushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia katika hoja hii ya taarifa ya serikali kuhusiana na utekelezaji wa ripoti ya Kamati Teule. Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti naomba kwa dhati kabisa kwa sababu sijapata fursa kuzungumzia kuhusiana na hii ripoti niipongeze sana Kamati Teule na naipongeza kwa dhati kwa sababu pamoja na yaliyozungumzwa katika utekelezaji lakini mimi ninaamini na ninaomba niwatanabahishe wenzangu kwamba katika usimamizi wa sheria, basi ile kwamba sheria imesimamiwa imetekelezwa ni jambo moja kubwa sana. Na nani katiwa hatiani ni hatua nyengine ambayo inawezekana kwamba kuna wengi uliowatuhumu, lakini suala la kumtia hatiani unayemtuhumu ni suala jengine. Lakini kwamba umeisimamia na umesimamia kwamba ukataka itekelezwe, mimi naamini kwamba inawakumbusha wengi kuwa nchi yetu inaendeshwa na sheria na taratibu na ni lazima zizingatiwe.

Kwa hivyo sehemu kubwa ya ripoti ya Kamati Teule imetukumbusha umuhimu wa kufuata taratibu. Na mimi nasema kwa dhati kabisa kwamba hii imesaidia sana inawezekana kila mtu na maoni yake anahisi kwamba ili isaidie labda ilikuwa lifanyike hili au matokeo yawe haya. Lakini mimi nasema binafsi yangu ninajihisi kama nimeishi katika Zanzibar mbili. Maana yake Zanzibar ya kwanza ni Zanzibar ile ambayo ulikuwa unalaumiwa kwa nini unataka kumuajiri mtu kwa kumfanyia usaili, kwa kuhoji vigezo, kwa kuhoji uwezo wake, ulikuwa unalaumiwa hiyo nimeishi Zanzibar hiyo.

Lakini baada ya ripoti ya Kamati Teule imenifanya niishi katika Zanzibar ambayo mtu analaumiwa kwa kumuajiri mtu, kwa mfano kwa kufuata vigezo na taratibu zinazotakiwa. Sasa mimi nasema kwamba hili ni jambo ambalo Kamati Teule imesaidia sana na Baraza hili kwa kweli linastahiki pongezi kwa dhati kabisa kwa kuunda Kamati Teule kwa sababu matokeo yoyote yale ambayo yametokea, lakini ninaamini utendaji hautokuwa sawasawa na kabla ya ripoti ya Kamati Teule. Hiyo ndiyo imani yangu na kwa kweli nishukuru sana nilipongeze sana Baraza kwa kuunda Kamati Teule hii na kazi ambayo Kamati Teule ilifanya.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye hili la ripoti nimesikia masikitiko au maoni ya Wajumbe kuhusiana na utekelezaji. Lakini mimi katika kujadili hili mara nyingi napenda nianze na maneno ya kiungwana kabisa ambayo alisema Mwenyekiti wa Kamati Teule wakati anawasilisha ripoti, alimalizia kwa kusema jamani tumefanya kazi hii kwa kadri ya uwezo wetu na kwa kadri ya uadilifu wetu, lakini sisi ni binaadamu na kama binaadamu basi inawezekana kuna mengine tumekosea. Hayo ni maneno mimi nasema ya kiungwana kabisa ambayo ameyasema au alimalizia Mhe. Omar Ali Shehe wakati anawasilisha ripoti ya Kamati Teule.

Sasa katika hatua za utekelezaji ambao serikali leo imewasilisha ripoti yake, mimi naomba niseme Mhe. Mwenyekiti kwamba hapa tunajenga misingi ya utendaji wa kazi wa vyombo vyetu wa Baraza letu, misingi ya utekelezaji wa kazi, wa serikali, misingi ya utekelezaji wa kazi wa taasisi nyengine ya kusimamia sheria ya mahkama. Kwa maana hiyo, hiyo ndio inaunda nchi yetu sasa ni lazima tujenge misingi ambayo itakubalika na itatuwezesha kwamba haya ndio majukumu ya chombo hiki, na haya ndio majukumu ya chombo hiki. Na moja ni hili katika utekelezaji wa yale ambayo Kamati Teule ilikuwa imependekeza.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ameeleza vizuri na mimi ninakubaliana naye kwamba ni vizuri kwa sababu tutakapojenga msingi huo ndio tutajenga msingi wa nchi yetu kuiendesha kwa utaratibu. Mhe. Mwenyekiti huwezi kujua raha ya utaratibu mpaka siku itakayotokea yamekufika wewe ndio muathirika. Pale inapotokea wewe kwa mfano umetuhumiwa basi pale ndio unapojua raha ya utaratibu, lakini ukituhumu wewe siku zote utaratibu ni udhia. Lakini ukituhumiwa wewe pale ndio unapokuja kujua kwamba utaratibu ni jambo muhimu. Na Mhe. Mwenyekiti hakuna mtu hapa ambaye yuko *immune* na kutuhumiwa, unaweza ukatuhumiwa la kweli, unaweza ukatuhumiwa jengine kwa sababu yoyote ile. Lakini suala la kutuhumiwa hakuna mtu ambaye atasema mimi siwezi kutokea nikatuhumiwa.

Sasa ukituhumiwa utaratibu ndio unapaswa ukulinde na hapo ndipo utapojua kwamba aha ule utaratibu kumbe uliosemwa siku zile kumbe faida yake ni hii. Lakini leo unatuhumu kweli utaratibu ni udhia, tena udhia kweli kweli, kwa hivyo mimi naomba kulikumbusha hili kwamba leo mtuhumu kesho anaweza akawa mtuhumiwa. Kwa hivyo ni vizuri tukajenga misingi na utaratibu maana tutakachokiamua leo tunajenga *precedent* ya kesho, tunajenga utaratibu wa kesho. Na mmoja katika msingi mkubwa wa kutuhumu katika haki Mhe. Mwenyekiti msingi mkubwa wa haki nao pia ni mgawanyo wa madaraka. Na mgawanyo huu wa madaraka unasema katika kutoa haki kwamba anayetuhumu hahukumu ndio msingi wa haki na ndio msingi wa kusimamia haki. Huwezi ukatuhumu halafu ukataka na wewe ndio uhukumu, hapo hapatakuwa na haki. Wewe tuhumu, lete tuhuma zako, lete ushahidi wako na hata mapendekezo, maana yake hata ukiandika hati ya mashtaka mahkamani unasema naomba mahkama iamue hili na hili na hili.

Sasa mimi siamini kwamba Waheshimiwa Wajumbe wanaamini au wanataka tujenge msingi wa kwamba Kamati Teule msingi wake ni tuhuma, na kanuni zetu zinasema kwamba yule aliyetuhumu awemo katika uchunguzi. Sasa siamini kwamba Wajumbe wanataka tujenge msingi wa kwamba baada ya tuhuma zile basi ule uamuzi uende ukatekelezwe moja kwa moja. Siamini kwamba tunataka kujenga msingi huo kwamba, tuhuma zimetolewa, zimechunguzwa, ushahidi upo basi unayempa ya kwenda kutekeleza basi na yeye asijiulize katika kutekeleza hili nifuate sheria gani? Katika kutekeleza hili nifuate utaratibu gani, siamini kama tunataka akatekeleze, akatekeleze lolote. Maana yapo mambo ambayo hata tumeruhusiwa maana kuchinja kwa mfano ni jambo limeruhusiwa, lakini hata kuchinja kwenyewe yule kuku basi pia kuna sheria zake. Huwezi kuchukua kigae ukachinjia kuku utakuwa wewe mwenyewe sasa unapata dhambi kwa jambo la halali.

Sasa katika hizi tuhuma kuna sheria nyingi katika kuzitekeleza zinazotakiwa zifuatwe, sasa huyu unayempa kutekeleza ni wajibu wake ajiulize katika kutekeleza haya je, ninapaswa nifuate utaratibu gani au nimeambiwa nimuwajibishe au nimfukuze basi nimfukuze bila ya kufuata utaratibu. Na katika kuchukua hatua zenyewe za kinidhamu wakati mwingine katika sheria yenyewe inasema kwamba aa aliyefanya kosa hili umpe adhabu hii,

aliyefanya kosa hili umpe adhabu hii. Sasa ni hayo ambayo wewe mtekelezaji unatakiwa na wewe utumie akili zako, utumie maarifa yako katika kuyatekeleza yale ambayo tuhuma zile zimekuja na kutoa ushahidi kwamba kuna tuhuma za namna hii.

Na hili mimi naomba niwakumbushe sana Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Mwenyekiti kwamba turudi kwa mfano kwenye mahkama. Mfano mzuri sana mahkama inatufunza jinsi ya kutekeleza maamuzi. Mhe. Mwenyekiti mahkama ndio inayosikiliza kesi kwa mfano na ndio inayotoa hukumu, lakini utaratibu wa kimahkama Mhe. Mwenyekiti mahkama inatoa hukumu lakini ikishatoa hukumu watu hawatoki kwa mfano wakaenda wakasema kwamba nyumba ivunjwe, kuna kitu kinaitwa kukaza hukumu ni hatua ya pili.

Katika kukaza hukumu unachojiuliza kwamba je hili ninalotaka kulitekeleza linatekelezeka? Na katika hatua ya kukaza hukumu unaweza kukuta hiyo nyumba uliyotoa amri ivunjwe au iende kwa mtu mwengine atatokea mtu mwengine ambaye hakuwemo kwenye kesi anasema aaa hii nyumba sio ya huyo mliomfikiria ni yake. Hii nyumba ya kwangu kwa hivyo haiwezi kutolewa ikauzwa kwa sababu ya kufidia deni la huyo mtu mnaesema. Hayo yanatokea na hilo ni jambo la kawaida na hii ndio faida ya kusema kwamba unapotoa hukumu unapotaka kutekeleza, kwa mfano hata kesi ya mahkama hiyo hiyo ndio inayotoa hukumu. Lakini inapotekeleza kuna mara nyingi inasema aa kumbe hii hukumu yenyewe haitekelezeki, kumbe kuna jambo hili na hili ambalo tulipaswa kulizingatia.

Sasa nasema Kamati Teule imefanya kazi yake, imezingatia ushahidi wake iliyouona ni sawa, imetoa mapendekezo yake, lakini hivyo ndio tunajenga msingi hapa kwamba basi yaliyotolewa yaende yakatekelezwe bila serikali kuzingatia sheria, bila kuzingatia taratibu. Mimi siamini kwamba huo ndio msingi ambao tunataka na ndio kilichofanyika katika jambo hili kwamba serikali imezingatia yaliyoelezwa, yanayotekelezeka, yametekelezwa na yamo mengi. Ninasikitika Waheshimiwa Wajumbe hawakuweza kuyaona kwamba lipi na lipi limetekelezwa mengine 100%. Mengine wala hayakupendekezwa lakini serikali imeona bora iyatekeleze vile vile na yamo yameelezwa katika ripoti hii.

Lakini la pili mimi naomba Mhe. Mwenyekiti niwakumbushe pia Waheshimiwa Wajumbe iliundwa Tume ya Kuchunguza ajali ya MV Spice Islander. Tume ile iliongozwa na Jaji wa Mahkama Kuu, Katibu wake ni mwanasheria tena ni muendesha mashtaka na miongoni mwa wajumbe wake mlikuwa na wanasheria vile vile. Imekuja imetoa mapendekezo yake lakini bado kwa utaratibu ule ule kwamba yale mapendekezo yaliyotolewa yamo yaliyotekelezwa 100% mengine yakasemwa aa hebu tuyapeleke kwa vyombo vinavyohusika. Maana Tume kwa mfano ilipendekeza kwamba haya hawa wachukuliwe hatua za kisheria. Ukisema hatua za kisheria maana yake ni nini? Ukisema hatua za kisheria maana yake ni kwamba ni kesi ya jinai, kesi ya jinai inaanzia kwa Polisi kufanyiwa upepelezi. Kamati ya ile ripoti inakuwa inasaidia tu lakini inabidi na wao wafanyiwe upelelezi wao, muendesha mashtaka na yeye aende akaamue kwamba aa ushahidi huu unatosha kufungua mashtaka kwa kosa hili.

Maana unapofanya uchunguzi mara nyingi lile jambo ambalo linahitajika kwa ajili ya kufungua mashtaka unakua hulioni mpaka anayetaka kufunga mashtaka ndio atakuja kukwambia aa hapa kuna mapungufu haya, ili tufungue mashtaka inabidi tulipate hili, tulipate hili, tulipate hili. Na kama hamjaelewana mchunguzi na muendesha mashtaka siku zote mtagombana. Mhe. Mwenyekiti nimefanya kazi hiyo miaka 9 nimeona ugomvi tunaokuwa nao mara nyingi baina ya mchunguzi na mfungua mashtaka. Lakini mnafika pahala mnaelewana mnakubaliana kwamba kweli hapa pana mapungufu lakini tukayatafute tukayafanyie kazi.

Sasa Tume ile iliongozwa na Jaji wa Mahkama Kuu, lakini aliposema mapendekezo yake mengine hakusema tu moja kwa moja mtu anampa adhabu kwa sababu yeye ni Jaji wa Mahkama Kuu. Utaratibu umefuatwa na matokeo ya wengine waliopendekezwa washtakiwe. Muendesha mashtaka kasema aa ushahidi kwa hili haupo wa kutosha wa kufungua mashtaka. Sasa pengine tungeweza kulalamika kama ni sisi kwamba itakuwaje Jaji aone yeye kwamba kuna ushahidi muendesha mashtaka asione, ndio ilivyo ndio utaratibu wake, kila mtu ana kazi yake na kila mtu anapofanya kazi fulani unakuwa na vigezo vyako na anaefanya kazi nyengine anakuwa na vigezo vyake.

Kwa hivyo, mimi sijaona katika hili kuna lililopunguzwa, sijaona katika ripoti hii kama kuna jambao ambalo halikufanyiwa kazi au kuna jambo ambalo serikali imelipuuza na kusema serikali kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais sio yeye aliyesoma hii ni serikali yote nzima, Rais mwenyewe, Makamu wa Kwanza, Makamu wa Pili wote jambo hili wamelipitia na wakaona kwamba katika hili basi hili lazima litekelezwe, hili utaratibu wake ufuatwe hivi na hili tunaona jamani hata kama tunachukia vipi.

Kwa sababu kuna mambo mengine unaweza ukamtuhumu mtu lakini tuhuma hata zikiwa kubwa namna gani haina maana kwamba ni ushahidi wa kumtia mtu hatiani, inawezekana unalichukia sana kama katika Dini yetu ya Kiislamu Mhe. Mwenyekiti, inavyochukia zinaa, lakini imeweka utaratibu kwamba ili mtu atiwe hatiani kwa kosa lile basi lazima aonekane na tena sio tu aonekane, imekwenda mbali zaidi wapo mashekhe wanasema na mashahidi wanne, hao mashahidi wanne sio waone kama tunavyoona kwenye sheria hizi za Kiingereza, maana sheria za Kiingereza wanasema kwamba uwaone *in flagranted delicto* ndivyo wanavyosema, yaani uwaone katika mazingira ambayo utasema hawa bwana lazima limepita jambo, lakini Sheria ya Kiisilamu inasema uwaone *Dakhala Kharaja*, umuone mtu anaingia akitoka watu wanne.

Swali hivi wakiwaona watu wawili hivi ndio hapajafanyika jambo? Lakini ndio utaratibu uliowekwa na sheria kwamba inawezekana lile jambo kweli limefanyika lakini ili umtie hatiani lazima hili na hili litimie. Sasa leo unasema mtu akimili hisa katika Kampuni kamapuni ndio imefanya makosa basi ya yeye ameshaingia hatiani. Jamani wapo wanasheria watasema kwamba kwanza ukiwa na hisa kama kampuni inafanya kosa mwenye kosa si mwenye hisa na *Director*, mana kampuni ina *level* ya wenye hisa ina na *level* ya *Directors,* sasa *Director* ndiye mwenye kosa.

Lakini la pili kama tunasema yeye mwenye hisa lakini katumia nafasi yake basi tuieleze kwamba kuna siku alikwenda kwa huyu alichukua hatua hii, alifanya hiki, sasa yanapokuwa hayapo tunapotaka tutumie kosa lake la kuwa na hisa ndio keshafanya kosa mimi nadhani ni mambo ambayo ni vyema tutafakari na ninasema naomba nirudie tena Mhe. Mwenyekiti, raha ya utaratibu ni siku unayotuhumiwa. Kwa sababu ukituhumiwa ulinzi wako ni ule utaratibu na sisi sote mimi niliwahi kuwaambia wenzangu tuseme sote jamani kila mtu ana mapungufu yake, leo mtu ukiacha hili ikija Kamati Teule nyengine itawapata wengine, na Kamati Teule nyengine itawapata wengine, tukubali kwamba tunakotoka taratibu uzingatiaji wake haukuwa mkubwa na hii kamati ndio maana nasema ripoti hii baada ya ripoti hii mimi nasema usimamizi wa shughuli za serikali ni tofauti utakavyokuwa tunauona sisi tuliomo na huko tunakotoka na hii ndio faida ya kitu kama hichi.

Sasa kama tutasema kwamba tufanye hivi basi tutafika pahala sote tutaumia maana yake kwa mazingira yetu nilikuwa nawaambia wenzangu hapa kwamba aah, unajua Waswahili wanasema kwamba, “unachagua chua kwenye mchele sio kwenye mpunga”. Kwa sababu ukichagua chua kwenye mpunga utaumwaga wote. Sasa na sisi kwa jinsi tulivyokuwa tumejisahau katika utaratibu yako mengi ambayo yamefanyika na Kamati Teule moja kubwa ambayo imefanya ni kutukumbusha turudi katika utaratibu serikali inaendeshwa kwa kufuata sheria na utaratibu. Hili ni jambo kubwa sana kama Waheshimiwa hatulioni mimi naomba tulione tufumbue macho kwamba katika hili kwa kweli Baraza hili limefanya kazi kubwa sana ya kutanabahisha, ya kukumbusha na ya kutoa mfano hai kwamba katika hili na hili hatukufuata taratibu.

Sasa mimi nadhani ingekuwa jambo la busara kama tungeweza kusema jamani hili kweli mmelifanya tukubali pale serikali ilipofanya, lakini jamani serikali kwenye hili hamjalifanya. Mimi nadhani hivyo ndio busara nzuri ya kuendesha nchi yetu, kwamba pale tulipofanya tuseme kwamba jamani tumefanya japo hatukuridhika lakini hili mmelifanya au mnaonaje mngefanya hivi. Lakini jengine hili jamani hamjalitekeleza mkatwambia na serikali italitekeleza kama msingi ndio kama huu nilioeleza sheria zipo za kutekeleza, utaratibu upo wa kutekeleza sidhani kwenye hili kwamba serikali ilikusudia kumlinda mtu yeyote. Kwa sababu kwa kutekeleza haya serikali yenyewe inapunguza kazi ya kuleta ufanisi, sasa sidhani kwamba serikali itafumba masikio kusema kwamba kuna hili tunahisi halikutekelezwa basi tulitekeleze, lakini kusema kwamba serikali haikutekeleza mimi nadhani sikuitendea haki serikali, sidhani kama ni kuitendea haki hata nchi yetu.

Kwa sababu vyombo hivi lazima vifanye kazi kwa pamoja na vyombo hivi vikishikana mimi naamini maovu yote ambayo tunayaona kuwa yametendeka basi serikali itaweza kuyasimamia na kuweza kuyapatia ufumbuzi. Lakini tukiwapa *impression* watu kwamba serikali haiku *serious* haitaki haya yaondoke mimi nadhani itakuwa hatuitendei haki serikali yenyewe na hatuwatendei haki wananchi kwa sababu wameiamini serikali yao kama walivyowaamini Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachohisi ni wakati tufanye kazi kwa pamoja kama kuna kasoro tuelezane ile kasoro lakini tusiwape watu mawazo kwamba serikali haikutaka kufanya au haikufanya kitu, yapo mengi ripoti imeeleza kwa uwazi yaliyoelezwa na yapo mengine ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kwamba huo ndio msingi wa kwenda, tuseme moja moja hili limetekelezwa, hatukuridhika au tumeridhika lakini limetekelezwa tukubali ukweli. Hili halikutekelezwa twambieni tutatekeleza nadhani hiyo ndio njia ambayo itatusaidia katika kutekeleza jambo hili na katika kuendeleza nchi yetu. Kwa sababu yaliyoelezwa humu ni ya msingi na ni wajibu na ni hamu ya serikali kuona kwamba yametekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kwa mara nyengine kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia kutuwezesha tena jioni hii kukutana hapa tukiwa wazima tukiendelea kufanya shughuli zetu vizuri. Aidha nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili nami niweze kueleza machache.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa michango yao na kutokana na michango ambayo wameitoa mbele ya Baraza lako Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza uniruhusu niwatambue.

1. Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Mambo mbali mbali).
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Hija Hassan Hija
4. Mhe. Salmin Awadh Salmin
5. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
6. Mhe. Subeit Khamis Faki
7. Mhe. Saleh Nassor Juma
8. Mhe. Ali Salum Haji
9. Mhe. Rufai Said Rufai
10. Mhe. Ussi Jecha Simai
11. Mhe. Hamza Hassan Juma
12. Mhe. Ashura Sharif Ali
13. Mhe. Hassan Hamad Omar
14. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
15. Mhe. Mohammed Haji Khalid
16. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
17. Mhe. Abdi Mosi Kombo
18. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
19. Mhe. Mussa Ali Hassan
20. Mhe. Hemed Suleiman Khamis
21. Mhe. Farida Amour Mohamed
22. Mhe. Asha Abdu Haji
23. Mhe. Nassor Salim Ali
24. Mhe. Salim Abdalla Hamad
25. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
26. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na
27. Mhe. Mwanasheria Mkuu

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nataka niwashukuru sana Waheshimiwa wote lakini shukurani maalum ziende kwa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Mwanasheria Mkuu kwa kueleza kwa undani kabisa hoja za Kamati Teule.

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe sote tunaamini kabisa kwamba tume teule imefanya kazi nzuri na kutokana na kazi yake nzuri imeleta mabadiliko ndani ya serikali na mabadiliko ni *process* hayawezi tu kwa mara moja tukaona tayari mabadiliko yametokea, lakini mabadiliko yameanza na tukipima tutaona mabadiliko hayo. Kwa hivyo sisi ndani ya serikali hata siku moja hatuwezi kusema tunadharau maoni ya Tume, tunadhalilisha Baraza ama lugha ya aina yoyote ile ya kuonesha kutokuyaamini mapendekezo au maamuzi ambayo Tume teule imetuletea. Sisi kwa kweli ndani ya serikali tuliyafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, asubuhi hapa nilikuwa nasoma, nimesoma kifungu baada ya kifungu na jumla humu mna vifungu 13 vilivyogawika katika sehemu ndogo ndogo na hakuna hata kifungu kimoja Mhe. Mwenyekiti, ambacho serikali

ilidharau ama serikali haikutoa majibu, ilifanya hivyo kwa kusimamia misingi ya haki, ilifanya hivyo kwa kusimamia misingi ya katiba, ilifanya hivyo kwa kusimamia misingi ya sheria kwa sababu serikali yetu, Baraza letu hili tukufu linaongozwa na katiba na sheria. Tunapokwenda nje ya taratibu za sheria kwa njia moja ama nyengine hatuwezi kupata muwafaka ulio mzuri, lakini yale yote ambayo Kamati Teule imeelezea serikali basi serikali imeyafanyia kazi kwa sababu serikali yenyewe tokea awali nia yake ni kuleta mabadiliko, nia yake ni kujenga uadilifu, nia yake ni kuacha kufanya kazi kwa mazowea na kufanya kazi kwa ufanisi na tija. Kwa hivyo, mengi ambayo Kamati Teule wameyasema ndio hayo ambayo serikali tunayafanyia kazi.

Kwa hivyo, ningependa tuondoshe dhana kwamba kuna aina yoyote ya dharau ama ya kutotekeleza maagizo ya Kamati Teule. Sisi ni watu wamoja inabidi tufanye kazi kwa pamoja. Namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu alipoeleza suala zima la kufanya kazi kwa pamoja kwa nia ya kufikia malengo ya kuwatumikia wananchi. Mwisho wa siku muajiri wetu sote ni wananchi, sote wanatupima, lakini wanachokitaka kutoka kwetu mambo yote tunayoyafanya tuyafanye kwa misingi ya haki. Kwa hivyo, jahazi letu ni moja.

Kubwa Waheshimiwa Wawakilishi tulizungumzia hapa suala la kuondoa muhali, kwa kiasi kikubwa serikali imeondoa muhali na imefanya kazi na hatua zimeanza kuchukuliwa. Kuna hatua ya kiutawala zimechukuliwa, kuna baadhi ya watendaji wameondoshwa kwenye nafasi zao na kuna wengine hatua zinaendelea kuchukuliwa na wengine hatua za kisheria zinachukuliwa. Kwa hivyo, hakuna jambo ambalo halikuchukuliwa na sisi tulikuja na kila kifungu na majibu yake na ukitizama hata Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakati wakitoa michango yao hawakwenda kwenye kifungu kwa kifungu walikuja na michango ya jumla kwa sababu waliona kwamba kuna kazi tayari zimeshafanywa. Kwa hivyo, ningependa tuwahakikishie Wajumbe wa Baraza letu tukufu kwamba nia na madhumuni ya serikali hii ni kufanya kazi kwa pamoja na kuondosha kila tatizo ambalo limetokea.

Lakini lazima tukubali kwamba, Katiba yetu hii inatuelekeza mgawanyo wa madaraka, serikali ina majukumu yake, Baraza la Wawakilishi lina majukumu yake, Mahkama ina majukumu yake. Sasa ni vizuri tukaweka misingi hiyo kwa msingi wa kufanya kazi pamoja, kwa msingi wa kuheshimiana ili yale ambayo wananchi wamekusudia wayapate tuweze kuwafanyia na kuwatumikia.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Mwenyekiti, na serikali kwa jumla tumeyasikia yale yote ambayo Waheshimiwa wameyaeleza hapa kwa kina. Ninachotaka kukuhakikishia kwamba yale yote ambayo yanahitaji sheria basi mkondo wa sheria utafanya wajibu wake na yale ambayo yanahitaji kuchukuliwa hatua za kiutawala tayari hatua zinachukuliwa na nyengine zitaendelea kuchukuliwa. Na kwa yale ambayo yanahitaji moja kwa moja kupata tafsiri yake ya Kimahkama basi hayo nayo yatakwenda kwa msingi huo huo.

Mimi nakumbuka hapa Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Spika, akifanya majumuisho hasa alipozungumzia mambo ya mikataba alisema ni vyema mambo haya mkayachukua, lakini yale ambayo mtaona yanaweza kuleta hasara zaidi kwa serikali basi hayo muyafanyie maamuzi ya busara ili serikali isipate hasara. Kwa hivyo, msingi wetu mkubwa yote ambayo tumeshauriwa sisi tumekwenda nayo.

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, sisi kwa sababu tulikuja na kipengele kimoja baada ya kimoja na kwa sababu michango ya leo haikuonesha ni kipengele kipi Wajumbe wa Baraza lako tukufu ambacho hawakuridhika nacho na majibu yetu ama ni maelezo gani ya ziada wanahitaji imekuwa ni vigumu sana kuweza kueleza ni nini.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Mwenyekiti, na serikali nina ushauri mmoja, kwa kuwa nia yetu ni kujenga, nia yetu ni kutatua matatizo, nia yetu ni kuhamasisha watu wetu wakawa waadilifu na nia ni kuwatumikia wananchi kwa busara, hekima, uadilifu na haki na serikali yetu haina nia ya kumuonea mtu yoyote, basi pendekezo letu Mhe. Mwenyekiti, kwamba bado kwa kuwa nafasi ipo na *document* hii tunayo sisi kwa upande wa serikali tukae tena na Kamati Teule itwambie ni wapi ambapo wameona serikali imekuwa haikuchukua hatua zinazofaa. Ni wapi ambapo wanaona kuna mapungufu ili kama alivyosema Mwanasheria Mkuu pale panapohitaji ufafanuzi wa kisheria hapa tueleze, tumechukua hatua hii kwa sababu sheria inataka tufanye hivi, na hapa tumechukua hatua hii kwa sababu za kiutawala, na hapa tumechukua hatua hii kwa sababu ya utaratibu wa kisheria uliopo.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kama serikali tuko tayari tukae tena na Kamati Teule tuangalie kipengele kwa kipengele na baadae baada ya kwishakuipitia na Kamati Teule ili tuje hapa kwenye Baraza lako tukufu tuwasilishe makubaliano yetu tuliyokubaliana kati ya sisi na Kamati Teule.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naamini Wajumbe wa Baraza lako tukufu watakubaliana nasi ili tuondoke hapa tujenge msimamo mmoja, tujenge dhamira na malengo yetu ya kuwatumikia wananchi bila ya kuleta mvutano kati ya Baraza na serikali. Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Kimsingi unaondoa taarifa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Wajumbe hawakuridhika na utaratibu wetu ambao tumeuwasilisha hapa serikali bado iko tayari kuzungumza na Wajumbe wako ili tuhakikishe kwamba tumepata muwafaka wa pamoja. Nia yetu ni kujenga mazingira mazuri ya maendeleo ya nchi yetu.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati Teule ya Kuchunguza Utendaji wa Baraza la Manispaa Zanzibar

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Utendaji wa Baraza la Manispaa): Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, ifuatayo ni Ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Utendaji wa Baraza la Manispaa la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba sote kwa pamoja tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuturuzuku uhai na kutujaalia afya njema inayotuwezesha kuhudhuria katika Mkutano huu wa Tisa kwa amni huku tukiwa wazima wa afya na kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Hatuna budi tuendelee kumuomba Allah kwa njia ya kutekeleza mema aliyotuamrisha ili azidi kuturuzuku uhai na afya njema.

Mhe. Mwenyekiti, pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii kwa niaba ya Kamati Teule kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa lengo la kuwasilisha ripoti ya kazi ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi iliyoundwa na Mhe. Spika, chini ya matakwa ya Kanuni ya Baraza hili mwezi wa Aprili mwaka 2012.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Baraza la Wawakilishi ya kuunda Kamati Teule kwa madhumuni ya kuchunguza jambo maalum yameoneshwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Kanuni ya Baraza la Wawakilishi kifungu cha 120 cha Kanuni za Kudumu za Baraza hilo tolep Nam. 212.

Mhe. Mwenyekiti, kumbukumbu zinaonesha kwamba, mara ya mwisho Baraza hili kuunda Kamati Teule ilikuwa mwaka 2011 ambayo ripoti yake iliwasilishwa mwaka huu katika Mkutano wa Saba ambayo ilifuatilia mambo mbali mbali yaliyoibuka katika Bajeti ya mwaka 2011/2012.
Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati Teule sina budi kumpongeza kwa dhati Mhe. Spika, wa Baraza la Wawakilishi (Mhe. Pandu Ameir Kificho) kwa namna anavyoliendesha Baraza hili ambalo ndio chombo cha wananchi. Tunamuomba Mhe. Spika, aendelee kufuata kanuni na sheria za Baraza la Wawakilishi ikiwa ni pamoja na sheria zote za nchi bila ya kuyumba wala kkuyumbishwa ili kusimamia vyema mageuzi ya demokrasia na utawala bora nchini. Bila shaka historia itakukumbuka kwa yote utakayoyafanya.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mkutano wa Saba wa Baraza la Nane la Wawakilishi la Zanzibar kwenye Kikao cha Tisa cha tarehe 11 Aprili, 2012, Mkutano ambao ulikuwa ni maalum kwa ajili ya kujadili na kupitisha Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza la Wawakilishi la Zanzibar liliridhia kuundwa kwa Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Kanuni ya 120 ya Kanuni za Baraza, Toleo la 2012.

Kamati Teule iliundwa kwa ajili ya kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa la Zanzibar juu ya shutuma mbali mbali zinazotolewa juu yake. Kamati Teule imekamilisha kazi hiyo na ifuatayo ni Taarifa kamili kwa mujibu wa Kanuni ya 122 ya Kanuni za Baraza, Toleo la 2012.

CHIMBUKO LA KAMATI TEULE

Taarifa Rasmi (*Hansard*) ya Majadiliano ya Baraza ya Mkutano wa Saba wa Baraza la Nane katika Kikao cha Tisa cha tarehe 11 Aprili, 2012 inaonesha baada ya kuwasilishwa kwa ripoti na Mhe. Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambaye katika uwasilishaji wake alianza kwa kusema;-

"Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja ya kuwasilisha ripoti ya kamati ya kuangalia utendaji wa Baraza la Manispaa na kupendekeza hatua za kuchukuliwaza kuimarisha utendaji wa Baraza hilo, ripoti hiyo ni kama ilivyotayarishwa na Kamati iliyoteuliwa na Serikali".

Baada ya uwasilishwaji wa ripoti hiyo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walipewa fursa ya kuijadili na hatimae kuipitisha ripoti hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 44 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Hata hivyo, Wajumbe hao waliikataa ripoti hiyo ya Serikali na kumuomba Mhe. Spika kwamba Baraza liunde Kamati Teule kuchunguza suala hili, ambapo Mhe. Asha Bakari Makame alisema;

"Mhe. Spika, nilisema nizungumze haya mimi kama kawaida yangu niungane na wenzangu yale yote kwamba hii ikawekwe Manispaa ifanyiwe kazi, ripoti hii ndio iwe ripoti kama ni kuundwa Kamati Teule iundwe naunga mkono na katika mmoja atakaekataa ni miye, kwa sababu nilichangia na miongoni niliyotoa uoza wa Manispaa mwengine ni mimi. .....".

Sambamba na hilo, Wajumbe alisisitiza kuundwa kwa Kamati hiyo, hasa tukizingatia kwamba serikali haiwezi kujichunguza yenyewe ni lazima kazi hiyo ifanywe na chombo chengine kama Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Omari Ali Shehe anathibitisha kauli hii kwa kusema kama ifuatavyo;-

"Mheshimiwa Spika, bado nasikitika kwamba serikali haikuleta jawabu juu ya tuliyoyataka, kwa kweli imetupotezea muda, kwa sababu tuliliomba Baraza hili liunde Kamati Teule kuchunguza serikali ikaingilia kati. Kwa maana hiyo Mhe. Spika, mimi nataka nitoe hoja, kwamba ripoti hii tunaikataa kwa sababu haikufanya chochote."

Kauli hii ya Mheshimiwa Omar inalega kupinga ripoti iliyowasilishwa na Serikali kuhusu kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa baada ya kuibuka mambo mbali mbali katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2011/2012, ambapo Wajumbe waliomba Baraza liunde Kamati Teule kuchunguza suala hili na badala yake serikali iliomba nafasi hiyo ya kuunda Tume juu ya suala hili.

Aidha, Mhe. Omar aliendelea kwa kusema;-

"Mheshimiwa Spika, kwa wakati ule Baraza lilitoa hoja lakini Serikali iliingilia kati ikasema wao tayari wameshaunda Tume, wameharibu wao na wao waunde Tume wajichunguze wao, kitu ambacho leo kimedhihirika kwamba Serikali haikuwa na uwezo huo wa kuharibu na kujichunguza wenyewe. Ripoti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri imeonyesha hivyo…."

Katika kuweka msisitizo juu ya hoja ya kuundwa Kamati Teule na kwa mnasaba wa kuikataa ripoti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Makame Mshimba Mbarouk nae alichangia kama ifuatavyo;-

"Mheshimiwa Spika, siku moja nilisema hapa kuwa tutumieni kanuni ya ukurasa wa 88, kifungu cha 117, nilisema hapa kwa vizuri tu leo ataona dhahiri Mheshimiwa Rais kama hatuna watendaji, tuseme ukweli. Sasa kweli leo Mheshimiwa Rais aangalie ripoti hii na ya Madiwani ipi ya kweli, Madiwani hatukuwaambia sisi undeni Tume……".

Hivyo, maelezo yote hayo ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi yanalenga kuunga mkono hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule ili kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa.

Baada ya Mheshimiwa Spika kukubaliana na hoja hiyo ya kuundwa Kamati Teule alisema maneno yafuatayo;-

"Waheshimiwa wajumbe nilitaka nichukue kipengele hicho, kazi ya kupendekeza Kamati teule kwa njia ya hoja ilikwishafanyika ambapo Mheshimiwa Asha Bakari Makame ndiye aliyetoa hoja hiyo na wajumbe mkaamua

kwamba sawa hiyo kamati teule iundwe. Kwa hivyo, kwa mujibu wa kanuni hiyo ya 117(2) kazi ya kuamua au kuunda hiyo kamati teule ni kazi ya Spika. Hivyo chini ya ibara hiyo ninafuraha kutangaza hiyo kamati teule ambayo inaundwa kwa mujibu wa kifungu hicho".

MUUNDO WA KAMATI

Kutokana na maamuzi hayo ya Baraza, mnamo tarehe 20/04/2012, Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi aliteua Wajumbe wa Kamati Teule kwa mujibu wa kifungu cha 120(3) cha Kanuni za Baraza, Toleo la 2012, kwa ajili ya kazi hiyo. Wajumbe hao ni hawa wafuatao:-

1. Mheshimiwa Salmin Awadh Salmin Mjumbe.
2. Mheshimiwa Asha Bakari Makame Mjumbe.
3. Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu Mjumbe.
4. Mheshimiwa Mwanaidi Kassim Mussa Mjumbe.
5. Mheshimiwa Abdalla Juma Abdalla Mjumbe.

Kamati Teule ilikuwa na Makatibu wawili wafuatao: -

1. Ndugu Nasra Awadh Salmin Katibu.
2. Ndugu Maryam Rashid Ali Katibu.

Mhe. Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwasilisha shukurani za Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwako kwa busara na hekma yako ya kututeuwa kuunda kamati hii ambayo ina changamoto nyingi.

Aidha naomba pia niwasilishe shukurani za Waheshimiwa Wajumbe wa kamati, Waheshimiwa wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuridhia kwako kuunda kamati hii kwa lengo lile lile la kusimamia utekelezaji bora wa shughuli za serikali yetu. Naomba nitumie nafasi hii kwa kuwashukuru sana.

HADIDU REJEA:

Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa Azimio la Baraza la tarehe 11 Aprili, 2012 ilipewa Hadidu za Rejea Nne kama ifuatavyo: -

1. Kuchunguza Mikataba ya uwekaji Mabango ya Matangazo katika barabara mbali mbali iliyoingiwa baina ya Baraza la Manispaa Zanzibar na Kampuni mbali mbali na utekelezaji wa masharti ya mikataba hiyo.

2. Kuchunguza taratibu za uidhinishaji wa matumizi na uuzaji wa mali za Baraza la Manispaa Zanzibar.

3. Kuchunguza taratibu za uajiri na upandishaji vyeo katika Baraza la Manispaa na kama taratibu hizo zinazingatia sifa zinazohitajika kwa nafasi husika.

4. Kuchunguza utendaji wa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa Zanzibar juu ya tuhuma za kutofuata Sheria na Kanuni kwa makusudi, ubadhirifu wa fedha na kuhusika kwake katika migogoro inayolikumba Baraza la Manispaa.

NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA KUKAMILISHA KAZI

Mhe. Mwenyekiti, Kamati Teule imezifanyia kazi Hadidu za Rejea Nne ilizopewa kwa kufanya yafuatayo: -

1. Kupitia Sheria na Kanuni mbalimbali na kuzichambua kwa kuzioanisha na Hadidu za Rejea.

   Sheria na Kanuni zilizohusika ni pamoja na: -
   - i. Sheria ya Manunuzi na Mauzo ya Mali za Serikali, Namba 9 ya 2005.
   - ii. Sheria ya Baraza la Manispaa, Namba 3 ya 1995.
   - iii. Sheria ya Ardhi, Namba 12 ya 1992
   - iv. Sheria ya Kinga, Fursa na Uwezo wa Wajumbe, Namba 4 ya 2007.

v. Sheria ya Makosa ya Jinai, Sura ya 13.
vi. Kanuni za Baraza la Manispaa za 2003.
vii. Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Toleo la 2012.
viii. Kanuni ya Utumishi Serikalini ya mwaka 1997

2. Kufanya mahojiano na watu mbalimbali kama ifuatavyo: -

i. Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
ii. Mstahiki Meya wa Manispaa ya Zanzibar.
iii. Madiwani wa Baraza la Manispaa la Zanzibar.
iv. Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa, Zanzibar.
v. Watendaji mbali mbali wa Baraza la Manispaa
vi. Wafanyabiashara mbali mbali.
vii. Wateja au Watu mbali mbali wanaotoa huduma katika Baraza la Manispaa.

3. Kufanya ziara katika maeneo mbali mbali kutokana na hadidu rejea husika.

4. Kupitia na kuzichambua nyaraka mbali mbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati.

UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI.
Mhe. Mwenyekiti, kamati hii lianza kazi zake rasmi mnamo tarehe 21/05/2012 kwa muda wa wiki mbili, ambapo katika kikao chake cha mwanzo Wajumbe walimchagua Mwenyekiti wa Kamati, kwa kuzingatia Kanuni ya 120(4), ambapo Wajumbe kwa umoja wao waliniteua mimi (Mheshimiwa Salmin Awadh Salmin) kuwa Mwenyekiti wa Kamati Teule.

Kamati iliendele kufanya kazi hadi siku za mapumziko kutokana na umuhimu wa kazi yenyewe. Vile vile, katika kuhahakikisha kazi hii inakamilika kwa wakati Kamati iliendelea na kazi kwa wiki ya tatu baada ya kupata ridhaa ya Mheshimiwa Spika. Kwa ujumla Kamati hii ilifanyakazi kwa muda wa siku kumi na tisa (19).

Mhe. Mwenyekiti, ripoti tunayoiwasilisha leo ina jumla kurasa 62 na viambatanisho 59 pamoja na footnote 84. Naomba sasa nitumie nafasi hii kuwasilisha ripoti hii kwenu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu ikiwa ni matokeo ya uchunguzi wa kamati kwa kila hadidu rejea.

HADIDU REJEA YA KWANZA

KUCHUNGUZA MIKATABA YA UWEKAJI MABANGO YA BARABARANI ILIYOINGIWA BAINA YA MANISPAA NA KAMPUNI MBALIMBALI.

Utangulizi.
Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilitakiwa kuchunguza Mikataba ya uwekaji mabango ya barabarani iliyoingiwa baina ya Baraza la Manispaa na Kampuni mbali mbali na kuangalia utekelezaji wa masharti ya Mikataba hiyo. Katika kutekeleza hilo, Kamati kwanza ilitaka kujiridhisha kuwepo kwa Mikataba hiyo, na ndipo kuweza kuangalia utekelezaji wa masharti ya mikataba hiyo, na kama utekelezaji wake unafuata utaratibu wa kisheria.

Ili kujiridha kuwepo kwa mabango hayo baada ya hapo ilikutana na viongozi wa kampuni zenyewe ili kupata uhalisia wa kadhia hiyo. Katika kupata ufafanuzi yakinifu wa hadidu rejea hii, kamati ilikutana na madiwani ambao ni sehemu ya Baraza la Manispaa tarehe 4/6/2012 katika afisi za Baraza la Manispaa ziliopo Malindi Zanzíbar

Pia, tarehe 5/6/2012 Kamati ilikutana na Ndugu Mzee Khamis Juma ambae alishiriki katika utiaji saini kwa baadhi ya Mikataba pamoja na Ndugu Mwamvua Nassor ambae ni afisa mabango na ambae anahusika katika utaratibu mzima wa mabango. Vile vile, katika kupata upembuzi halisi juu ya hadidu rejea hii kamati ilikutana na kufanya mahojiano na Kaimu Mhasibu Mkuu wa Baraza la Manispaa, Ndugu Eshe Juma Abdalla ambae alihusika katika masuala mazima yanayohusiana na malipo ya uwekaji mabango hayo.

Aidha, Kamati ilikutana na aliyekuwa Mwanasheria wa Baraza la Manispaa Ndugu Omar Mcha Hamza, ambapo Kamati ilitaka kujua iwapo alishiriki kuandaa mikataba hiyo au la na iwapo alishiriki jee mikataba hiyo imefuata utaratibu wa Sheria.

Kamati haikuishia hapo, iliziita pia, Kampuni zilizoingia mkataba na Baraza la Manispaa na ilibahatika kukutana na mwakilishi wa Kampuni ya Syscorp Ndugu Beatus F. Kaboja ambae ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo mnamo tarehe 8/6/2012. Watendaji wengine waliotoa maelezo yao mbele ya Kamati kuhusiana na Hadudi Rejea hii ni pamoja na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa, Mstahiki Meya wa Baraza na Waziri wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Mwinyihaji Makame.

Baada ya utangulizi huo ni vyema tukapata ufafanuzi juu ya hadidu rejea husika.

Uchambuzi wa hadidu rejea husika.
Kamati iliigawa hadidu rejea hii katika makundi mawili kama ifuatavyo;-

1. Mabango ya matangazo yaliyowekwa kwenye taa za barabarani.

2. Mabango ya matangazo ambayo yanawekwa maeneo mengine ya barabarani.

Kabla ya kutoa uchambuzi wa makundi haya ni vyema tukaeleza namna wafanyabiashara wanavyofanya hadi kupata kibali cha kuweka matangazo hayo. Katika kupata taarifa juu ya kadhia hii, Afisa anaehusika na mabango ya matangazo Ndugu Mwamvua Nassor aliieleza Kamati kwamba baada ya Wafanyabiashara kufika Afisini hapo hupatiwa maelezo ya awali ikiwa ni pamoja na kushauriwa kukagua eneo wanalohitaji kuweka matangazo yao, na baada ya kukagua na kuridhika na eneo hilo ndipo wanapotakiwa kuwasilisha maombi yao kwa Mkurugenzi. Baada ya maombi hayo kukubaliwa taratibu za malipo hufuata, ambapo Kitengo hiki hupokea malipo kwa ajili ya shughuli hii chini ya Tsh. 1,500,000/- na zaidi ya hapo hupokelewa kwa Mhasibu.

Mabango ya matangazo yaliyowekwa kwenye taa za barabarani
Baraza la Manispaa ndilo lenye mamlaka ya kusimamia taa za barabarani, kwa kuwa muda mrefu taa hizo zilikuwa haziwaki, Baraza hilo lilikuja na wazo la kuwahamasisha wafanyabishara kwa ajili ya kuweka mabango ya matangazo ya biashara kwa malengo ya kuziwasha taa hizo.

Kamati katika kufuatilia hadidu rejea hii, iligundua kuna Mikataba minne (4) ya uwekaji mabango iliyoingiwa baina ya Manispaa na Kampuni mbali mbali kama zifuatazo;-

a) Kampuni ya Ashton Media Ltd
b) Kampuni ya Syscorp Media Ltd
c) Kampuni ya Continental Outdoor (INM)
d) Kampuni ya East Africa Media Ltd

Uchambuzi juu ya mikataba.
Kati ya mikataba minne iliyofungwa na Baraza la Manispaa na Kampuni zinazohusika na matangazo, Kamati imeichambua mikataba mitatu. Hii ni kutokana na kuwa Kampuni ya East Africa Media Ltd imelishtaki Baraza la Manispaa Mahkamani na kwa mujibu wa kanuni ya 59(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012, jambo ambalo lipo Mahkamani halipaswi kujadiliwa na Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Ufungwaji wa Mikataba na Utekelezwaji wake.
Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kuna malalamiko mbali mbali kuhusiana na mikataba iliyofungwa baina ya Baraza la Manispaa na Kampuni mbalimbali, Kamati ilitaka kujua namna mikataba hiyo ilivyofungwa na jinsi ilivyotekelezwa.

Kampuni ya Ashton Media Ltd ndio Kampuni ya mwanzo iliyofunga mkataba na Baraza la Manispaa kwa ajili ya kuweka mabango ya matangazo ya biashara kwa malengo ya kuwasha taa za barabarani mnamo tarehe 23 Januari, 2009. Kampuni hiyo ilifunga mkataba wa miaka mitano (5) ambao ulisainiwa na aliekuwa Mkurugenzi wa Baraza Ndugu Mabrouk Jabu Makame kwa madhumuni yaliyoyaelezwa hapo kabla.

Kwa mujibu wa Mkataba huu Kampuni hii ilitakiwa kuweka taa katika barabara tatu kama zifuatazo;-

i. Kutoka 'Creek road' hadi Chuo cha Mafunzo, kupitia Kariakoo hadi Benki Kuu ya Tanzania (Bank of Tanzania – BOT).
ii. Kutoka Benki Kuu ya Tanzania hadi Mtoni Petrol depot.
iii. Kutoka 'Creek road' hadi BOT

Katika Mkataba huu, Kampuni hii ilitakiwa kuanza kuweka, kutengeneza na kutumia milingoti ya taa za barabarani ndani ya wiki mbili baada ya kusainiwa kwa Mkataba huu na kukamilisha kazi hiyo si zaidi ya miezi 3, kushindwa kutekeleza hilo upande wa pili wa mkataba ambao ni Baraza la Manispaa utaingia mkataba mwengine na Taasisi nyengine.

Mnamo tarehe 23 Aprili, 2009, Kampuni ya E.A Media Ltd ilifunga mkataba na Baraza la Manispaa kwa madhumuni kama hayo na kwa kipindi cha miaka mitano. Barabara zenyewe ni kama zifuatazo;-

i. Kutoka Mlandege hadi Michenzani Roundabout.
ii. Kutoka Michenzani Roundabout hadi Gofu Msikitini

Katika Mkataba huu, Kampuni hii ilitakiwa kuanza shughuli zake kwa masharti kama iliyopewa Kampuni ya Ashton Media Ltd.

Mnamo tarehe 31 Agosti, 2009 Baraza la Manispaa lilifunga mkataba na Kampuni ya INM Outdoor (T) Ltd (ambayo kwa sasa hivi inajulikana kuwa ni Continetal Outdoor) kwa ajili ya kuweka mabango ya matangazo ya biashara kwa malengo ya kuwasha taa za barabarani. Mkataba huo ni wa miaka mitano (5), ambapo Kampuni hii ilitakiwa kuanza kuweka, kutengeneza na kutumia milingoti ya taa za barabarani ndani ya wiki mbili baada ya kusainiwa kwa Mkataba huu na kukamilisha kazi hiyo si zaidi ya miezi 3, kushindwa kutekeleza hilo upande wa pili wa mkataba ambao ni Baraza la Manispaa utaingia mkataba mwengine na Taasisi nyengine.

Mkataba huo ulihusisha barabara moja tu, nayo ni kutoka Maisara (Mnazi Mmoja Hospital) mpaka Uwanja wa Ndege, (Nyerere Road).

Kamati haikubahatika kuhojiana na Viongozi wa Kampuni ya INM Outdoor kwa kuwa walikuwa wanakabiliwa na shughuli nyengine. Hata hivyo, katika kuchunguza kadhia hii ilifanikiwa kupata baadhi ya taarifa kama ifuatavyo;-

Katika kutekeleza mkataba wake Kampuni hii iliwahi kuweka mabango katika barabara iliyoruhusiwa pamoja na kufanya malipo ya awali ya Tsh. 32,408,000/- kwa Hundi Namba 008513 na kupatiwa risiti ya tarehe 25 Novemba, 2009 yenye nambari 00204.

Kamati ilikutana na kufanya mahojianao na Watendaji wa Baraza la Manispaa ambao waliieleza Kamati kwamba Kampuni ya INM Outdoor (T) Ltd iliwahi kufunga mkataba na Baraza kwa ajili ya kazi hiyo. Hata hivyo, Kampuni hii ilishindwa kutekeleza masharti ya mkataba na kutokana na hilo Baraza la Manispaa liliamua kuondoa mabango yaliyokuwa yamewekwa na Kampuni hii.

Kuhusiana na malipo ya Tsh. 32,408,000/- Watendaji hawa waliieleza Kamati kuwa fedha hizo zilitolewa kama ni mchango wa kusaidia kutengeneza taa za Mji Mkongwe na sio kama zinavyoonyeshwa kwenye risiti.

Pamoja na mkataba wa tarehe 23 Januari, 2009, Kampuni ya Ashton Media Ltd iliomba kufunga mkataba wa nyongeza 'Addendum to Contract' mnamo tarehe 20 Oktoba, 2009 na kuongezewa barabara zifuatazo;-

i. Kutoka Mlandege mpaka Maisara kupitia Michenzani Roundabout.

ii. Kutoka Uwanja wa Ndege mpaka Mnazi Mmoja Hospital.

iii. Kutoka Uwanja wa Ndege mpaka Mtoni kupitia Mombasa.

Mkataba huu ulielekeza kwamba masharti yaliyotajwa kwenye Mkataba Mama (Principal Contract) yatatumika pia katika mkataba huu wa nyongeza, isipokuwa, Kampuni hii imetakiwa kukamilisha utekelezaji wa Mkataba Mama ndani ya miezi sita.

Mnamo tarehe 10 Novemba, 2010 Kampuni ya Syscorp Media Ltd ilifunga mikataba miwili na Baraza la Manispaa kwa ajili ya kuweka mabango ya matangazo ya biashara kwa nia ya kuwasha taa za barabarani. Barabara zenyewe ni kama zifuatazo;-

i. Kutoka barabara ya BOT mpaka Prison headquater.

ii. Kutoka barabara ya Airport mpaka Mnazi Mmoja.

Masharti ya utekelezaji wa mikataba hii imefanana na yale masharti ya Kampuni nyengine.

Katika kufuatilia utekelezwaji wa mkataba huu Kamati ilibahatika kuhojiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Syscop Media Ltd Ndugu Beatus Francis Kaboje ambaye alieleza kwamba mnamo mwaka 2010 walipeleka maombi ya kuweka matangazo katika barabara moja ya Uwanja wa Ndege hadi Mnazi Mmoja.

Suala la kupewa barabara ya pili kutoka BOT hadi Mnazimmoja lilikuja kutokana na kwamba hapo awali kulikuwa na baadhi ya Kampuni ambapo ziliwahi kuomba shughuli ya kuweka matangazo katika taa za barabarani na kutakiwa kuwasha taa kwanza na baadae ndio waweke matangazo. Kampuni hizo zilishindwa kutekeleza hilo na waliweka matangazo yao kinyume na mkataba. Mkurugenzi wa Baraza aliitaka kwanza Kampuni hii kuwasha taa za barabara ya kutoka BOT hadi Chuo cha Mafunzo bila ya mkataba wowote. Walihisi wameambiwa wafanye hivyo kama ni kutumikia adhabu ya Kampuni nyengine zilizoshindwa kutekeleza mikataba yao. Kwa kuwa utengenezaji huo utawagharimu fedha nyingi takriban Tsh. 100, 000,000/- hawakuwa tayari kutekeleza hilo. Hata hivyo, baadhi ya watu waliwatia moyo na kuwaomba watekeleze na hapo baadae watapatiwa mkataba na walifanya hivyo.
Alieleza kwamba walifanikisha hilo ndani ya mwezi mmoja na baada ya hapo wakarudi kwa Mkurugenzi ili waweze kupatiwa mkataba huo. Baada ya usumbufu mkubwa ndio wakapatiwa mkataba kwa masharti ya kwamba watangaze matangazo ya Kampuni ya Zantel na kwa vile walikuwa wana mkataba na Kampuni hiyo haikuwa tatizo kwa upande wao kutekeleza hilo.

Baada ya Kampuni ya Syscorp kuanza kazi ya kuweka matangazo Kampuni mbili (Kampuni ya Ashton Media Ltd na Kampuni ya E.A Media Ltd) ziliwasilisha taarifa zao Makao Makuu ya Zantel na kudai kuwa wao ndio wenye mkataba wa barabara hiyo (Uwanja wa Ndege hadi Mnazi Mmoja), ingawa Kampuni hizo zilishindwa kutekeleza masharti ya mkataba huo. Kampuni ya Ashton Media ndio ya kwanza kupewa kazi hiyo na kufuatiwa na Kampuni ya E.A Media ambayo iliweka matangazo kwa muda wa miaka miwili ingawa ilishindwa kuwasha taa.

Alieleza kuwa wakati wanaweka mabango walivamiwa na kundi la vijana ambao walikuwa wanayashusha mabango hayo kwa kushirikiana na Polisi. Kutokana na hali hiyo baadhi ya Watendaji wao walikamatwa na Polisi hao na kuwekwa ndani bila ya hatia yoyote. Kwa kuwa Kampuni ya Syscop baadhi ya Watendaji wake wametoka nje ya nchi, Mabalozi wa nchi za nje ambazo Watendaji hao wanatoka walilaani sana kitendo hicho na hasa baada ya Baraza la Manispaa kushindwa kutoa msaada wa kuwatoa baada ya kuombwa na Kampuni hiyo.

Hali hii ya uvunjwaji wa amani ilijitokeza baada ya Baraza la Manispaa kuipatia Kampuni ya Syscop mabango yaliyokuwa yanamilikiwa na Kampuni ya Continental Outdoor. Kampuni ya Syscop ilitakiwa na Baraza kuyalipia mabango hayo Tsh. 12, 000,000/- ikiwa ni gharama ya kushushwa kwenye milingoti ya taa. Fedha hizo zililipwa kwa awamu mbili kama ifuatavyo;- Awamu ya kwanza walilipa Tsh. 3, 000,000/- kwa Hundi Namba 295446 ya tarehe 10 Novemba, 2010 na awamu ya pili walilipa Tsh. 9, 000,000/- kwa Hundi Namba 295255 ya tarehe 10 Disemba, 2010. Malipo hayo hayakuwa na maslahi kwao kwani mabango hayo baadae yalichukuliwa na wenyewe (Kampuni ya Continental Outdoor).

Halikadhalika, Ndugu Kaboje aliieleza Kamati kuwa waliwahi kulipa Tsh. 800,000/- kwa Hundi Namba 295246 ya tarehe 10 Novemba, 2010 kwa ajili ya malipo ya gari ‘Cren’ ambayo waliitumia kwa kazi ya ushushaji wa mabango.

Mkataba na Zantel ulitakiwa uanze tangu mwezi wa Januari, 2011. Hata hivyo, kutokana na sababu hizo mkataba ulianza mwezi wa Juni, 2011. Kitendo hiki kiliwatia sana hasara kwani baadhi ya vitu vilikuwa vimeshaibiwa pamoja na baadhi ya nyaya kukatwa katwa kutokana na matengenezo ya barabara. Hali hii iliwaongezea gharama kwani kila mwezi iliwagharimu sio chini ya Tsh. 25, 000,000/- na pale wanapoieleza hali hii kwa Mkurugenzi wa Manispaa anakuwa hataki kuelewa na hutoa vitisho mbali mbali na kusisitiza kuwa anachotaka yeye ni taa kuwaka tu.

Kwa upande wa barabara ya Maisara hadi Uwanja wa Ndege, Ndugu Kaboje alieleza kuwa waliruhusiwa kuweka matangazo katika nguzo za taa kwa barua yenye kumbukumbu Namba ZMC/MB VOL.IV/41 ya tarehe 13 Oktoba, 2011 baada ya kuwasha taa.

Alieleza kuwa baadhi ya cable zilikuwepo katika barabara hiyo lakini walifanya kazi ya kuweka taa hizo katika mazingira magumu. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya wananchi walikuwa wakizifukua na kuziiba cable. Kitendo hiki kimewafanya kutumia gharama za ziada ili kufanikisha kazi yao. Suala hili la wizi Mkurugenzi wa Baraza analifahamu na imefika wakati anawasaidia kutafuta cable.

Katika kupata maelezo zaidi Kamati ilifanya mahojiano na baadhi ya Watendaji wa Baraza la Manispaa ambao waliithibitishia Kamati kuwa Kampuni hii ilipewa kazi hizo na Baraza la Manispaa. Katika kutekeleza shughuli zake Kampuni hii ilitakiwa kulipia gharama za ushushwaji wa mabango ya Kampuni ya Continetal Outdoor Ltd uliofanywa na Mkandarasi ambazo ni Tsh. 12, 000,000/-. Aidha, walieleza na Kamati iliridhika kuwa wakati Kampuni hii inafanya malipo hayo mabango yalikuwa tayari yameshashushwa na Mkandarasi.

Kamati katika kuzidi kupata taarifa kuhusiana na hadidu rejea hii ilikutana na Madiwani ambao walieleza kwamba hawajawahi kupitisha mikataba kuhusiana na mambo ya mabango katika ngazi ya Kamati za Kudumu na Baraza Zima hata kwa wale Madiwani ambao wamo katika Baraza kwa vipindi viwili sasa. Sambamba na hilo walieleza kuwa hawajui hata Kamati yenye mamlaka ya kujadili na kupitisha mambo hayo.

Kuchunguza kama ufungaji wa Mikataba hii imefuata masharti ya Sheria na Kanuni zilizopo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati katika kuchunguza mikataba hii ilikuwa na shauku ya kutaka kujua pamoja na mambo mengine kama mikataba hii imefungwa kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Manispaa, Namba 3 ya 1995 na Kanuni za Kudumu za Baraza la Manispaa.

Kamati ilizingatia masharti ya kanuni ya 55(b) ya Kanuni za Baraza la Manispaa za 2003 ambayo inaeleza kuwa;-

'Bila kuathiri masharti ya Sheria ya Baraza la Manispaa, 1995, Baraza linaweza kufanya mikataba kwa kuzingatia taratibu zifuatazo;-

Iwapo thamani ya kazi inayofanywa au thamani ya mali itakayoagizwa ni zaidi ya Shilingi 5, 000,000/- kibali cha Baraza kwa azimio hilo itabidi kipatikane'.

Kwa mnasaba wa kanuni hiyo, Kamati hii ilimhoji Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ambaye alieleza kwamba mikataba hiyo imefuata matakwa ya kanuni hiyo. Katika kuthibitisha kauli yake hiyo Kamati ilimtaka Mkurugenzi huyo kuipatia nakala ya kumbukumbu za mikutano ya Baraza ambayo imepitisha azimio hilo. Hadi Kamati inawasilisha ripoti hii Mkurugenzi wa Baraza alishindwa kuwakilisha kumbukumbu hizo kwa kisingizio kwamba baadhi ya Nyaraka huibiwa na watendaji wa Baraza la Manispaa.

Vile vile, katika kuchunguza suala hilo Kamati ilizingatia masharti ya kifungu cha 20(2) cha Sheria Namba 3 ya 1995. Kifungu hiki kinaelekeza kwamba;-

'Kila mkataba ambao Baraza limepewa uwezo kisheria kufunga utatiwa muhuri wa Baraza mbele ya Meya au Naibu Meya, na Mkurugenzi au afisa mwengine yeyote wa Baraza.....' (Tafsiri ya Kamati).

Kwa mujibu wa kifungu hicho mikataba hiyo haikuzingatia masharti yanayotakiwa ya uwepo au ushuhuda ama wa Mstahiki Meya au Naibu Meya na badala yake sehemu zote mbili hushuhudiwa na Mkurugenzi au Afisa mwengine wa Baraza.

Kuzingatia kama Kanuni za Kawaida za Utawala kama zinafuatwa katika utekelezaji wa Mkataba

Mhe. Mwenyekiti, takriban Mikataba yote ya Mabango ya Matangazo iliyofungwa na Baraza la Manispaa ilikuwa na kifungu 1.1 kilichohusu masharti ya muda wa utekelezaji wa mikataba (Duration). Kifungu hicho kinatoa mamlaka kwa Baraza la Manispaa kuingia mkataba na Kampuni nyengine endapo Kampuni iliyopewa kazi hiyo awali itashindwa kutimiza masharti hayo.

Ingawa utekelezaji wa kipengele cha 1.1 cha mikataba hii kilizitaka Kampuni hizi kuanza kuweka, kutengeneza na kutumia milingoti ya taa za barabarani ndani ya wiki mbili baada ya kusainiwa kwa Mkataba huu na kukamilisha kazi hiyo si zaidi ya miezi 3, kushindwa kutekeleza hilo upande wa pili wa mkataba ambao ni Baraza la Manispaa utaingia mkataba mwengine na Taasisi nyengine. Hata hivyo, Mkurugenzi alitakiwa ama kuiita au kuiandikia barua Kampuni yoyote iliyokuwa inakwenda kinyume na mkataba ili kuepusha mizozo isiyo yalazima.

Kampuni zilizohusika zililalamikia kwamba masharti ya kifungu hiki yalikuwa yakitumika kuwafutia mikataba bila ya hata kufuata kanuni za kawaida za utawala (Routeen administrative procedure) za ama kuwaita au kuwaandikia barua kuwapa indhari juu ya lengo la kufuta mikataba nao.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa aliieleza Kamati kuwa alifuata kipengele Namba 1.1 ambacho kinampa mamlaka ya kufunga mkataba na mtu mwengine, endapo aliyefunga mkataba wa awali atakwenda kinyume na mkataba huo.

Pamoja na hayo alitueleza kwamba mara kadhaa aliwahi kuzungumza na Kampuni hizo na kuwataka kutekeleza mikataba yao. Hata hivyo, Mkurugenzi huyo aliwasilisha mbele ya Kamati kumbukumbu moja tu ya Kikao kinachohusiana na mazungumzo hayo.

Kamati ilimhoji pia Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Baraza la Manispaa naye alieleza kuwa baada ya ugomvi kutokea aliziita Kampuni zote pamoja na Mkurugenzi wa Baraza ili kutatua mgogoro huo. Kwa bahati hawakuwahi kufikia suluhisho Mkurugenzi alipata maradhi na hakukuwa na mtendaji yeyote wa Baraza ambaye aliweza kutoa taarifa.

Kwa kuwa shughuli ya utengenezaji wa mikataba inahitaji taaluma ya sheria, Kamati ilimhoji aliyekuwa Mwanasheria wa Baraza la Manispaa Ndugu Omar Mcha Hamza ambaye alieleza kwamba baadhi ya mikataba ilifungwa bila ya kutoa ushauri wake. Kutokana na kitendo hicho imebainika kuwa mikataba hiyo ina baadhi ya mapungufu.

Kuchunguza taratibu za uwekaji wa Mabango ya Matangazo yaliyokuwa hayakuwekwa kwenye taa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilifuatilia utaratibu wa uwekaji wa mabango ya matangazo yaliyokuwa hayakuwekwa kwenye taa. Mabango haya ni yale yaliyopo katika barabara mbali mbali za Mji wa Zanzibar kama vile katika makutano ya barabara ya Kinazini, Michenzani, Kariakoo, Kiembesamaki na kwengineko, pamoja na yale matangazo yanayoandaliwa kwa vitambaa.

Kamati ilielezwa na Mkurugenzi pamoja na Watendaji wa Baraza la Manispaa kwamba mabango haya hayana mikataba, isipokuwa, wahusika huandika barua ya maombi kwa Mkurugenzi na akiridhika huwakubalia.

Mabango ya matangazo yaliyopo barabarani ambayo sio ya vitambaa hulipiwa kwa mwaka na malipo yake hufanywa kwa mujibu wa ukubwa wa bango lenyewe, ambapo kwa futi wanalipa Tsh. 10,000/-. Kabla ya Baraza kuruhusu kuwekwa bango hilo huwasiliana na Idara ya Majenzi ambayo huangalia kama eneo hilo haikupita miundo mbinu ya aina yoyote. Endapo Idara hii itaridhika kuwa hakuna hitilafu yoyote dhidi ya eneo hilo hatua za kuwaruhusu huafuata.

Muhtasari wa mambo yaliobainika katika hadidu rejea hii

Baada ya kufuatilia kadhia hii Kamati hii imebaini mambo yafuatayo;-

i) Watendaji wa Baraza la Manispaa wakiongozwa na Mkurugenzi, hawafuati Sheria na Kanuni za Baraza katika kuingia na kufunga mikataba.

ii) Masharti ya mikataba hiyo hayatekelezwi ipasavyo, kwa mfano; kipengele cha 1.1 katika mikataba yote ya uwekaji mabango ambacho kinazungumzia kuhusu suala la muda kimekuwa kikitumika vibaya kwa upande mmoja kutoa maamuzi bila ya kuuhusisha upande wa pili. Hali ambayo imepelekea kutokezea kwa muingiliano wa mikataba na kupelekea migogoro baina ya Kampuni za matangazo na Baraza la Manispaa.

iii) Gharama walizotumia Kampuni ya *Syscorp* haziendani na gharama halisi ya kazi ya ushushaji wa mabango mbali ya kwamba Kamati ilijiridhisha kwamba hakukuwa na mabango yaliyokuwa yanahitaji kushushwa kwa wakati ule.

iv) Baadhi ya watendaji wa Baraza la Manispaa hawafuati maadili ya kazi kama wanavyotakiwa bali hufanya kazi zao kinyume na utaratibu kwa kufuata maelekezo ya Mkurugenzi.

v) Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa amekuwa akitumia madaraka yake vibaya kwa kuamua vile anavyoona inafaa.

vi) Suala la mabango, uendeshaji wake na mapato yake yanaamuliwa kibinafsi zaidi kutokana na kutowekwa chini ya Kamati yoyote kati ya Kamati za Baraza la Manispaa.

vii) Mkataba wa Baraza na Kampuni ya *Syscorp* ulifungwa wakati Baraza la Manispaa lililopita limemaliza muda wake na Baraza jipya halijazinduliwa na hivyo kushindwa kupata azimio la Baraza.

viii) Mwanasheria wa Baraza hashirikishiwi ipasavyo katika uandaaji wa Mikataba mbali mbali. Kitendo hiki hupelekea mikataba ya Baraza kuwa na mapungufu mengi na kuifanya mikataba hiyo iweze kutangazwa kuwa batili.

Hatua za kuchukuliwa kutokana na matokeo ya uchunguzi huo:

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na matokeo ya uchunguzi, Kamati inapendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe:-

i. Kutokana na vitendo mbalimbali vya ukiukaji wa Sheria na Kanuni za Baraza vilivyobainika dhidi ya Baraza la Manispaa, Kamati hii inaishauri serikali kumchukulia hatua za kinidhamu na kisheria Mkurugenzi huyo.

ii. Ingawa Baraza la Manispaa ni Taasisi inayojitegemea (*Body Corporate*) kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Baraza la Manispaa, bado serikali kwa kupitia Waziri mwenye dhamana na taasisi hii, ihakikishe kuwa taasisi zake zinatekeleza majukumu yake waliyopewa kwa misingi ya Sheria na Kanuni za nchi.

iii. Katika kuhakikisha kuwa kuna utekelezwaji mzuri wa masharti ya mikataba lazima mikataba hiyo izingatie sheria zinazoongoza masuala ya mikataba na kanuni za kawaida za mikataba.

iv. Serikali ichukue hatua za makusudi kuona kwamba pande mbili za Baraza (Madiwani na Watendaji) zinashirikiana ili kuleta tija iliyokusudiwa.

v. Usimamizi wa fedha katika uwekaji wa mabango uimarishwe.

HADIDU REJEA YA PILI:

KUCHUNGUZA TARATIBU ZA UIDHINISHAJI WA MATUMIZI NA UUZAJI WA MALI ZA BARAZA LA MANISPAA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilitakiwa kuchunguza taratibu zinazotumiwa na Baraza la Manispaa wakati wa kuidhinisha matumizi pamoja na kuuza mali zake.

Katika kufanikisha hili, Kamati iliwahoji Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Zanzibar, Madiwani, baadhi ya watendaji wa Baraza la Manispaa, Mkurugenzi wa Baraza, wafanyabiashara mbali mbali na wateja wa Baraza.

Baada ya utangulizi huo, ni vyema sasa tukapata ufafanuzi wa Hadidu Rejea hii kama ifuatavyo:-

Uchambuzi wa Hadidu Rejea husika:-

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeigawa hadidu rejea hii katika sehemu tatu kutokana na uasili wake sambamba na kueleweka vyema kama ifuatavyo:-

1. Kuchunguza taratibu za kupitisha bajeti ya mwaka ya Baraza la Manispaa,
2. Kuchunguza taratibu za uidhinishaji wa matumizi,
3. Kuchunguza taratibu za uidhinishaji wa manunuzi na
4. Kuchunguza taratibu za uuzaji na ukodishwaji wa mali ya Baraza la Manispaa.

Kuchunguza taratibu za kupitisha bajeti ya mwaka ya Baraza la Manispaa:

Mhe. Mwenyekiti, baada ya Baraza la Manispaa kupitisha makisio ya mapato na matumizi ya kila mwaka, jambo hili husaidia ugawaji wa mali za Baraza na kipimo cha utawala au udhibiti wa mali hizo.
Kamati moja kwa moja ilihoji taratibu zinazotumiwa na Baraza la Manispaa wakati wa kupitisha bajeti yao ya mwaka. Katika kupata ufafanuzi wa kipengele hiki Kamati ilikutana na Madiwani ambao waliieleza Kamati kwamba kabla ya makisio kuwasilishwa mbele ya Baraza Zima kila Kamati ya kisekta huandaa makisio ya bajeti yake na baadae huyawasilisha mbele ya Kamati ya Fedha na Uchumi na hatimaye huwasilishwa mbele ya Baraza Zima kwa kuidhinishwa. Maelezo haya yamethibitishwa na Kanuni ya 66 ya Kanuni za Baraza la Manispaa.
Kamati ilihitaji kupata maelezo zaidi kuhusiana na kadhia hii na katika kufanikisha hili ilikutana pia na baadhi ya watendaji wa Baraza la Manispaa ambao maelezo yao hayakupingana na yale ya Madiwani.

Yaliyobainika na Kamati kufuatia Uchunguzi wa suala hili:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati hii imeridhika kwamba taratibu za kupitisha bajeti ya mwaka ya Baraza la Manispaa inafuata matakwa ya Kanuni za Baraza.

Kuchunguza taratibu za uidhinishaji wa Matumizi:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilihoji taratibu zinazotumiwa na Baraza la Manispaa wakati wa kuidhinisha matumizi yanayofanywa. Katika kutoa ufafanuzi wao kuhusiana na kipengele hiki, Madiwani waliieleza Kamati kwamba katika Baraza la Manispaa hakuna uwazi kwenye suala la matumizi, jambo ambalo hupelekea mgongano baina ya Madiwani na Watendaji wa Baraza endapo Madiwani watahoji suala lolote. Kutokana na hilo watendaji wa Baraza hili huwadharau Madiwani na kujiona wao kuwa juu zaidi (*superior*).

Kamati ilielezwa pia kwamba baadhi ya mambo huamuliwa na Kamati pekee, jambo hili hupelekea baadhi ya Madiwani kukosa taarifa na kuonekana kuwa hawafuatilii ipasavyo shughuli za Baraza.

Vile vile, tulielezwa kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 23 cha Sheria Namba 3 ya 1995 kuna ulazima wa kuundwa Kamati Maalum ya Kuratibu na Kudhibiti Matumizi ya Baraza la Manispaa.

Jambo la kusikitisha hadi tunapokea taarifa hii Baraza limeshindwa kuunda Kamati hii ingawa Madiwani wameithibitishia Kamati kwamba wamekuwa wakidai kutekelezwa sharti hili kila mwaka bila ya mafanikio. Kukosekana kwa chombo hiki kunapelekea kila Kamati ya kisekta ya Baraza kufanya matumizi yake kama inavyoona inafaa.
Kwa kuwa Mstahiki Meya ndio msimamizi Mkuu wa Baraza la Manispaa, Kamati ilimtaka atoe maelezo kuhusiana na hoja hiyo nae alieleza kwamba, Kamati hiyo haijaanzishwa kwa kuwa hapo kabla hapakuwa na Mkaguzi wa Ndani pamoja na Mwanasheria. Kwa kuwa watendaji hao hivi sasa wapo Mstahiki Meya aliahidi kuwa wakati wowote ataiunda Kamati hiyo.

Kamati haikuridhishwa na kauli hiyo, kimsingi Kamati Maalum ya kuratibu na kudhibiti matumizi huundwa na Madiwani pekee na haiwajumuishi watendaji hawa.
Sambamba na hayo Kamati ilielezwa kwamba, Baraza hufanya baadhi ya matumizi bila ya kuwa na bajeti ya jambo husika na wala haijawahi kuwasilishwa katika Baraza nyongeza ya makisio kama Kanuni ya 68 ya Kanuni za Baraza la Manispaa inavyoelekeza.

Kutokana na kauli hiyo Kamati ilitaka kutajiwa mfano wa matumizi ya ziada yaliyofanywa na Baraza la Manispaa wakati kulikuwa hakuna bajeti ya jambo husika. Katika kufafanua hili, Madiwani kwa pamoja waliieleza Kamati kuwa Ujenzi wa Bwawa la Michenzani uliogharimu takriban shilingi 19, 000,000/= haukuwa na bajeti na ulijengwa kwa fedha za Baraza kwa shindikizo la Serikali wakati wao kama Wahusika Wakuu wa ujenzi huo waliukataa kwa kuwa haukuwa na bajeti.

Jambo la kushangaza ujenzi huo ulifanywa bila ya ridhaa ya Madiwani na hadi leo hii wanashindwa kujua matumizi ya ujenzi huo fedha zake zilitoka katika kifungu gani cha Baraza.

Ili kupata uchambuzi wa kina katika hadidu rejea hii Kamati pia ilikutana na baadhi ya watendaji wa Baraza la Manispaa na waliieleza Kamati, kwamba kabla ya matumizi kufanywa Kamati husika ya kisekta hukutana na kuidhinisha matumizi husika.

Kutokana na maelezo ya Watendaji Kamati hii ilibaini kuwa kuna njia nne za kuomba matumizi ya fedha katika Baraza la Manispaa. Njia zenyewe ni kama zifuatazo:-

1. Baada ya Kamati kuridhia matumizi hayo, Mkuu wa Idara humuandikia barua ya kuidhinisha matumizi Afisa Utawala ambaye huyapitia tena matumizi hayo na akiridhika nayo humuandikia barua Mkurugenzi wa Baraza, kwa ajili ya kuidhinisha malipo hayo na baada ya hapo Mkurugenzi humuandikia Mhasibu kwa hatua ya kufanya malipo. Endapo Afisa Utawala hakuridhika na maombi hayo basi huyarejesha kwa wahusika, ili wayapitie upya na kufanya marekebisho.

2. Baada ya Kamati kuridhia matumizi hayo na endapo Mkuu wa Idara husika hayupo Afisa Utawala huomba matumizi hayo kwa Mkurugenzi kwa niaba ya Idara husika na baadae Mkurugenzi humtaka Mhasibu kuchukua hatua husika.

3. Baada ya Kamati kuridhia matumizi hayo Mkuu wa Idara husika humuomba kwa mdomo Afisa Utawala ambaye huomba matumizi hayo kwa Mkurugenzi kwa maandishi kwa niaba ya Idara husika na baadae Mkurugenzi humtaka Mhasibu kuchukua hatua husika.

4. Baada ya Kamati kuridhia matumizi hayo Mkuu wa Idara humuandikia barua ya kuidhinisha matumizi Mkurugenzi, na baadae Mkurugenzi humuandikia dondoo Mhasibu, ili achukue hatua zinazohusika, na nakala ya barua hiyo hutumwa kwa Afisa Utawala.

Mhe. Mwenyekiti, ingawa watendaji wa Baraza walizitaja njia hizo. Hata hivyo, Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa hakukubaliana nazo na alieleza kwamba, matumizi katika Baraza hufanyika baada ya Kamati husika kuridhia matumizi hayo na Mkuu wa Idara humuandikia moja kwa moja Mkurugenzi barua ya kuidhinisha matumizi na baadae Mkurugenzi humuandikia dondoo Afisa Utawala, ili ajue kinachoendelea ndani ya Baraza kwa kuwa ndiye Mkuu wa Utawala pamoja na Mhasibu ili achukue hatua za malipo.

Sambamba na hayo, Ndugu Eshe Abdalla Juma ambaye ni Kaimu Mhasibu Mkuu wa Baraza la Manispaa aliieleza Kamati kwamba baadhi ya wakati hufanya matumizi mbali mbali kutokana na maelekezo ya Mkurugenzi wa Baraza.

Kutokana na kauli yake hiyo Wajumbe wa Kamati walimuomba aeleze baadhi ya malipo aliyoyafanya kwa njia hiyo. Alieleza kwamba aliwahi kumlipa Ndugu Ali Abdalla Ali (Kibasi) kwa ujenzi wa Bustani ya Donge, Darajani pamoja na kulipa baadhi ya gharama za ujenzi wa Bwawa la Michenzani; zikiwemo ununuzi wa vifaa vya umeme, mabomba ya maji, pampu za maji na vifaa vyenginevyo.

Yaliyobainika na Kamati katika kuchunguza suala hili:

Mhe. Mwenyekiti, baada ya uchunguzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

1. Katika Baraza la Manispaa hakuna utaratibu maalum unaotumika wakati wa kuidhinisha matumizi, jambo ambalo ni kinyume na taratibu za fedha kwani kuna taratibu nne katika Baraza la Manispaa kama zinavyoonekana kwenye ukurasa wa 18 na 19 wa ripoti hii.

2. Hakuna matumizi yoyote yanayofanywa bila ya kushirikishwa Afisa Utawala (kiuhalisia ni Mkuu wa Idara ya Utawala na Sheria) ambaye ana hadhi sawa na Wakuu wengine wa Idara kwa mujibu wa vifungu vya 51, 52 na 53 vya Sheria ya Baraza la Manispaa Zanzibar Namba 3 ya 1995.

   Hali hii inaonesha kwamba Afisa Utawala ndiye mwenye uwezo (*power*) kuliko mtu yeyote katika kuidhinisha matumizi ya Baraza la Manispaa, Sheria na Kanuni za Baraza Sehemu ya Nne na ya Sita hazimtambui afisa huyu katika masuala ya matumizi.

3. Kutoundwa kwa Kamati ya Kudumu ya Kuratibu na Kudhibiti Masuala ya Fedha ndani ya Baraza la Manispaa, jambo ambalo ni matakwa ya sheria Namba 3 ya 1995 limekuwa ni jambo la kawaida kwa miaka mingi. Hivyo, hupelekea kutumika fedha za wananchi kinyume na masharti ya sheria.

4. Maamuzi ya matumizi ya fedha na maamuzi mengine yanayotolewa na Kamati za Kudumu za Baraza la Manispaa hayawasilishwi mbele ya Baraza Zima.

Kwa msingi huo Kamati inapendekeza mambo yafuatayo:-

1. Kuwe na utaratibu maalum unaofuatwa wakati wa kuomba na kuidhinishwa matumizi.

2. Afisa Utawala awe na hadhi sawa na Wakuu wengine wa Idara.

3. Kwa kuwa Kamati za Kudumu hushughulikia zaidi masuala ya kisekta ni vyema maamuzi yanayotolewa na Kamati hizi yawasilishwe mbele ya Baraza Zima, ili kutekeleza dhana ya uwajibikaji wa pamoja na utawala bora.

4. Shughuli ya Utawala na Utumishi ziendelee kuwa chini ya Mkurugenzi isipokuwa ateuliwe Afisa maalum wa kumsaidia Mkurugenzi katika masuala hayo. Afisa huyo atakuwa Msaidizi wa Mkurugenzi lakini asiwe na mamlaka sawa au zaidi ya Wakuu wa Idara waliotajwa ndani ya Sheria.

   Hivyo, muundo wa Idara uende sawa na muundo wa Kamati. Kwa msingi huo, kifungu cha 51 cha Sheria Namba 3 ya 1995 kionekane kama kilivyotajwa kwenye kifungu cha 49(1) (c) cha Sheria hii.

5. Kuwepo na kanuni inayokidhi matakwa ya kifungu cha 23 cha Sheria Namba 3 ya 1995 kuhusu kuundwa Kamati ya Kudumu ya Kuratibu na Kuthibiti Masuala ya Fedha.

Kuchunguza taratibu za manunuzi:

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa lina haki ya kufanya manunuzi kama taasisi nyengine. Kamati ilitaka kujua namna Baraza linavyofanya manunuzi.

Katika kufuatilia hili, Kamati iliwahoji watendaji wa Baraza ambao walieleza kwamba katika Baraza la Manispaa masuala ya manunuzi yanafanywa na Mkurugenzi, Mwangalizi wa Ofisi, Mkuu wa Utawala pamoja na Mhasibu. Kauli hii inathibitishwa na barua ya tarehe 9 Julai, 2010, tafadhali angalia Dondoo la Mkurugenzi la tarehe 16 Julai, 2010.

Ingawa Baraza lilipata Afisa anayehusika na manunuzi kwa takriban mwaka mmoja sasa, afisa huyo hutumiwa na viongozi wa Baraza baada ya kubaini kuwa wamefanya makosa katika manunuzi husika. Hivyo, afisa huyo

hutumika kwa lengo la kuziba pengo lililobainika. Baadhi ya vitu vilivyonunuliwa na Baraza kwa kufuata mfumo huo ni pamoja na ununuzi wa vipuri vya kijiko, kigari cha kubebea mizigo '*carry'* na vifaa vyenginevyo.

Yaliyobainika na Mapendekezo ya Kamati kufuatia Uchunguzi wa suala hili:

1. Watendaji wa Baraza la Manispaa wakiongozwa na Mkurugenzi hufanya manunuzi kwa kuwatumia watu, jambo ambalo linaleta hisia kuwa na maslahi binafsi.

2. Takriban shughuli nyingi za manunuzi katika Baraza la Manispaa hufanywa bila ya kutolewa zabuni kwa yale manunuzi yanayohitaji kufanyiwa hivyo kama ilivyoelezwa na kanuni ya 55, 56 na 57. Sharti la kutangaza zabuni pia linamfunga Mkurugenzi kwa mujibu wa kifungu cha 11(2) cha Sheria Namba 3 ya 1995 kinachomtaka azingatie Sheria nyengine zote za nchi, ambapo akiwa Afisa muwajibikaji Mkuu wa masuala ya fedha anapaswa kuzingatia Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Umma Namba 9 ya 2005.

3. Afisa Manunuzi hutumiwa baada ya manunuzi kufanyika.

Kamati inapendekeza yafuatayo:-

1. Afisa Manunuzi ashirikishwe wakati wa manunuzi na asitumike kuziba mianya ya ukiukwaji wa sheria.

2. Baraza la Manispaa lifuate masharti ya Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali na Kanuni zake, Sheria ya Baraza la Manispaa na Kanuni za Kudumu za Baraza la Manispaa wakati wa manunuzi na uuzaji wa mali zake.

Kuchunguza Taratibu za Uuzaji na Ukodishwaji wa Mali za Baraza la Manispaa:

Kamati imejiridhisha kwamba Baraza la Manispaa linamiliki mali mbali mbali. Miongoni mwa mali hizo ni Soko la Mwanakwerekwe, Soko la Darajani, Soko la Mikunguni, Soko la Saateni, *Diplomatic Supermarket*, Gari, Bustani, Vyoo, Gereji, na nyenginezo. Kamati ilihitaji kujua taratibu zinazotumiwa na Baraza la Manispaa katika kuuza mali zake hizo.

SOKO LA MWANAKWEREKWE:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara katika Soko la Mwanakwerekwe tarehe 07/06/2012, ili kuona hali halisi ya mambo yanayolalamikiwa pamoja na kuwaomba baadhi ya wafanyabiashara wa soko hilo kutoa maelezo yao kuhusiana na kile wanachokifahamu siku ya tarehe 09/06/2012 katika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi huko Mbweni. Hii ni kutokana na kuwa katika Soko hili kuna mali mbali mbali ambazo Baraza hujipatia mapato yake.

Miongoni mwa mali hizo ni kama zifuatazo:-

UKODISHWAJI WA VIBARAZA:

Mhe. Mwenyekiti, katika kupata ufafanuzi wa suala hili Kamati ilielezwa na Wafanyabiashara kwamba kabla ya kujengwa vibaraza walikuwa wanapanga biashara zao chini. Katika kulinda afya za watumiaji Baraza la Manispaa likawaagiza kupanga biashara zao katika meza na hatimae likaja wazo la kujengwa vibaraza.

Utaratibu wa Ujenzi wa Vibaraza:

Kamati ilitaka kujua utaratibu uliotumika wakati wa ujenzi wa vibaraza vya soko hilo. Katika kupata ufafanuzi wa kipengele hiki wafanyabiashara wa Soko la Mwanakwerekwe waliieleza Kamati hii kwamba, vibaraza vya soko hilo vilijengwa na Ndugu Khamis Ali Khamis lakini hawajui kaipata vipi kazi hiyo. Hapo awali walidhani kuwa ni mfanyakazi wa Baraza la Manispaa kwa kuwa takriban shughuli nyingi za Baraza hufanywa na yeye.

Lakini baadae waligundua kuwa Ndugu Khamis Ali Khamis ni mkandarasi anayejitegemea ila ni mtu wa karibu na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa. Kwa mujibu wa ujenzi wa vibaraza vilivyojengwa imekuwa ni vigumu kwa Kamati kujua idadi halisi ya vibaraza hivyo. Hata hivyo, Kamati imefanikiwa kuviona vibaraza 604.

Pamoja na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kudai kwamba utaratibu wa ujenzi wa vibaraza hivyo ulifuata mfumo wa *Build Operate Transfer (BOT)*. Kamati imegundua kwamba mkandarasi aliyetajwa hakutumia fedha zake katika ujenzi huo na badala yake Baraza kwa kushirikiana na mkandarasi huyo liliwataka wafanyabiashara waliokuwa wanatumia maeneo hayo kugharamia ujenzi wa vibaraza hivyo.

Kwa maelezo kuwa nje hakuruhusiwi mfanyabiashara yoyote kuuza bidhaa. Hata hivyo, hadi wanatoa taarifa hizi bado baadhi ya wafanyabiashara wanauza bidhaa zao nje ya soko hilo, ingawa mara kwa mara walikuwa wanalilalamikia suala hili kwa Mkuu wa Soko kwa kuwa asilimia kubwa ya wananchi hununua bidhaa zao nje ya soko (pembezoni mwa barabara) kwa kuwa zinauzwa bei nafuu, sambamba na kuepuka msongamano wa watu. Jambo hilo linawazoroteshea biashara zao wenye vibaraza na hubaki kufanyabiashara bila ya faida wala tija inayokusudiwa.

Wafanyabiashara hao walitueleza kuwa ili mfanyabiashara aweze kupewa kibaraza alitakiwa na Baraza la Manispaa kulipa shilingi 500,000/= fedha ambazo walimkabidhi Mkuu wa Soko hilo Ndugu Khamis Moh'd. Kati ya fedha hizo shilingi 100,000/= ziliingia katika mapato ya Baraza na shilingi 400,000/= alipewa mjenzi.

Ingawa Mkataba ulieleza kuwa wanalazimika kulipa fedha zote kwa pamoja, hata hivyo, hakukuwa na utaratibu maalum wa kulipa fedha hizo isipokuwa kila mfanyabiashara alikuwa analipa kutokana na uwezo wake (yaani wengine walilipa fedha zote shilingi 500,000/= kwa pamoja na wengine walilipa kidogo kidogo), na kwa wale walioshindwa kulipa fedha vibaraza vyao walipewa watu wengine.

Pia, walitueleza kuwa ingawa walitakiwa kulipa kiasi hicho cha fedha lakini kiuhalisia vibaraza hivyo vinagharimu chini ya kiwango hicho cha fedha na kwa kukisia kinaweza kugharimu shilingi 300,000/=.

Sambamba na hayo walitueleza kuwa hadi hivi sasa hawajui kama wanavimiliki vibaraza hivyo au wamekodishwa kwani kwa kawaida mtu akigharamia kitu au jambo linakuwa mali yake. Lakini kinachowashangaza wafanyabishara hao ni kuwa wamegharamia ujenzi wa vibaraza hivyo na hawavimiliki, kwa kuwa wamepewa kuvitumia kwa muda usiozidi miaka miwili.

Baada ya kumalizika miaka miwili wafanyabiashara hao walitakiwa na Baraza la Manispaa kulipa shilingi 100,000/= kama ni malipo ya ukodishwaji kwa muda wa mwaka mmoja. Kwa kuwa Kamati Teule ilikuwa inaendelea na uchunguzi wa eneo hilo ilimuomba Mhe. Waziri wa Wizara husika kusitisha zoezi hilo hadi hapo Kamati hii itakapomaliza shughuli hiyo na Baraza la Wawakilishi kutoa maelekezo yake.

Kamati haikutosheka na maelezo ya wafanyabiashara hao na katika kujiridhisha zaidi ilibahatika kuonana na Mkandarasi wa vibaraza hivyo Ndugu Khamis Ali Khamis, ambae aliieleza Kamati kwamba alitumia shilingi 180, 000,000/= katika ujenzi wa Mabanda na Vibaraza lakini Mkurugenzi aliona gharama hiyo ni kubwa na alimtaka Mkandarasi apunguze hadi shilingi 150, 000,000/=. Mkandarasi hakukubaliana na wazo hilo la Mkurugenzi kwa kuwa gharama hiyo ni ndogo ukilinganisha na ile aliyotumia na hatimae walikubaliana kwa shilingi. 166, 800,000/=.

Aliendelea kuieleza Kamati kwamba yeye hana mkataba na wakodishwaji wa vibaraza hivyo, isipokuwa alikuwa na mkataba na Baraza la Manispaa ambao kwa hivi sasa muda wake umekwisha, hivyo vibaraza kwa hivi sasa viko mikononi mwa Baraza. Baraza ilivikodisha vibaraza hivyo kwa shilingi 500,000/= kati ya fedha hizo shilingi 400,000/= alikuwa analipwa yeye na shilingi 100,000/= zilikuwa zinaingia katika mapato ya Baraza.

Kamati ilimtaka mkandarasi athibitishe kama ni kweli vibaraza hivyo vinagharimu kiasi hicho cha fedha au laa? Katika kujibu swali hilo alieleza kwamba kibaraza pekee hakigharimu kiasi hicho, isipokuwa kabla ya ujenzi wa kibaraza alianza na kazi ya kuweka sawa eneo hilo pamoja na kujenga paa. Mambo hayo mawili ndiyo yaliyochangia kibaraza kugharimu kiasi hicho cha fedha.

Sambamba na hayo, alieleza kwamba kuna baadhi ya watu wamelipa shilingi 100,000/= tu kati ya shilingi 500,000/=. Kwa kuwa muda wa kukodisha vibaraza hivyo umemalizika na baadhi ya wafanyabiashara wameshindwa kulipa fedha hizo aliliomba Baraza kumuachia vibaraza vile ili viwe mali yake.

Kamati ilimhoji Mkurugenzi wa Baraza kuhusiana na hili naye kwa upande wake alieleza kwamba hakuna mfanyabiashara hata mmoja aliyetozwa fedha kabla ya kukamilika kwa ujenzi wa vibaraza. Aliendelea kwa kueleza kuwa, hakuna mfanyabiashara aliyelipa fedha na asipewe kibaraza, na kwa kutilia mkazo suala hili alieleza kwamba wapo baadhi ya wafanyabiashara ambao hawakulipa fedha na wamepewa vibaraza.

UTUMIAJI WA MEZA:

Mhe. Mwenyekiti, katika kupata ufafanuzi wa suala hili Kamati ilielezwa na wafanyabiashara kwamba kabla ya kutumia meza walikuwa wanapanga biashara zao chini. Lakini katika kulinda afya za watumiaji Baraza la Manispaa likawaagiza kupanga biashara zao katika meza.

Utaratibu uliotumika wa Kutengeneza Meza:

Kamati ilitaka kujua utaratibu uliotumika wakati wa kutengenezwa meza za mbao za soko hilo. Katika kupata ufafanuzi wa suala hili wafanyabiashara wa Soko la Mwanakwerekwe waliieleza Kamati hii kwamba, Baraza la Manispaa lilitoa rai mbili kuhusu kutengezwa meza. Rai zenyewe ni kama zifuatazo:-

- Baraza la Manispaa kwa kutumia mafundi wake na kwa kutumia gharama zake litengeneze meza za mbao kwa thamani ya shilingi 400,000/= na mfanyabiashara atumie meza hiyo kwa kuuzia bidhaa zake kwa muda wa miaka miwili; au

- Mfanyabiashara ajenge meza za mbao kwa gharama zake na ailipe Baraza la Manispaa shilingi 350,000/= gharama za ujenzi na atumie eneo aloweka meza yake kwa muda wa miaka miwili.

Kwa kuwa meza ya kawaida ya mbao haifiki thamani ya shilingi 400,000/= wafanyabiashara waliamua kutengeneza meza kwa gharama zao (yaani waliikubali rai Namba 2) ijapokuwa walitakiwa kulipa shilingi 350,000/= kama ni gharama ya ujenzi wakati meza wamejigharamia wenyewe.

Kutokana na hali ilivyo wafanyabiashara hao wanashindwa kuelewa fedha walizolipa ni za kitu gani, ingawa stakabadhi zinaonesha kuwa ni malipo ya gharama za ujenzi lakini wanafikiria kuwa ni gharama ya matumizi ya eneo (ardhi) ambalo wameweka meza hizo.

Malipo mbali mbali yaliyofanywa na yanayofanywa na Wafanyabiashara wanaotumia Vibaraza na Meza katika Soko la Mwanakwerekwe:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilitaka kujua kama kuna malipo ya ziada waliyotoa au wanayotoa wafanyabiashara hao baada ya kulipa shilingi 500,000/= kwa wenye vibaraza na shilingi 350,000/= kwa wenye meza.

Katika kufuatilia hili Kamati ilielezwa na wafanyabiashara hao kwamba, wanalipa shilingi 1,000/= kwa siku sawa na shilingi 30,000/= kwa mwezi ambayo ni ada ya usafi. Aidha, walitueleza kwamba ingawa wanalipa fedha hiyo kwa ajili ya kupatiwa huduma hiyo, lakini bado usafi wanafanya wenyewe kwa kuwa taka zinazagaa katika maeneo yao na Baraza la Manispaa halitoi huduma hiyo ipasavyo.

Sambamba na hayo, tulielezwa kwamba walitakiwa kulipa shilingi 10,000/= kwa yule mfanyabiashara ambaye atahitaji kupatiwa nakala ya mkataba. Kwa kuwa kiwango cha fedha ni kikubwa, asilimia kubwa ya wafanyabiashara walikataa kupewa nakala hiyo.

Baadhi ya mambo muhimu yanayojitokeza katika utekelezwaji wa Mkataba:

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na ukweli wa kuwepo mikataba kwa wafanyabiashara wanaouza bidhaa katika vibaraza na wale wanaouza kwenye meza na Baraza la Manispaa, Kamati imebaini kuwa mikataba hiyo ina mapungufu kadhaa. Miongoni mwa mapungufu hayo ni kama yafuatayo:-

- Baadhi ya vipengele havikujazwa.
- Mikataba imesainiwa bila ya kufuatwa matakwa ya kifungu cha 20(2) cha Sheria Namba 3 ya 1995, ambacho kinahitaji uwepo au ushuhuda wa Mstahiki Meya au Naibu Meya na Mkurugenzi au Afisa mwengine wa Baraza.
- Kwa mujibu wa Mkataba wafanyabiashara walitakiwa kulipa fedha zote shilingi 500,000/= kwa pamoja lakini waliieleza Kamati kuwa walilipa kutokana na uwezo wao.
- Mikataba imewekwa muhuri wa Mkurugenzi badala ya muhuri wa Baraza la Manispaa.

Yaliyobainika katika Kuchunguza suala hili:

Baada ya uchunguzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo:

1. Kazi ya ujenzi wa vibaraza na meza ilitolewa bila ya kutangazwa zabuni, jambo ambalo ni kinyume na kanuni ya 55(b) ya Kanuni za Baraza la Manispaa pamoja na Sheria ya Mauziano na Uuzaji wa Mali za Umma, Namba 9 ya 2005.

2. Ingawa wafanyabiashara walilipa asilimia 80 ya fedha zote walizotakiwa kulipa (shilingi 400,000/= kati ya shilingi 500,000/=) kwa mkandarasi, jambo la kustaajabisha ni kwamba walitakiwa kufunga mkataba na Baraza la Manispaa badala ya mkandarasi huyo.

3. Kamati ina wasiwasi juu wa thamani halisi (*value for money*) ya ujenzi wa vibaraza na meza.

4. Ingawa Mkurugenzi na Mkandarasi walieleza kuwa Wakodishwaji wa vibaraza na meza wamelipa baada ya vibaraza na meza kujengwa, Kamati imebaini kuwa kauli hizo sio sahihi na badala yake kauli za wakodishwa ndio zenye ukweli. Tunatamka hivyo, baada ya kuangalia tarehe zilizotolewa risiti na tarehe ya kufungwa mikataba.

5. Kutokana na kasoro mbali mbali zilizojitokeza kwenye mikataba inadhihirisha wazi kuwa watendaji wa Baraza la Manispaa wakiongozwa na Mkurugenzi hawapo makini wakati wa kufunga mikataba.

6. Sio kweli kwamba mkandarasi alipeleka barua ya kuomba kupewa vibaraza kwa wale wafanyabiashara walioshindwa kulipa fedha.

Hatua za kuchukuliwa na maoni ya Kamati:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inapendekeza hatua zifuatazo kuchukuliwa:-

1. Kwa kuwa Mkurugenzi amemruhusu mjenzi kujenga bila ya kufuata taratibu za kisheria, Kamati inapendekeza kwamba Mkurugenzi achukuliwe hatua za kinidhamu.

2. Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa na Ndugu Khamis Ali Khamis (mjenzi wa vibaraza) wachukuliwe hatua za kisheria kwa kutoa ushahidi wa uongo mbele ya Kamati hii kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha Sheria Namba 4 ya 2007.

3. Kutokana na makosa yaliyobainika kuhusiana na mikataba, Kamati inapendekeza Mkurugenzi na watumishi wa Baraza waliohusika wachukuliwe hatua za kisheria. Aidha, Kamati inawashauri viongozi wa Baraza kuwa makini wakati wa kufunga mikataba ili kulinda uhalali wa mikataba hiyo.

UJENZI WA MADUKA:

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tuendelee kumsikiliza Mhe. Mwenyekiti ili aweze kumaliza haraka. Tuendelee.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Baraza la Manispaa): Mhe. Mwenyekiti, katika kupata ufafanuzi wa suala hili Kamati ilielezwa na wafanyabiashara, kwamba ujenzi wa Maduka ya Soko la Mwanakwerekwe umegawika katika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

1. Maduka 20 yaliyojengwa na baadhi ya Madiwa ambayo yamewekwa alama ya Px.

2. Maduka 22 yaliyojengwa na Mkandarasi ambayo yamewekwa alama ya PxB.

Utaratibu wa Ujenzi wa Maduka 20:

Kamati ilitaka kujua utaratibu uliotumika wakati wa ujenzi wa maduka 20 maarufu kama maduka ya Madiwani. Katika kupata ufafanuzi wa suala hili tulielezwa kwamba, wakati ndugu Mzee Khamis Juma anakaimu nafasi ya Ukurugenzi wa Baraza, baadhi ya Madiwani waliomaliza muda wao katika mwaka 2010 walivamia Soko la Mwanakwerekwe na kujipatia viwanja na hatimae kujengwa maduka 20.

Kwa msingi huo, viwanja hivyo viligaiwa bila ya kulishirikisha Baraza la Manispaa, hii ni kutokana na kuwa maduka hayo ishirini yalijengwa kama ni kianzio cha maisha kwa baadhi ya Madiwani hao.

Ingawa Baraza la Manispaa halikushirikishwa wakati Madiwani wanajigawia viwanja Sokoni hapo. Hata hivyo, Baraza hilo lilisimamia ujenzi wa maduka hayo.

Pamoja na hayo tulielezwa kuwa licha ya Madiwani kujichukulia maeneo katika soko hilo, pia walijipa jukumu la kutafuta wakodishwaji wa maduka hayo.

Yaliyobainika na Kamati katika kuchunguza hili:

Kamati ilibaini baadhi ya mambo kama ifuatavyo:-

1. Kuna ukiukwaji mkubwa wa maadili ya kazi na utumiaji mbaya wa madaraka. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya Madiwani hutumia madaraka yao kwa maslahi yao binafsi, jambo hili limechangia kuwa na migogoro ndani ya Baraza.

2. Baraza la Manispaa linahalalisha mambo kwa maslahi ya watu binafsi.

3. Baadhi ya Madiwani huzitumia Kamati za Kudumu za Baraza la Manispaa kuwa ni vitega uchumi vyao.

4. Kitendo cha Madiwani kutafuta wateja wa kukodi maduka hayo kinaashiria kuwa Madiwani huchangia kwa asilimia kubwa ukiukwaji wa sheria kwa maslahi yao binafsi.

Kuhusu Ukodishwaji wa Maduka 20:

Katika kupata ufafanuzi wa suala hili Kamati ilielezwa na wafanyabiashara wanaotumia maduka hayo, kwamba walitakiwa kupeleka barua ya maombi ya kukodishwa maduka hayo Baraza la Manispaa mnamo mwaka 2009.

Walitakiwa na aliyekuwa Mkuu wa Soko ndugu Mcha na Kamati iliyokuwa inafuatilia kadhia hii kuandika shilingi 500,000/= katika barua hizo za maombi kama ni ada ya ukodishwaji wa mlango huo wa duka wakati malipo halisi waliyolipa ni shilingi 5, 000,000/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 1, 500,000/= zilitumika kwa ujenzi wa duka, shilingi 3, 000,000/= walipewa Madiwani waliovamia viwanja hivyo, na shilingi 500,000/= ziliingia katika mapato ya Baraza la Manispaa. Maduka hayo yalijengwa na wafanyabiashara wenyewe kwa gharama tulizozieleza hapo kabla.

Aidha, walieleza kuwa walikuwa wanalipa shilingi 1500/= kwa siku sawa na shilingi 45,000/= kwa mwezi. Baada ya kuteuliwa Mkurugenzi mpya ndugu Rashid Ali Juma walitakiwa kulipa shilingi 50,000/= za kodi na shilingi 40,000/= za ada ya usafi kwa mwezi, wakati hapo awali walikuwa wanalipa shilingi 6000/-.
Pamoja na kiwango kikubwa cha ada ya usafi wanacholipa bado shughuli za usafi zinafanywa na wafanyabiashara wenyewe. Pia, walieleza kwamba milango hiyo wanakodishwa kwa mwaka, na kwa yule mfanyabishara anakayehitaji kupatiwa nakala ya mkataba basi hutozwa shilingi 8000/= ya ada ya fomu na shilingi 30,000/= ya mkataba. Jambo hili lilipelekea wafanyabiashara wengi kushindwa kuwa na mkataba.

Baadhi ya mambo muhimu yanayojitokeza katika utekelezwaji wa Mkataba:

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na ukweli wa kuwepo mikataba kwa wafanyabiashara waliokodishwa milango ya maduka 20, Kamati imebaini kuwa mikataba hiyo ina mapungufu kadhaa. Miongoni mwa mapungufu hayo ni kama yafuatayo:-

- Kuna viwango viwili tofauti vilivyoandikwa vinavyohusu kodi ya mlango wa duka, yaani shilingi 400,000/= kwa mwezi kwenye maelezo ya jumla na shilingi 50,000/= kwenye kipengele cha (2).

- Kipengele cha (3) kimemtaka mkodishwaji kulipia ada ya huduma ya usafi ya shilingi 90,000/= kwa mwezi wakati hali halisi analipia shilingi 40,000/= kwa mwezi.

- Mikataba imefungwa tarehe 1 Januari, 2011, lakini inaonesha kushuhudiwa na Mwanasheria wa Baraza la Manispaa aliyeajiriwa mwishoni mwa mwaka huo.

- Mikataba imesainiwa bila ya kufuatwa matakwa ya kifungu cha 20(2) cha Sheria Namba 3 ya 1995, ambacho kinahitaji uwepo au ushuhuda ama wa Mstahiki Meya au Naibu Meya na Mkurugenzi au Afisa mwengine wa Baraza.

Hatua za Kuchukuliwa:

Kamati inapendekeza hatua zifuatazo kuchukuliwa:-

1. Kwa kuwa imebainika kuwa wapo baadhi ya Madiwani walijichukulia maeneo ya maduka na kuwakodisha wafanyabiashara kwa maslahi yao binafsi, Kamati inapendekeza kwamba Madiwani hao wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa makosa ya kujipatia fedha kinyume na sheria.

2. Ilivyokuwa mikataba imekiuka masharti ya kifungu cha 20(2) cha Sheria Namba 3 ya 1995, Kamati inapendekeza kufungwa upya mikataba hiyo kama ilivyoelekezwa na kifungu hicho.

3. Kutokana na makosa yaliyobainika kuhusiana na mikataba, Kamati inapendekeza watendaji wa Baraza waliohusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Utaratibu wa Ujenzi wa Maduka 22:

Mhe. Mwenyekiti, katika kufuatilia hili Kamati hii ilitaka kujua namna ujenzi wa maduka 22 ulivyokuwa. Katika kupata ufafanuzi wa suala hili, Kamati ilifanya mahojiano na mjenzi wa maduka hayo ndugu Khamis Ali Khamis ambaye alieleza kwamba; alipewa kazi ya ujenzi wa maduka hayo mwishoni mwa utawala wa Mkurugenzi Mabrouk Jabu.

Alizidi kutueleza kwamba alijenga maduka hayo bila ya zabuni, mara baada ya kuanza kazi ya ujenzi alifuatwa na watu mbali mbali wakidai kwamba wamepewa milango ya maduka hayo na wengine walithubutu hata kutoa maelekezo juu ya ujenzi wa maduka yale. Hata hivyo, ndugu Khamis aliendelea na ujenzi huo na kuwaeleza kwamba yeye kapewa kazi hiyo na Baraza, hivyo hatambui madai ya mtu yeyote.

Baada ya ujenzi huo kukamilika alipokea barua kutoka Baraza la Manispaa ya kutakiwa kujaza mkataba, wakati huo Ndugu Mzee alikuwa Kaimu Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa na alifanya hivyo.

Alizidi kueleza kuwa wakati anaendelea na ujenzi ndugu Rashid Ali Juma aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa. Baada ya kuona kazi nzuri aliyoifanya mkandarasi huyo alimuomba aweke zege katika Soko lote la Mwanakwerekwe, na yeye alilikubali ombi hilo na kuanza kazi ya uwekaji zege.

Kwa kuwa Baraza lilikuwa halina fedha za kutosha kwa wakati ule alitakiwa na Mkurugenzi kuunganisha gharama zake na alipewa mkataba mmoja uliojumuisha ujenzi wa maduka 22 na utiaji wa zege.

Ukodishwaji wa Maduka 22:

Katika kupata ufafanuzi wa suala hili Kamati ilielezwa na wafanyabiashara wanaotumia maduka hayo, kwamba walitakiwa na mkandarasi wa maduka hayo kulipa shilingi 12, 000,000/= kama ni ada ya ukodishwaji wa mlango huo kwa muda wa miaka 10. Isipokuwa wapo baadhi ya wafanyabiashara waliolipa shilingi 12, 500,000/= kwa muda huo huo. Hata hivyo, kutokana hali tofauti ya kifedha ya wafanyabiashara hao, walilazimika kukodishwa milango hiyo kutokana na uwezo wao wa kifedha na kwa jinsi utakavyopatana.

Kwa mnasaba huo, wapo wafanyabiashara waliokodishwa duka kwa muda wa miaka 10 na walilipa shilingi 12, 500,000/=, wengine walilipa shilingi 8, 000,000/= na wamekodishwa kwa miaka 7, wapo waliolipa shilingi 6, 000,000/= na wamekodishwa kwa miaka 9 na wengi wengineo.

Kwa kuwa mkandarasi huyo hakuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi huo, aliwaomba wafanyabiashara hao kulipa fedha kabla, ili aweze kutumia fedha hizo kwa madhumuni hayo, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu. Vile vile, tulielezwa kwamba asilimia kubwa ya wafanyabiashara hao hawakupewa risiti kwa zile fedha walizolipa wala mikataba ya kukodishwa mlango wa duka na mkandarasi ingawa mara kadhaa walikuwa wanamdai.

Baadhi ya mambo muhimu yaliyojitokeza katika utekelezwaji wa Mkataba:
Pamoja na kuwepo mikataba kwa baadhi ya wafanyabiashara waliokodishwa milango ya maduka 22, Kamati imebaini kuwa mikataba hiyo ina mapungufu kadhaa. Miongoni mwa mapungufu hayo ni kama yafuatayo:-

- Mikataba haina hadhi imefutwafutwa.

- Wakodishwaji walipewa mikataba ambayo ni nakala '*copy'* na sio halisi '*original'*, ingawa Mahakama huzizingatia pia nakala za nyaraka lakini nyaraka halisi zinakuwa na nguvu zaidi.

- Mkodishaji (Baraza la Manispaa) hakuwapatia risiti baadhi ya wakodishwaji baada ya kufanya malipo mbali mbali yakiwemo ya leseni. Kitendo hiki ni kinyume na kipengele nambari tatu cha Mkataba.

- Wakodishwaji wanalipishwa ada ya usafi kinyume na mkataba.

Malipo mbali mbali yaliyofanywa au yanayofanywa na Wafanyabiashara wanaotumia kati ya Maduka 22 katika Soko la Mwanakwerekwe:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilitaka kujua kama kuna malipo ya ziada wanayotoa wafanyabiashara hao, mbali ya fedha zilizoelezwa hapo kabla. Katika kufuatilia hili Kamati ilielezwa na wafanyabiashara hao kwamba, kila siku wanalipa ada ya usafi, ambapo; kwa wale wafanyabiashara wanaouza biashara zao ndani ya duka hulipa shilingi 1,000/= na kwa wale wanaouza biashara zao ndani na nje ya duka hulipa shilingi 2,000/=.

Pia, wanalipia ada ya ulinzi ambapo baadhi ya wafanyabiashara hulipa shilingi 200/- na wengine shilingi 300/=. Halikadhalika, wanalipia ada ya leseni, ambapo asilimia kubwa ya wafanyabiashara walitakiwa kulipa shilingi 100,000/=, lakini hulipa chini ya hapo endapo atakuwa mpatanaji mzuri.

Mambo yaliyobainika na Kamati katika kuchunguza hili:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilibaini baadhi ya mambo kama ifuatavyo:-

1. Kuna ukiukwaji mkubwa wa maadili ya kazi na utumiaji mbaya wa madaraka. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya Madiwani hutumia madaraka yao kwa maslahi yao binafsi, jambo hili linatia doa na kulipaka matope Baraza la Manispaa na kulishushia hadhi baraza hilo.

2. Kamati ya Kudumu ya Kazi za Ujenzi na Mazingira ya Baraza la Manispaa hutumiwa vibaya na Madiwani kama ni sehemu ya kujipatia maslahi yao.

3. Kitendo cha kuwatoza ada ya usafi wafanyabiashara wanaopanga biashara zao ndani na nje ya duka ni cha dhulma. Hii ni kutokana na kuwa ndani ya duka Baraza la Manispaa halitoi huduma hiyo.

Hatua za kuchukuliwa:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inapendekeza hatua zifuatazo kuchukuliwa:

1. Serikali ichukue hatua kwa wale wote waliobainika kutofuata Sheria na Kanuni za Baraza la Manispaa pamoja na sheria nyengine zinazohusiana na manunuzi.

2. Baraza liache kuwatoza mara mbili ada ya usafi wafanyabiashara wanaoweka biashara zao nje na ndani ya duka.
3. Kwa kuwa Kamati imegundua kuwa mikataba mingi iliyofungwa haikufuata taratibu za kisheria, hivyo Kamati inapendekeza Baraza la Manispaa lipitie upya mikataba yote iliyofungwa kipindi kilichopita, ili lijiridhishe na utaratibu uliotumika.

SOKO LA DARAJANI:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara katika Soko la Darajani tarehe 07/06/2012, ili kuona hali halisi ya mambo yanayolalamikiwa pamoja na kuwaomba baadhi ya wafanyabiashara wa soko hilo kutoa maelezo yao kuhusiana na kile wanachokifahamu.

Katika kupata ufafanuzi wa suala hili Kamati ilielezwa na wafanyabiashara kwamba ujenzi wa Maduka ya Soko la Darajani umegawika katika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

1. Ujenzi wa Maduka 13 na

2. Ujenzi wa Maduka 16

Utaratibu wa Ujenzi wa Maduka 13:

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa maduka haya ulifanyika baada ya kubomolewa kwa uzio na baadhi ya maduka ya wauza ndizi. Katika kufuatilia ujenzi huu Kamati ilikutana na wajenzi wa maduka haya siku ya tarehe 08/06/2012 katika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi huko Mbweni, kwa ajili kupata taarifa ya kina na yenye uhakika. Kamati ilizungumza na wajenzi wa maduka hayo ambao ni ndugu Rashid Khalfan Ali na ndugu Suleiman Msellem Nassor.

Katika kutoa taarifa zake ndugu Rashid alitueleza kwamba alifuatwa na ndugu Seif Zahran ambaye ni rafiki wa karibu wa ndugu Vuai Ame Vuai na kuelezwa suala la ujenzi wa maduka haya. Kwa kuwa ndugu Rashid anajishughulisha na masuala haya alikubali kujenga maduka hayo bila ya pingamizi yoyote. Kutokana na kukubali kwake huko ndugu Vuai alimkutanisha ndugu Rashid na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kama ni kumtambulisha.

Vile vile, alieleza kwamba ndugu Vuai ndio aliyekuwa anafuatilia masuala yote ya ujenzi, ikiwa ni pamoja na kupatikana kibali cha ujenzi kutoka Mamlaka ya Mji Mkongwe na wao walikuwa wanalipa gharama za fedha wanazoambiwa kulipa tu. Alikubaliana na Baraza kujenga maduka matatu, kati ya maduka hayo atakodishwa maduka mawili kwa muda wa miaka mitano ili afidie gharama zake alizotumia.

Amekodishwa maduka hayo kwa muda huo kwa kuwa walikubaliana na Baraza kujenga maduka hayo kwa gharama ya shilingi 4, 000,000/= na ametakiwa kulipa asilimia ishirini (20%) Baraza la Manispaa na asilimia thamanini

(80%) afidie gharama aliyotumia. Ama kwa upande wa duka moja lililosalia atalipwa fedha zake za ujenzi ndani ya miezi sita kwa vipindi vitatu.

Ndugu Rashid aliendelea kueleza kwamba kwa kuwa alikuwa hajaanza kulipwa gharama alizotumia za duka moja, alisita kulipa ile asilimia ishirini aliyotakiwa kuilipa Baraza hadi pale alipopewa barua na Baraza ya kumtaka alipe fedha hizo. Kutokana na barua hiyo aliamua kulipa shilingi. 880,000/= ikiwa ni malipo ya miaka miwili. Hata hivyo, alishindwa kulipa fedha hizo kwa kuwa aliambiwa ni vyema akaonana na Mkurugenzi na kwa siku ile hakuonana nae.

Kwa upande wa ndugu Suleiman Msellem Nassor alitueleza kwamba alifuatwa na dalali ndugu Othman na kumueleza kadhia hii na hatimaye alimkutanisha na ndugu Vuai. Alitueleza kwamba alikuwa mtu wa mwanzo kupewa taarifa ya ujenzi huo, na hapo awali ilikubalika kujengwa maduka matatu, lakini baada ya kuchelewa kuchukua hatua nafasi hiyo alipewa ndugu Rashid.

Baada ya hapo Baraza la Manispaa liliamua kuongeza kujengwa maduka kumi ambayo alikabidhiwa ndugu Suleiman na kufanya jumla ya maduka hayo kuwa kumi na tatu. Aliomba kujenga maduka hayo kwa gharama ya shilingi 50, 000,000/=. Hata hivyo, walikubaliana na Baraza kujenga kwa shilingi 40, 000,000/=, ambapo kila mlango utagharimu shilingi 4, 000,000/=.

Kama kawaida ilipatiwa mkataba wa ujenzi wa maduka hayo, isipokuwa, badala ya kupewa mkataba wa ujenzi wa maduka kumi alipewa mkataba unaoonesha kuwa atajenga maduka matatu. Baada ya kugundua kasoro hiyo, aliomba kupatiwa mkataba ambao anaufanyia kazi, yaani mkataba wa ujenzi wa maduka kumi lakini Baraza la Manispaa halikumpatia mkataba huo na lilimuomba aendelee na kazi na suala hilo litarekebishwa.

Ndugu Suleiman aliendelea kujenga maduka hayo bila ya mkataba na alipofika hatua ya uwekaji wa fremu za milango alisitisha ujenzi huo kwa takriban mwezi mmoja, kwa kuwa Baraza halijampa mkataba. Kutokana na uamuzi wake huo ndugu Vuai alimuomba aendelee na ujenzi huo na hatua zitachukuliwa. Kwa kuwa mjenzi huyo alitumia gharama zake nyingi aliendelea na zoezi hilo. Siku chache baadae alipata taarifa kwamba maduka hayo yanakodishwa.

Kutokana na taarifa hiyo alimtafuta Ndugu Vuai ili kupata maelezo zaidi na alimueleza kuwa, ni kweli maduka hayo yanakodishwa na Baraza la Manispaa, na yeye kama mjenzi atapewa maduka mawili ikiwa ni fidia ya gharama zake, jambo ambalo ni kinyume na makubaliano yao, kwani walikubaliana kuwa atapewa maduka sita ili kufidia gharama zake.

Ingawa ndugu Suleiman alilidai Baraza la Manispaa kumpatia mkataba wa ujenzi wa maduka kumi mara kadhaa. Hata hivyo, Baraza lilikataa kumpatia mkataba huo na hatimae lilimpatia mkataba ambao uko kinyume na makubaliano yao ya awali. Ndugu Suleiman aliamua kuukataa mkataba huo, hata hivyo, alilazimika kutia saini baada ya kuelezwa na ndugu Vuai kwamba endapo hatotia saini atanyang'anywa maduka hayo na kukodishwa watu wengine.

Aliendelea kutueleza kwamba baada ya Baraza kuamua kumpa maduka mawili alitaka kujua hatma ya fedha zake zilizosalia ambazo ni shilingi 38, 000,000/=. Ndugu Vuai alimtaka akachukue shilingi 10,000,000/= kama ni kianzio cha fidia ya gharama zake alizotumia, ingawa, baadae alijuulishwa kwamba fedha hizo zimeingia kimakosa kwenye akaunti ya ndugu Ramadhan Abdalla (Songa) ambaye kwa muda huo alikuwa Dar es Salaam.

Siku chache baadae aliambiwa tena na ndugu Vuai kuwa akachukue shilingi 20, 000,000/=, lakini majibu yalikuwa ni yale yale kwamba fedha zimeingia kimakosa kwenye akaunti ya ndugu Ramadhan Abdalla (Songa) na amekwenda Dubai kuzifanyia biashara. Kutokana na kauli hizo alimuomba Ndugu Vuai amkutanishe na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kwa kuwa ndiye aliyefunga naye mkataba. Ndugu Suleiman alikutana na Mkurugenzi lakini hakuweza kuzungumza nae kutokana na sababu mbali mbali.

Ndugu Suleiman alitueleza kuwa wakati wa ujenzi wa maduka hayo alitafuta watu mbali mbali wa kumkopesha fedha ili akamilishe kazi hiyo kwa wakati. Kwa kuwa mjenzi huyu alichelewa kulipa fedha anazodaiwa kama alivyojikubalisha, wadai hao walitaka kumshtaki mjenzi huyu kwa kuchelewa kwake huko. Miongoni mwa wadai hao ni pamoja na fundi wa milango ambaye alikuwa anadai shilingi 8, 000,000/=.

Hadi inatimia miaka miwili hakuna maelezo wala fedha zozote alizolipwa wakati aliahidiwa na Baraza kupitia kwa Ndugu Vuai kuwa fedha zake atalipwa katika awamu tatu, yaani kila baada ya miezi miwili atalipwa asilimia thelathini na tatu (33%). Kwa kuwa Mjenzi hakulipwa fidia ya ujenzi na Baraza alisitisha kufanya malipo ya asilimia ishirini (20%), isipokuwa amelipa fedha za usafi tu ambayo ni shilingi 9, 000,000/= kwa mwezi.

Ndugu Rashid Khalfan na Ndugu Suleiman kwa pamoja walitueleza kwamba ingawa wamekubali kila duka kugharimu shilingi 4, 000,000/=, hata hivyo maduka hayo yaligharimu zaidi ya kiwango hicho. Hii ni kutokana na kuwa maduka hayo yalijengwa kwa mujibu wa matakwa ya Baraza la Manispaa, jambo hilo lilipelekea mara kwa mara kubomolewa na kujengwa tena maduka hayo.

Aidha, walieleza kwamba mikataba yao (wajenzi) na wafanyabiashara wote waliokodishwa maduka hayo haina tofauti (yaani walitakiwa kulipa asilimia ishirini (20%) Baraza la Manispaa na asilimia thamanini (80%) wajilipe gharama zao za ujenzi) wakati wao hawakujenga chochote.

Walizidi kueleza kwamba hawana uhakika na bei halisi waliyokodishwa wenzao, hata hivyo, baadhi ya maduka yalikodishwa kati ya shilingi 7, 000,000/= na shilingi 15, 000,000/=. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya maduka yamepatikana kwa njia ya kilemba.

Pia, walieleza kwamba mkataba wa ujenzi wa maduka hayo walifunga na Baraza la Manispaa na sio *F & K Enterprises*. Hadi Kamati inaandaa taarifa hii Ndugu Rashid Khalfan Ali na Ndugu Suleiman Msellem Nassor wanalidai Baraza la Manispaa.

Kamati ilishindwa kupata mikataba ya wakodishwaji wengine wa maduka hayo kwa kuwa Baraza la Manispaa imeikusanya mikataba yote kwa lengo la kuifanyia marekebisho.

Kamati ilibahatika kuonana na Ndugu Vuai Ame Vuai ambae alieleza kwamba, chimbuko la kupewa kazi hiyo ni kutokana na ushauri wake alioutoa kwa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa la kujengwa majengo ya kudumu katika eneo hilo, ili kudhibiti uchafu ambao mara kwa mara Kampuni ya *F & K Enterprises* ambayo wanahisa wake ni ndugu Khalid Iddi Mabrouk, Mama Fatma Karume, Vuai Ame Vuai na ndugu Ramadhan Abdalla Songa ilikuwa inapewa kazi ya kusafisha eneo hilo. Baada ya Baraza kuukubali ushauri huo liliitaka Kampuni hiyo kuandaa *Build Operate Transfer (BOT)*, ili kuanza kazi ya ujenzi wa maduka kumi na tatu.

Kwa kuwa Kampuni kwa wakati ule ilikuwa haina fedha za kutosha za kuifanya kazi hiyo ilitafuta wafadhili wawili wa kugharamia kazi hiyo ambao ni ndugu Suleiman Msellem Nassor na ndugu Rashid Khalfan Ali. Baraza la Manispaa ndilo lililochora ramani ya eneo husika na kupata kibali cha Mamlaka ya Mji Mkongwe cha kujenga eneo hilo.

Ingawa ramani ya ujenzi ilirekebishwa na Mamlaka ya Mji Mkongwe na ujenzi huo kusimamiwa pia na Watendaji wa Mamlaka akiwemo ndugu Sabiha, na wajenzi wa maduka hayo kutakiwa na Mamlaka kuwalipa Watendaji hao, bado ujenzi wa maduka ulikuwa unakwenda kinyume na taratibu za ujenzi za Hifadhi ya Mji Mkongwe jambo ambalo liliipelekea Mamlaka hiyo mara kadhaa kurekebisha ujenzi huo kwa kuvunjwa maeneo hayo na kuelekeza namna inavyotakiwa kujengwa.

Kwa kuhakikisha hilo Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe alikuwa anatembelea eneo hilo kila wiki. Kutokana na sababu hiyo wajenzi walitumia gharama kubwa kinyume na walivyotarajia ambapo jumla ya shilingi 61, 000,000/= zilitumika badala ya shilingi 52, 000,000/=.

Halikadhalika, aliieleza kamati kuwa kabla ujenzi huo kufanywa wafanyabiashara waliokuwa wakitumia eneo hilo ambao jumla yao ni kumi na tatu (13) walipatiwa nafasi nyengine ya kufanyia shughuli zao na Mkurugenzi. Ujenzi wa maduka hayo kwa upande wa Baraza la Manispaa ulisimamiwa na Mkandarasi ndugu Abdulkadir Moh'd Khatib na Afisa Mipango Miji ndugu Khamis Mwalim Khamis.

Alieleza kwamba Kampuni ya *F & K* ilitakiwa na Baraza kujenga maduka hayo na kuwakodisha watu ili ijilipe fedha zake ndani ya miaka mitano na baada ya hapo maduka hayo yakabidhiwe kwa Baraza. Wakati kamati inapokea taarifa hii ni miaka miwili tangu maduka hayo yakamilike kujengwa.

Kwa kuwa Kamati haikuridhika na namna ndugu Vuai alivyokuwa akitoa maelezo yake, na kwa kuwa kamati ilikuwa tayari ina baadhi ya taarifa kuhusiana na kadhia hii, ilimtaka ndugu Vuai kuthibitisha taarifa ilizokuwa nazo. Baada ya kamati kuamua hivyo ndugu Vuai alitoa taarifa tofauti na zile alizozitoa awali baada ya kugundua kuwa kumbe Kamati tayari ina taarifa ambazo zina ukweli ndani yake.

Miongoni mwa taarifa hizo ni pamoja na kueleza kwamba hakukuwa na mkataba baina ya Wajenzi na Kampuni ya *F & K Enterprises* na badala yake mkataba ulifungwa baina ya Baraza la Manispaa na Wajenzi, ingawa, Baraza lilimpa Ndugu Vuai mamlaka ya kuwakodisha watu maduka hayo wakati maombi ya ukodishwaji yaliwasilishwa kwa Baraza.

Pia, alieleza kuwa ujenzi wa eneo hilo ulianza bila ya wajenzi kuwa na mkataba wowote. Aidha, wakodishwaji wa milango hiyo walilipa ada ya ukodishwaji ya miaka mitano kwa ndugu Ramadhan Abdalla (Songa) ambaye ni mwanahisa wa kampuni hii, jumla ya fedha hizo ni shilingi 30, 000,000/=, fedha ambazo zililipwa kabla ya maduka kumalizika na kabla yakufungwa mkataba na hatimaye aliondoka na fedha hizo.

Hata hivyo, hakuna risiti yoyote waliyopatiwa kwa malipo hayo waliyoyafanya. Hatimaye wakodishwaji hawa walipewa mikataba na Baraza ya ujenzi na ukodishwaji, jambo ambalo limepelekea pia wakodishwaji hawa kulipa asilimia Ishirini (20%) sawa na wajenzi.

Katika kupata ukweli wa kadhia hii Kamati ilikutana pia na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ambaye alieleza kwamba hakuna zabuni '*tender'* iliyoitishwa kuhusiana na ujenzi wa maduka kumi na tatu (13) katika Soko la Darajani. Isipokuwa, mjenzi ambaye ni Kampuni ya *F & K Enterprises* alipatikana na kwa njia ya '*Build Operated Transfer' (BOT)*.

Baada ya kauli hiyo kamati ilitaka kujua uhalali wa mikataba iliyofungwa baina ya Baraza la Manispaa na ndugu Rashid Khalfan Ali na ndugu Suleiman Msellem Nassor. Mkurugenzi alieleza kuwa mikataba hiyo ipo kimakosa kwa kuwa mjenzi ni Kampuni ya *F & K*.

Endapo kuna mtu yeyote aliyeathirika kutokana na ujenzi wa maduka hayo:

Mhe. Mwenyekiti, katika kufuatilia kadhia hii kamati ilitaka kujua kama kuna mtu au watu aliyeathirika au walioathirika kutokana na ujenzi wa maduka hayo. Kamati katika kuchunguza hilo ilikutana na wawakilishi wa wafanyabiashara waliokuwa wanatumia eneo hilo na walieleza kwamba wamekuwa wakilitumia eneo hilo tangu hapana majengo na baadaye walitakiwa na Baraza kujenga vibanda kwa gharama zao wenyewe. Baraza lilijenga kibanda kimoja na kila mfanyabiashara alitakiwa kujenga kibanda kwa kufuata ramani hiyo, jumla yao walikuwa ni kumi na tatu.

Mnamo mwaka 2010 walitakiwa na Baraza kuhama katika eneo hilo kwa kuwa linafanyiwa matengenezo, kwa masharti ya kuwa mfanyabiashara yeyote atakayehitaji eneo hilo basi apeleke barua ya maombi katika Baraza la Manispaa.

Wafanyabiashara wote waliomba kurejeshwa tena katika eneo hilo lakini hakukuwa na majibu yoyote ya barua zao walizopeleka Baraza la Manispaa, licha ya baadhi yao kupeleka barua za ukumbusho baada ya kuona siku nyingi zimepita bila ya mafanikio yoyote.

Walieleza kuwa pamoja na kumfuata afisini kwake Mkurugenzi wa Baraza mara nne hawakubahatika kuonana nae hata mara moja. Jambo hili liliwasababisha wapeleke malalamiko yao kwa viongozi mbali mbali wakiwemo Diwani wa Mkunazini katika Jimbo la Mji Mkongwe, Mstahiki Meya wa Baraza la Manispaa, Mkuu wa Soko la Darajani Ndugu Fadhil na wengi wengineo, hata hivyo, hakuna mafanikio waliyoyapata.

Kati ya wafanyabiashara kumi na tatu ni wafanyabiashara wawili tu waliopatiwa nafasi katika maduka hayo ambao ni Ndugu Othman Mwinyi Chande na Ndugu Issa Ali Kondo, lakini hawaelewi wameyapata kwa njia gani, ingawa maduka yote yalishakodishwa.

Wafanyabiashara hao baada ya kuona utaratibu uliotumika wa kujengwa maduka hayo walihisi kuwa maduka hayo hayatotumika tena kwa kuuza ndizi. Hivyo, walijiandaa kwa kufanya biashara nyengine na walikuwa tayari kulipa gharama zozote watakazoambiwa lakini hadi wanatoa taarifa hizi kwa Kamati mnamo tarehe 29 Septemba, 2012 wengi wao hawakubahatika kupata maduka hayo na kuishia kujibanabana kwa wafanyabiashara wengine.

Kitendo cha kuhamishwa katika eneo lile limefanya maisha yao kuwa magumu kutokana kushuka kwa biashara, kwani kwa yule aliyekuwa anauza mikungu ya ndizi kumi na tano sasa anauza mitano au chini ya hapo.

Muhtasari wa Mambo yaliyobainika na Kamati kufuatia Uchunguzi wa suala hili:

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kufuatilia kadhia hii Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

1. Shughuli ya ujenzi ilifanywa bila ya kutangazwa zabuni jambo ambalo ni kinyume na kanuni ya 55(b) ya Kanuni za Baraza la Manispaa na Sheria ya Mauziano na Uuzaji wa Mali za Umma, Namba 9 ya 2005.

2. Baraza la Manispaa limefunga mkataba wa ujenzi wa eneo hilo na watu mbali mbali ambao ni Kampuni ya *F & K Enterprises Limited*, Ndugu Rashid Khalfan Ali na Ndugu Suleiman Msellem Nassor pamoja na waliokodishwa maduka. Hivyo, Kamati ilishindwa kujua mjenzi halisi wa maduka hayo.
3. Kampuni ya *F & K* imesajiliwa kisheria, isipokuwa kwa mujibu wa kipengele cha 3(a) – (r) cha '*Memorandum of Association*' Kampuni hii haina jukumu la kufanya shughuli za usafi pamoja na shughuli za ujenzi.

4. Wajenzi wametumia gharama kubwa (zaidi ya walichokubaliana na Baraza la Manispaa), kinyume na makubaliano kutokana na maelekezo mabaya ya Mshauri wa Ujenzi wa Baraza la Manispaa Ndugu Abdulkadir.

5. Wajenzi hawakulipwa gharama za fedha ambazo wamezitumia.

6. Wakodishwaji wengine wamejazishwa mikataba kama wao ni wajenzi wa maduka hayo na wanalipa asilimia sawa na waliojenga. Kamati haikufanikiwa kuipata mikataba hiyo kwa kuwa Baraza la Manispaa imeikusanya mikataba hiyo kwa lengo la kuifanyia marekebisho.

7. Ugawaji wa maduka ya kujifidia wajenzi haukuzingatia idadi ya ujenzi wa maduka, wajenzi wote wamepewa maduka mawili, jambo ambalo ni kinyume na makubaliano yao.

8. Baraza la Manispaa lilishindwa kutimiza ahadi ya kuwapatia milango wafanyabiashara waliokuwa wanatumia eneo lile, yaani wauza ndizi.

9. Ujenzi wa maduka haya umekosesha baadhi ya wananchi ajira jambo ambalo limepelekea hali zao za maisha kuwa ngumu.

Hatua za Kuchukuliwa kutokana na matokeo ya uchunguzi huo.

Kamati inapendekeza mambo yafuatayo:

1. Kwa kuwa Ndugu Vuai alitoa maelezo yanayotofautiana mbele ya Kamati kwa lengo la kuipotosha Kamati hiyo na kuficha ukweli wa kiutendaji katika Baraza la Manispaa, tunapendekeza achukuliwe hatua za kisheria chini ya kifungu cha 22 cha Sheria Namba 4 ya 2007.

2. Kwa kuwa mikataba ya ujenzi ilitolewa na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa bila ya kufuata Sheria, Kamati inapendekeza kuwa Mkurugenzi huyo achukuliwe hatua za kisheria.

3. Baraza litimize ahadi yake ya kuwapatie eneo mbadala watumiaji wa eneo husika au kupatiwa mitaji wale wote wanaohamishwa ili wakaendeleze shughuli zao za kujipatia riziki.

4. Baraza la Manispaa liachane na tabia ya kujenga maduka ya kudumu katika masoko na badala yake ibakie dhana ya kuwa na masoko.

Utaratibu wa Ujenzi wa Maduka 16

Mhe. Mwenyekiti, maduka haya yalijengwa katika eneo lililokuwa likitumika kwa mnada wa viungo katika soko la mboga mboga baada ya kuwahamisha baadhi ya wafanyabiashara waliokuwa wakitumia eneo hilo.

Katika kufuatilia hili Kamati ilifanya mahojiano na Ndugu Ussi Ali Pandu ambaye alikuwa mtu wa mwanzo kuliomba Baraza la Manispaa kujenga maduka kumi na sita katika sehemu ya ndani ya Soko la Matunda Darajani.

Ndugu Ussi aliieleza Kamati kuwa alifunga mkataba na Baraza la Manispaa kuhusiana na ujenzi wa maduka hayo mnamo tarehe 20 Januari, 2009 wakati Baraza hilo lipo chini ya Mkurugenzi Mabrouk Jabu Walikubaliana na Baraza la Manispaa kujenga maduka hayo kwa gharama ya Tsh. 119, 033,200/- ambapo Mkodishwaji atapaswa kulipa kodi ya maduka hayo kwa asilimia Ishirini na Tano (25%) kwa Baraza la Manispaa na asilimia Sabini na Tano (75%) atajifidia gharama alizotumia.

Ndugu Ussi hakuanza shughuli za ujenzi kwa kuwa alikuwa analisubiri Baraza la Manispaa kuwaondosha wafanyabiashara waliokuwa wanatumia eneo lile. Hata hivyo, alianza kuchukua hatua mbali mbali kama vile ya kulipia kibali cha ujenzi Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe. Kwa kuwa Baraza lilishindwa kuwaondosha wafanyabiashara hao kwa wakati Mkodishwaji alilazimika kukata vibali vitatu tofauti ambavyo vilimgharimu Tsh. 1, 500,000/-

Vile vile, aliandaa michoro ya ramani mbili tofauti za ujenzi huo ambapo kila ya ramani ilimgharimu Tsh. 300,000/-. Ramani hizo zilikataliwa na Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe, cha kushangaza ramani hizo ndizo zilizotumiwa kujengwa maduka hayo.

Aliendelea kueleza kwamba baada ya kuteuliwa Mkurugenzi Rashid alipeleka barua ya ukumbusho lakini hakupata majibu yoyote.

Kamati ilikutana pia na mjenzi wa Maduka haya Ndugu Abdalla Thiney siku ya tarehe 08/06/2012 katika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi huko Mbweni kwa ajili kupata taarifa sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutoa maelezo yake Ndugu Abdalla alisema kwamba alijaribu kuomba eneo la Saateni kwenye Ushirika wa Zinamola mwaka 2005, kwa lengo la kufanya biashara na aliwahi kutumia baadhi ya gharama lakini hakufanikiwa kupata eneo hilo. Aliendelea na zoezi la kutafuta eneo na hatimae alipata taarifa kuhusu ujenzi wa Darajani katika eneo la mbogamboga. Alipeleka maombi ya ujenzi kwa Mkurugenzi Mabrouk Jabu lakini kabla ya kuanza kufunga mkataba akateuliwa Ndugu Rashid kuwa Mkurugenzi wa Baraza na baada ya uteuzi huo alimfuata ili kujua hatma yake. Baada ya siku chache kupita aliarifiwa kuwa Baraza la Manispaa limekubali kujengwa eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya Ndugu Abdalla kupewa eneo hilo kulikuwa na maombi ya mtu mwengine ambaye alielezwa kwamba alishindwa kuendeleza ujenzi ule ndio maana kapewa yeye. Kwa kuthibitisha hilo aliieleza Kamati kwamba Mkurugenzi wa Baraza (Ndugu Rashid) hakukubaliana na masharti ya mkataba uliokuwepo awali, hata hivyo, alielezwa na Ndugu Abdalla kwamba mkataba huo yeye hahusiki nao na aliliomba Baraza kufunga naye mkataba kwa masharti watakayokubaliana. Alikubaliana na Baraza kujenga maduka kumi na sita kwa jumla ya Tsh. 98, 047,000/- ambapo kila duka litagharimu Tsh. 6, 000,000/-. Mkataba huo ni wa miaka mitano ambapo atamlipa Mkodishaji (Manispaa) asilimia Ishirini na Tano (25%) ya kodi ya maduka hayo na asilimia Sabini na Tano (75%) atajilipa Mkodishwaji gharama zake.

Endapo kuna mtu yeyote ambae ameathirika kutokana na ujenzi wa maduka hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilitaka kujua kama kuna mtu au watu yeyote au wowote walioathirika kutokana na ujenzi wa maduka kumi na sita.

Katika kufuatilia hili Kamati ilielezwa na Mjenzi wa maduka hayo (Ndugu Abdalla Thiney) kwamba Baraza la Manispaa iliwaita wafanyabiashara waliokuwa wanatumia eneo lile kwa madhumuni ya kuwapangia eneo jengine. Pamoja na juhudi hiyo ni wafanyabiashara wachache tu ndio walioitikia wito huo na kupangiwa eneo linalotumiwa na mamantilie. Kwa kuwa mazingira ya eneo walilopelewa wafanyabiashara hao lilikuwa sio la kuridhisha, mjenzi huyu aliamua kusaidia ujenzi wa eneo lile ingawa sio jukumu lake. Lengo la kufanya hivyo ni kuepuka mizozo isijitokeze hapo baadae.
Kamati haikuridhika na maelezo ya upande mmoja tu na ilikutana na wawakilishi wa wafanyabiashara waliokuwa wanatumia eneno lile na walieleza kwamba, baadhi yao walikuwa wanafanya shughuli zao Sokoni hapo tangu mwaka 1983. Mnamo mwaka 1988walihamishiwa eneo jengine ambalo lilikuwa chafu na wakaamua kulisafisha eneo lile kwa gharama zao kwa kuweka zege ili kunusuru maisha ya walaji. Kwa kuwa eneo lile halikuwa na jengo lolote waliomba kujenga mabanda mawili ili kujihifadhi na jua na mvua.

Wafanyabiashara hao walieleza kwamba katika mwaka 2005 walipatiwa barua ya kuhama na Baraza la Manispaa kwa wale wote wanaotumia kuanzia eneo la wauza kuku hadi mwisho kwa kuwa hawana mikataba na kwa wale wenye mikataba waende Baraza la Manispaa kwa maelekezo zaidi. Wafanyabiashara hao hawakukubaliana na maamuzi hayo na walipeleka malalamiko yao kwa aliyekuwa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Amani Karume pamoja na vyombo mbali mbali vya habari. Kutokana na maamuzi hayo waliyochukua Baraza la Manispaa lilisitisha zoezi lile na mnamo mwaka 2009 Baraza likaamua kuwahamisha wafanyabiashara hao ambao jumla yao ni kumi na nane. Kwa kuwa hali ya Soko haikuwa nzuri hawakuwa na pingamizi wala mashaka na utengenezwaji ule. Kutokana na muundo wa maduka yale wakavunjika moyo na kuona kuwa hawatokuwa tena na kazi, kwa kuwa hawana uwezo wa kulipa kodi.

Kamati ilimhoji pia Mkurugenzi wa Baraza ambaye aliieleza Kamati kwamba hakuna mtu au watu walioathirika na ujenzi ule, isipokuwa waliokuwa wanatumia eneo lile ni mamantilie ambao walipatiwa eneo jengine.

Muhtasari wa Mambo yaliyobainika na Kamati kufuatia
Uchunguzi wa suala hili:

Katika kadhia hii Kamati imebaini mambo yafuatayo;-

1. Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa alishindwa kutekeleza matakwa ya kifungu cha 29(2) cha Sheria Namba 3 ya 1995 kinachomtaka aendeleze mikataba halali aliyoirithi.

2. Maeneo yaliyokuwa na Masoko hujengwa majengo ya kudumu (Maduka) jambo ambalo huondosha dhamira ya kuwa na Masoko.

3. Baadhi ya vipengele vya mkataba havikujazwa.

4. Kipengele cha 14(c) cha Mkataba kinachoeleza kwamba Mkodishwaji (Mjenzi) akodishe maduka kwa watu wengine kwa makubaliano na Mkodishaji (Manispaa) hakifuatwi. Hii ni kutokana na kuwa Mkodoshwaji amewakodisha watu bila ya kutoa taarifa kwa Mkodishaji.

5. Shughuli ya ujenzi imetolewa bila ya kufuatwa utaratibu wa zabuni jambo ambalo ni kinyume na kanuni ya 55(b) ya Baraza la Manispaa pamoja na Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Umma.

6. Ujenzi wa maduka haya umewawakosesha ajira wananchi na baadhi yao kubakia kutangatanga mitaani na wengine kujibana kwa wenzao na kupelekea kushuka kwa shughuli za biashara.

7. Baraza lilishindwa kutimiza ahadi iliyoitoa kwa wafanyabiashara waliokuwa wanatumia eneo lile.

Maoni ya Kamati kutokana na matokeo ya uchunguzi huo.

Kamati inapendekeza yafuatayo;-

1. Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa achukuliwe hatua za kinidhamu kwa kutofuta Sheria za nchi.

2. Baraza la Manispaa limlipe gharama alizotumia Ndugu Ussi Ame Pandu wa SLP 318 kwa mujibu wa thamani ya soko. Sambamba na hilo, Baraza la Manispaa limlipe fidia Ndugu Ussi kwa usumbufu alioupata.

3. Baraza litimize ahadi yake ya kuwapatie eneo mbadala watumiaji wa eneo husika au kupatiwa mitaji wale wote wanaohamishwa ili wakaendeleze shughuli zao za kujipatia riziki.

4. Baraza la Manispaa liachane na tabia ya kujenga maduka ya kudumu katika masoko na badala yake ibakie dhana ya kuwa na masoko.

Bustani ya Jamhuri

Kamati ilitaka kujua namna mkodishwaji alivyopata nafasi ya kukodishwa eneo la Bustani ya Jamhuri.

Kamati ilibahatika kuonana na Mkodishwaji wa bustani ile Bi Asya Mohammed Bafadhili ambaye aliiomba Kamati ashirikishwe na mumewe Ndugu Ali Abdalla Ali (Kibasi) kwa kuwa yeye ndiye anayeyajua mambo hayo kwa kina ingawa mkataba alifunga yeye. Kwa kuwa lengo la Kamati ni kupata taarifa za uhakika haikuwa na pingamizi na ombi hilo.

Katika kutoa maelezo yao walieleza kwamba chimbuko la kutaka kulitengeneza eneo lile ni baada ya kutengeneza Bustani ya Forodhani na wananchi wengi kuonesha hamu ya kuitumia bustani hiyo. Kutokana na hilo walihisi kumbe wananchi wanahitaji huduma ile.

Kwa kuwa eneo la Forodhani lilikuwa ni dogo, na kwa kuwa walikuwa wana baadhi ya vifaa ambavyo havijatumika kwa ajili hiyo, na kwa kuwa waliwahi kutoa huduma kama hiyo kwa Jumuiya ya Agakhan Foundation kwa wageni wao kutoka Jumuiya ya Al – Ismailia, Bi Asya aliliomba Baraza la Manispaa kupatiwa eneo lile ili atengeneze kiwanja cha kufurahishia watoto.

Walizidi kuieleza Kamati kwamba matengenezo ya Bustani ile yangegharimu Tsh. 160, 000,000/-, lakini Baraza likapunguza hadi Tsh. 96, 374,000/-, kwa maelezo kwamba mikataba ya Serikali ya ukodishaji haizidi miaka 10 na kwa kiwango hicho (Tsh. 160, 000,000/-) wangekodishwa kwa miaka 30. Kwa kuwa Mkodishwaji keshatumia gharama zake mbali mbali alikubaliana na maamuzi ya Baraza ingawa kiasi hicho hakikuwa na tija kwa upande wake. Kwa msingi huo, alitakiwa na Baraza kukodishwa eneo lile kwa Tsh. 1, 000,000/- kwa mwezi ambapo atalipa Tsh. 100,000/- kwa Baraza na kiwango kilichobaki (Tsh. 900,000/-) atajilipa gharama zake alizotumia. Eneo hilo limekodishwa kwa miaka minane kuanzia tarehe 1 Novemba, 2010

Wakodishwaji hawa waliendelea kueleza kwamba wanalipa leseni ya biashara Tsh. 400,000/- kwa mwaka. Baada ya kumalizika mkataba huo wa miaka minane na wakiona hawana hamu ya kuendelea na biashara ile wataondoka na vifaa vyao.

Kwa kuwa lengo la mkodishwaji ni kuona kwamba watoto wote wanapata sehemu ya kuchezea kwa zile siku za sikukuu waliliomba Baraza la Manispaa kuwapatia eneo jengine ambalo yatari wameshalitengenza kwa kuweka miundo mbinu mbali mbali kama vile taa, maji, milango, mabao ya kukalia, pia walipanda miti na gharama nyingi nyenginezo. Baraza lilikubali kutoa eneo hilo kwa makubaliano kwamba kila siku alipe Tsh. 100,000/-, hivyo, kwa sikukuu nne analipa Tsh. 400,000/-.

Vile vile, walieleza kwamba eneo lile linawagharimu fedha nyingi sana kwa kuwa wametakiwa kuweka taa na kulipia gharama za umeme eneo lote, ili kuepuka vitendo vya uhalifu, pia, wameajiri vijana 50 ambao wanafanya shughuli mbali mbali zikiwemo za usafi, kuhakikisha eneo linakuwa salama. Vijana hawa wanalipwa Tsh. 80,000/- kwa kila mwezi. Pia, wananunua maji ambayo yanawagharimu kwa kila siku Tsh. 40,000/- kwa ajili ya bustani na kwa siku za sikukuu huajiri vijana wakiwemo Polisi Jamii sio chini ya 50 kwa lengo la kulinda usalama katika eneo lile.

Kwa kuwa wanatumia gharama kubwa kinyume na walivyotarajia, na kwa kuwa kipato kinachopatikana ni kidogo hasa tukizingatia kuwa biashara kubwa hufanyika zaidi siku za sikukuu ukilinganisha na siku za kawaida, mambo yote haya yamepelekea hata baadhi ya miezi kushindwa kuwalipa wafanyakazi wao ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hii ripoti ambayo Mwenyekiti anaisoma imebakia kidogo sana ili aweze kumaliza. Sasa tungeomba basi Waziri wa Katiba na Sheria tuongoze katika hili ili tuweze kuongeza muda na tumalize hii ripoti ili kesho tuje kwa mambo mengine.

TAARIFA

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nitumie kifungu cha 64 cha Kanuni. Kwa sababu mtoa hoja nahisi kama kifua chake ni kigonjwa na kwa sababu bado kurasa nyingi kidogo kumalizika. Na kwa sababu kuna watu wengi waliofunga katika Mwezi huu Mtukufu. Na kwa sababu unao uwezo wa kumtaka mtoa hoja kufanya *summary* ya maelezo yake.

Naomba kutoa hoja kwamba tuakhirishe Baraza lako mpaka kesho na umtake mtoa hoja afanye *summary* ya maelezo ili kesho aje amalize. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa nichukue fursa hii kukushukuruni kwa namna tulivyoweza kushirikiana hadi kufikia hapa kwa siku ya leo na tutalaza shughuli zetu hizi hadi kesho siku ya Jumaane tarehe 23/10/2012 Saa: 3:00 za asubuhi. Baada ya maelekezo hayo naomba kuakhirisha Baraza.

(Saa 1:38 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 23/10/2012 saa 3.00 asubuhi)